# Kiswahili

## Kwa Vyuo Vya Ualimu(TTC)

Kitabu Cha Mwanafunzi

3

MCHEPUO WA ELIMU YA LUGHA (LE)

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya  Bodi ya Elimu Rwanda.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# VIFUPISHO

**agh**: aghalabu

**Bi**: Bibi

**Bw**: Bwana

**k.v**: kama vile

**mf**: mfano

**S.L.P**: Sanduku la Posta.

**n.k**: nakadhalika

**tnbh**: tanbihi

## DIBAJI

Mwanafunzi mpendwa**,**

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima ya kuwasilisha Kitabu cha Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa tatu, Mchepuo wa Elimu ya lugha katika vyuo vya ualimu.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri maisha yake na kumpa fursa ya kujipatia ajira au kuandaa miradi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii anamoishi.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza kuhusu umuhimu wa kufungamanisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji pamoja na zana na mitaala ili kufanikisha mchakato mzima wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale yanayofundishwa na uwezo waupatao wanafunzi. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Hivyo basi, kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza unaokuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti ya kibinafsi na yale utakayofanya katika makundi kwa msaada wa wakufunzi ambao huwajibika kufanikisha ufundishaji. Aidha, utapata stadi muhimu zitakazokuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha halisi ili uweze kuonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Mwelekeo uliozingatiwa katika kitabu hiki unatofautiana na ule uliotiliwa maanani katika mfumo wa zamani ambapo mchakato wa kujifunza ulifanywa kwa kutilia mkazo upataji wa maarifa kutoka kwa mkufunzi ambaye pia alifikiriwa kumzidi mwanafunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi. Kwa hivyo, dhana huanzishwa aghalabu kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na kupata maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya ujifunzaji hujihusisha na shughuli mbalimbali zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri kuhusu yale anayoyafanya, kuonyesha uzoefu wake halisi na maarifa aliyo nayo katika mchakato huo wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, utakuwa na majukumu yafuatayo ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi, mazoezi yanayolenga kwenye mada. Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kupitia mawasilisho, mijadala, kazi za makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, mitandao na hata nje ya shule.
- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti.
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi ulizopewa kupitia maelezo na majadiliano kila unapoongea hadharani.
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi yako ya ujifunzaji.

Mwishowe, ningependa kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wao kwa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioongoza mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Elimu Rwanda katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

## YALIYOMO

**VIFUPISHO** ........................................................................................................iii
**DIBAJI** ................................................................................................................iv
**SHUKRANI** .........................................................................................................vi
**UTANGULIZI**.........................................................................................................1
**MADA YA 1: UFAHAMU NA UFUPISHO** ....................................................3
SOMO LA 1: UFAHAMU ....................................................................................4
1.1. Kusoma na Ufahamu: Miti ..........................................................................4
1.2. Msamiati kuhusu Kifungu ..........................................................................5
1.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno ..................................................................6
1.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Ufahamu ...................... 10
1.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................................ 11
1.6. Kuandika .................................................................................................... 11
SOMO LA 2: UFUPISHO.................................................................................... 12
2.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ................................................................... 12
2.2. Msamiati kuhusu Hotuba ........................................................................... 14
2.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno .................................................................. 15
2.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Ufupisho ...................... 23
2.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................................ 25
2.6. Kuandika .................................................................................................... 25
**MADA YA 2: UTUNGAJI WA BARUA RASMI** ..........................................26
SOMO LA 3: MWONGOZO WA KUTUNGA BARUA RASMI/KIKAZI.. 27
3.1. Kusoma na Ufahamu: Baruaya Kuomba Kazi........................................ 27
3.2. Msamiati kuhusu Barua ............................................................................ 28
3.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi rejeshi -po-............................................. 29
3.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Uandishi wa Barua Rasmi ... 31
3.5. Kusikiliza na kuzungumza......................................................................... 35
3.6. Kuandika .................................................................................................... 36

SOMO LA 4: MIFANO YA BARUA RASMI .......... 36
4.1. Kusoma na Ufahamu: Barua ya Kuomba Ruhusa .......... 36
4.2. Msamiati kuhusu Barua ya Kuomba Ruhusa .......... 37
4.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi Rejeshi -PO- .......... 38
4.4. Matumizi ya Lugha : Mifano ya Barua Rasmi .......... 39
4.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 41
4.6. Kuandika: Utungaji .......... 41
**MADA YA 3: UTUNGAJI WA INSHA..........43**
SOMO LA 5: MAANA YA INSHA .......... 44
5.1. Kusoma na Ufahamu: Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu .......... 44
5.2. Msamiati kuhusu kifungu .......... 46
5.3. Sarufi: Matumizi ya Alama za Vituo .......... 47
5.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu utungaji wa insha .......... 52
5.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 54
5.6. Kuandika .......... 54
SOMO LA 6: INSHA ZA MASIMULIZI .......... 55
6.1. Kusoma na Ufahamu: Mafanikio ya Kudumu .......... 55
6.2. Msamiati kuhusu Mafanikio ya kudumu .......... 57
6.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Maneno .......... 58
6.4. Matumizi ya lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Insha za Masimulizi .......... 64
6.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 65
6.6. Kuandika .......... 65
SOMO LA 7: INSHA ZA KUBUNI .......... 66
7.1. Kusoma na Ufahamu: Kioja katika Mbuga ya Mwangaza .......... 66
7.2. Msamiati kuhusu Kifungu .......... 68
7.3. Sarufi: Mnyumbuliko wa Vitenzi .......... 69
7.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Insha za Kubuni .......... 72
7.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 73
7.6. Kuandika .......... 73

**MADA YA 4: HOTUBA ......................................................................................... 75**

SOMO LA 8: MAANA YA HOTUBA ................................................................ 76

8.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Afisa wa Umoja na Maridhiano wilayani kwa Wananchi ....................................................................... 76

8.2. Msamiati kuhusu Hotuba ............................................................................ 78

8.3. Sarufi: Kueleza Tofauti kati ya Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa 78

8.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Hotuba ......................... 80

8.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................................ 82

8.6. Kuandika ...................................................................................................... 82

SOMO LA 9: MUUNDO WA HOTUBA ......................................................... 82

9.1. Kusoma na Ufahamu: Kazi ni Kazi ........................................................... 82

9.2. Msamiati kuhusu Hotuba ya Katibu Mtendaji ........................................ 84

9.3. Sarufi: Tofauti kati ya Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa ................. 85

9.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo muhimu Kuhusu Muundo wa Hotuba . 86

9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Hotuba .......................................................... 87

9.6. Kuandika: Ufupisho wa Hotuba ................................................................ 88

**MADA YA 5: UANDISHI WA RIPOTI ............................................................ 89**

SOMO LA 10: MAANA YA RIPOTI ................................................................ 90

10.1. Kusoma na Ufahamu: Ziara ya Kielimu ................................................. 90

10.2. Msamiati kuhusu Ripoti ............................................................................ 92

10.3. Sarufi: Vipashio vya Tungo za Kiswahili ................................................ 93

10.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu Kuhusu Ripoti ......................... 95

10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ................................................. 97

10.6. Kuandika ..................................................................................................... 97

SOMO LA 11: MAANDALIZI YA RIPOTI ...................................................... 98

11.1. Kusoma na Ufahamu: Ripoti ya Maandalizi ya Mafunzo ya Elimu Jumuishi .................................................................................................... 99

11.2. Msamiati kuhusu Mfano wa Ripoti ya Mafunzo Jumuishi ...............101

11.3. Sarufi: Vipashio vya tungo ......................................................................102

11.4. Matumizi ya Lugha: Maandalizi ya Ripoti ..........................................104

11.5. Kusikiliza na Kuzungumza ......105
11.6. Kuandika ......105
**MADA YA 6: UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI ...... 107**
SOMO LA 12: MAANA YA UHAKIKI......108
12.1. Kusoma na Ufahamu: Siku Njema Huonekana Asubuhi ......108
12.2. Msamiati kuhusu Kifungu ......110
12.3. Sarufi: Aina za Maneno ya Kiswahili ......111
12.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu Kuhusu Uhakiki wa Tanzu za Fasihi Simulizi ......118
12.5. Kusikiliza na Kuzungumza ......122
12.6. Kuandika ......122
SOMO LA 13: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI......123
13.1. Kusoma na Ufahamu: Kobe na Kijumbamshale ......123
13.2. Msamiati kuhusu Kobe na Kijumbanshale ......125
13.3. Sarufi: Aina za Maneno ya Kiswahili ......127
13.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Uhakiki wa Hadithi za Masimulizi ......130
13.5. Kusikiliza na Kuzungumza ......136
13.6. Kuandika ......137
**MADA YA 7: TANZU ZA FASIHI ANDISHI ...... 138**
SOMO LA 14: FASIHI ANDISHI NA DHIMA YAKE KATIKA JAMII ......139
14.1. Kusoma na Ufahamu: Mwangaza wa Maisha ......139
14.2. Matumizi ya msamiati ......142
14.3. Sarufi: Maana ya tungo......142
14.4. Matumizi ya lugha: Fasihi andishi na dhima yake katika jamii ......145
14.5. Kusikiliza na Kuzungumza ......146
14.6. Kuandika ......147
SOMO LA 15: TANZU ZA FASIHI ANDISHI......147
15.1. Kusoma na Ufahamu: Akili ni Mali......148
15.2. Matumizi ya msamiati ......150

15.3. Sarufi: Aina za tungo katika Kiswahili ........ 150
15.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Tanzu za Fasihi Andishi ........ 152
15.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 157
15.6. Kuandika ........ 157
**MADA YA 8: UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI ........ 159**
SOMO LA 16: MAANA YA UHAKIKI NA DHIMA ZAKE ........ 160
16.1. Kusoma na Ufahamu: Uhakiki kama Kazi ya Kitaalamu ........ 160
16.2. Matumizi ya Msamiati ........ 163
16.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Rejeshi – ye - ........ 164
16.4. Matumizi ya Lugha: Dhima za Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi na Nafasi ya Mhakiki ........ 165
16.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 166
16.6. Kuandika ........ 166
SOMO LA 17: TARATIBU ZA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI ........ 167
17.1. Kusoma na Ufahamu: Uhakiki wa Fani na Maudhui ........ 167
17.2. Matumizi ya Msamiati ........ 169
17.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi rejeshi – o – katika Majina ya Ngeli ya A-WA, LI-YA na KI-VI ........ 170
17.4. Matumizi ya lugha: Mwongozo katika uhakiki wa kazi za fasihi andishi.... 171
17.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 175
17.6. Kuandika ........ 176
SOMO LA 18: MFANO WA UHAKIKI WA TAMTHILIA ........ 176
18.1. Kusoma na Ufahamu: Muhtasari wa Hawala ya Fedha ........ 176
18.2. Matumizi ya Msamiati ........ 178
18.3. Sarufi: Matumizi ya kirejeshi – o – katika majina ya ngeli ya U-I na U-ZI 178
18.4. Matumizi ya lugha: Uhakiki wa Tamthilia ........ 179
18.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 184

18.6. Kuandika ........................................................................................184

SOMO LA 19: MFANO WA UHAKIKI WA HADITHI FUPI ....................185

19.1. Kusoma na Ufahamu: Kila Mtoto na Koja Lake ................................185

19.2. Matumizi ya Msamiati ................................................................187

19.3. Sarufi: Matumizi ya kirejeshi – o – katika Majina ya Ngeli ya U- na PA-M-KU ........................................................................................188

19.4. Matumizi ya lugha: Uhakiki wa Hadithi Fupi......................................189

19.5. Kusikiliza na Kuzungumza ..........................................................192

19.6. Kuandika ........................................................................................192

**MAREJEO ......................................................................................... 194**

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda na hata katika jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa mwaka wa tatu katika vyuo vya ualimu nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki imegawanywa katika mada masomo ambapo kila somo limegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Matumizi ya lugha
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia na elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza

uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa muda mrefu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili nchini Rwanda. Kwa hiyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki kwa kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# MADA YA 1

# UFAHAMU NA UFUPISHO

## Uwezo mahususi

Kufupisha matini zenye urefu wowote kulingana na kanuni zinazohusika.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani,
- Kuonyesha dhamira kuu au kiini cha habari kinachozungumziwa,
- Kupanga mawazo muhimu yaliyozungumziwa katika matini,
- Kubainisha mbinu au taratibu za ufupisho,
- Kubainisha sifa za ufupisho,
- Kuonyesha umuhimu wa ufupisho,
- Kufupisha matini mbalimbali za Kiswahili kulingana na taratibu au mbinu za ufupisho,
- Kuambisha maneno ya Kiswahili.

## Kidokezo

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini**



1. Wahusika wanaoonekana kwenye mchoro huu wanafanya nini?
2. Kazi hizo zilizotajwa katika swali la kwanza hufanyika Jumamosi ya mwisho wa mwezi katika………………………………..

# SOMO LA 1: UFAHAMU

## 1.1. Kusoma na Ufahamu: Miti

**Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini**

Miti ina faida nyingi. Si kwa binadamu tu bali hata kwa wanyama, ndege, wadudu na viumbe wa baharini. Kuna miti inayotoa vyakula kwa watu na kwa wanyama. Miti hiyo ni kama michungwa, mipapai, milimau, mipea, mikanju, miwa, fito na kadhalika. Miti mingine hutupatia vifaa vya kukidhi mahitaji yetu. Vifaa hivyo ni kama samani yaani meza, makabati, viti, madawati na vifaa vingine kama vinu, michi, mipini ya majembe na mashoka, mivure na kadhalika. Miti hiyo ni kama mivule, mikalitusi, misonobari na mikangazi. Baadhi ya miti hutupa dawa za kutibu magonjwa mbalimbali.

Halikadhalika, miti hutupa mvua na kutuepusha na jangwa. Miti pia ni kuni na makaa ya kupikia vyakula. Na miti hutumiwa kwa kujengea mapaa ya nyumba. Vilevile, miti ni mapambo ya mazingira.

Kwa kuona faida na umuhimu wa miti, watu duniani walitenga siku maalum, kila mwaka, ya kupanda miti. Nchi yetu nayo haikubaki nyuma kama mkia bali nayo hushiriki kikamilifu katika shughuli ya upandaji wa miti. Mbali na siku hiyo maalum, serikali yetu inahamasisha raia kupanda miti. Jambo hili, hufanyika katika misaragambo au katika hafla mbalimbali. Kulingana na jambo hili Wanyarwanda wana msemo usemao "*Ukikata mmoja (mti), panda miwili.*" Isitoshe, serikali ya Rwanda ilitunga sheria za kuzuia uharibifu wa misitu. Uharibifu huu unahusiana na ukataji wa miti kwa kutafuta kuni, kuchoma makaa na hata kuchoma misitu na vichaka kwa utafutaji wa malisho ya mifugo. Ikumbukwe kuwa misitu ni makazi ya ndege na wanyama wa porini. Misitu hii ikiharibika kutokana na ukataji wa miti ndege na wanyama hawa watakosa vyakula na mahali pa kuishi.

Miti ikiendelea kukatwa ovyo bila ya kupanda mingine ama misitu ikiendela kuharibiwa, mazingira yetu hayatakuwa safi. Nchi yetu Itakosa mvua na hata dunia nzima itageuka jangwa. Ni wajibu wetu wa kulinda mazingira kwa kupanda miti na kutoikata ovyo ili tusikumbane na madhara yatakayotokana na kuchafuka kwa hali ya hewa. Sababu ni kwamba miti ina umuhimu mkubwa katika maisha ya hapa duniani.

KAZI 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Kifungu hiki kinazungumzia juu ya nini?
2. Miti ina uhumimu gani kwa watu?
3. Ni kipi kilichofanyika duniani baada ya kutambua umuhimu wa miti?
4. Wanyarwanda wana msemo gani kuhusiana na ukataji wa miti?
5. Wajibu wetu ni upi kulingana na kifungu hiki?

## 1.2. Msamiati kuhusu Kifungu

KAZI 2

**Eleza maneno yafuatayo:**

a) Samani
b) Mivure
c) Mazingira
d) Malisho
e) Jangwa

KAZI 3

**Tafuta majina kumi ya miti kwenye mraba ufuatao:**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | M | B | U | Y | U | V | M |
| U | P | O | L | E | F | Z | C |
| W | E | A | U | Y | I | R | H |
| A | A | S | P | E | T | I | O |
| S | I | M | B | A | O | K | N |
| I | M | B | U | N | I | W | G |
| M | K | O | R | O | S | H | O |
| M | N | A | Z | I | T | I | M |
| M | U | Y | W | A | O | F | A |
| M | C | H | U | N | G | W | A |

## 1.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno

### KAZI 4

**Chunguza maneno yaliyopigiwa mstari kisha ueleze mabadiliko utakayoyaona**

- Kamali **alipanda** miti mingi.
- Miti mingi **ilipandwa** na Kamali.
- Serikali yetu **ilipandisha** miti mingi.
- Kamana ni **mpandaji** wa miti.
- **Upandaji** wa miti husaidia hali ya hewa kuwa nzuri.
    - **Alipanda, ilipandwa, ilipandisha:** Ni vitenzi vinavyotokana na kitenzi kupanda
    - **Mpandaji na upandaji:** Ni nomino zinazotokana na kitenzi kupanda.
    - Mabadiliko yanayojitokeza yalisababishwa na mbinu iitwayo « **Uambishaji**. »

**Maelezo muhimu kuhusu uambishaji**

Uambishaji ni mbinu ya kuzalisha maneno mapya kutoka maneno mengine. Mbinu hii hufanyika kwa kuongeza kwenye sehemu fulani (viini, mizizi au mashina) za maneno hayo viambishi mbalimbali mwanzoni au mwishoni. Mbinu hii huitwa tena mnyambuliko. Katika sarufi ya lugha ya Kiswahili kuna :

- Uambishaji wa vitenzi
- Uambishaji wa nomino
- Uambishaji wa vielezi
    - **Uambishaji wa vitenzi**

Uambishaji wa vitenzi ni uundaji wa vitenzi vipya kutoka maneno mengine. Kuna :

- Uambishaji wa vitenzi kutoka vitenzi vingine
- Uambishaji wa vitenzi kutoka majina
- Uambishaji wa vitenzi kutoka vivumishi
- Uambishaji wa vitenzi kutoka vielezi

### i) Uambishi wa vitenzi kutoka vitenzi vingine

Uundaji huu wa vitenzi vipya hufanyika kwa kuongezea mzizi wa kitenzi viambishi tamati vya kauli au vya hali. Ni kusema kuwa tunachukua kitenzi katika kauli ya kutenda na kukitia katika kauli nyingine.

**Mifano:**

| Kauli ya kutenda | Kauli ya kutendea -il- | Kauli ya kutendesha -ish-/-y-/ | Kauli ya kutendana -an- | Kauli ya kutendua -ul- | Kauli ya kurudia -il-il-ang- | Kauli ya kutendeka -ik- | Kauli ya kutenduka -uk- | Kauli ya kutendwa - w- |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| piga | pigia | pigisha | pigana | - | pigilia | pigika | - | pigwa |
| finya | finyia | finyisha | finyana | - | finyanga | finyika | - | finywa |
| funga | fungia | fungisha | fungana | fungua | fungilia | fungika | funguka | fungwa |
| funda | fundia | fundisha | fundana | - | fundilia | fundika | - | fundwa |
| | | | - | - | | | | |

## KAZI 5

**Jaza jedwali lifuatalo**

| Kauli ya kutenda | Kauli ya kutendewa | Kauli ya kutendeshwa | Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeana |
|---|---|---|---|---|
| | imbiwa | | | |
| Cheza | | | | |
| | | | | someana |
| | | vushwa | | |
| | | | Pimia | |

## KAZI 6

**Tia vitenzi vilivyo mabanoni katika kauli mwafaka**

1. Gari lili……….na dereva bingwa (enda).
2. Mpishi ali….moto ndipo akapika (waka).
3. UKWIMWI kweli unatu….. (ogopa).
4. Sijui kwa nini aliku………mzigo huo (beba).
5. Mbona unataka kutu………katika mashaka (ingia)?

### ii) Uambishaji wa vitenzi kutoka majina

Uundaji wa vitenzi kutoka majina hufanyika kwa kuongeza kwenye shina la jina kiambishi awali **ku**- na viambishi tamati (viambishi vya kauli na viishio).

**Mifano:**

| Jina | Kitenzi |
|---|---|
| dhana | Kudhani: ku- dhan-i<br><br>Kudhaniwa: ku-dhan-iw-a |
| Fedheha | Kufedheheka: ku-fedheh-ik-a<br><br>Kufedhehesha: ku-fedheh- ish-a<br><br>Kufedheheshwa: ku-fedheh-il-ish-w-a |
| Sala | Kusali: ku-sal-i<br><br>Kusalia : ku- sal-il-a |
| Mzozo | Kuzozana : ku-zoz-an-a<br><br>Kuzozania: ku- zoz-an-il-a |

**KAZI 7**

**Unda vitenzi kutoka majina yafuatayo**

Hesabu

Adhabu

Ahadi

Safari

Sababu

### iii) Uambishaji wa Vitenzi kutoka Vivumishi

Uundaji wa vitenzi kutoka vivumishi hufanyika kwa kuongezea shina la kivumishi kiambishi awali **ku**- na viambishi tamati (vya kauli na viishio).

**Mifano:**

| Kivumishi | Kitenzi |
|---|---|
| Refu | Kurefusha: ku-refu-sh-a<br><br>Kurefuka: ku-refu-k-a |
| Pana | Kupanua: ku-pan-ul-a<br><br>Kupanuliwa: ku-pan-ul-il-w-a |
| Chafu | Kuchafuliwa: ku-chaf-ul-il-w-a |
| Duni | Kudunisha : ku-dun-isha |

## KAZI 8

**Unda vitenzi kutoka vivumishi vifuatazo**

Bora

Safi

Imara

Halali

Pevu

### i) Uambishaji wa vitenzi kutoka vielezi

Uambishaji wa aina hii hufanyika kwa kuongeza kwenye kielezi au sehemu ya kielezi kiambishi awali **ku**- na viambishi tamati (viambishi vya kauli na viishio).

**Mifano:**

| Kielezi | Kitenzi |
|---|---|
| Karibu | Kukaribisha: ku-karib-ish-a |
| Sawa | Kusawazishwa: ku-sawa-al-y-ish-w-a |

## KAZI 9

**Tafuta mifano mingine ya vitenzi vilivyoundwa kutoka vielezi.**

## 1.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Ufahamu

**KAZI 10**

**Soma maelezo hapo chini kisha ujibu maswali husika**

Ufahamu ni neno ambalo linatokana na kitenzi "kufahamu." Yaani kujua, kutambua na kuelewa unachosoma au unachoambiwa. Ufahamu ni dhana inayolenga kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya bila kupotosha maana yake ya awali. Ufahamu ni somo la kupata mbinu zote za kuelewa mambo tunayosikia au tunayosoma.

Ufahamu unaweza kufanyika kwa kusikiliza yanayosemwa au kwa kusoma yaliyoandikwa. Kwa hiyo, kuna aina kadhaa za ufahamu: ufahamu wa kusoma, ufahamu wa kusikiliza, ufahamu wa kutazama na kusikiliza (runinga au filamu) na ufahamu wa kutazama tu (picha za filamu au video ambazo hazina sauti).

Tunapozungumza au tunaposoma maandishi fulani ni lazima tuelewe na kuelewana. Kuelewa mambo yanayosemwa na mtu mwingine ni hatua ya kwanza. Hatua ya pili ni kuweza kupata ukweli wa yale yanayosemwa na kuyakubali au kuyakana. Hatua ya tatu ni kujenga uhusiano na uelewano kati ya hao wawili wanaozungumza.

Ili mtu aweze kufahamu anayoambiwa au anayoyasoma, au tunayoyatazama kuna mbinu anazopaswa kutumia. Mbinu hizo ni hizi zifuatazo:

a) Kujua ujumbe wa maandiko mazima au mazungumzo. Hili hufanyika kwa kusoma vizuri kwa kuzingatia matumizi ya alama za vituo. Katika mazungumzo msikilizaji anapaswa kusikiliza vizuri kwa kuzingatia matamshi ya msemaji.

b) Kuelewa maana za maneno na misemo tofauti: msomaji au msikilizaji anatakiwa kubaini maana ya maneno hayo ili kuelewa vema maana ya maneno aliyoyatumia mwandishi au msimuliaji.

c) Kuchunguza mawazo makuu na yale madogo madogo katika maandiko hayo au masimulizi hayo kwa kujenga ujumbe.

d) Kuelewa utanzu anaousoma au anaousikiliza: Anapokuwa na makini kuhusu utanzu anaousoma au anaousikiliza, ndipo msomaji au msikilizaji anaelewa vizuri jambo analolisoma au analolisikiliza.

Ufahamu una umuhimu mkubwa kwa kuwa ni fursa njema ya kupanua msamiati. Kutokana na kuwa mwandishi au msemaji hutumia hasa maneno na misemo mbalimbali ambayo hutuongezea ujuzi wa lugha.

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ufahamu ni nini?
2. Kuna aina gani za ufahamu?
3. Ni hatua zipi zinazofuatiliwa katika kufahamu?
4. Taja mbinu za kutumia ili uweze kufahamu unayoyasoma au unayoyasikiliza.
5. Ni nini umuhimu wa ufahamu?

## 1.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 11**

Sikiliza wimbo wa Kiswahili kwenye redio kisha uzungumze na mwenzako kuhusu mawazo makuu yanayopatikana katika wimbo huo.

## 1.6. Kuandika

**KAZI 12**

Andika matini fupi kuhusu namna ya kupambana na uharibifu wa mazingira.

# SOMO LA 2: UFUPISHO

**KAZI 1**

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini.**



1. Una maoni gani kuhusu picha hii?
2. Nini kilichokuvutia na mabacho hakijakuvutia katika picha hii?

## 2.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba

**Soma hotuba ifuatayo, kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini.**

**Hotuba: Jifya Moja Haliinjiki Chungu**

Mheshimiwa Mkurugenzi wa Masomo hapa shuleni,

Mheshimiwa Mkuu wa Nidhamu hapa shuleni,

Waheshimiwa Walimu,

Na wanafunzi wote hamjambo?

Tumekutana sote hivi leo, viongozi, walimu na wanafunzi wa shule yetu ya Mwangaza ili tuzungumze kwa kawaida yetu kuhusu mada ya "Ndi Umunyarwanda." Asubuhi hii ningependa tuzungumzie waziwazi juu ya umuhimu wa ushirikiano baina yetu sote iwapo tunataka maendeleo mazuri ya shule yetu. Wahenga walisema: "Ngozi ivute ingali mbichi". Tupo mwanzoni mwa mwaka. Ndiyo maana nimewaita hapa ili tuanze safari ya mwaka huu. Hii ni safari ndefu na ngumu na msafiri ni aliye bandarini.

Madhumuni ya kuwataka viongozi, walimu na wanafunzi kushirikiana ni kwa sababu matokeo mazuri yanategemea ushirikiano wetu sisi sote pamoja. Jifya moja haliinjiki chungu. Kitu ambacho ningependa kusisitiza ni kwamba wanafunzi wote ni sawa. Wawe wavulana, wawe wasichana. Hatuwezi kusema wanafunzi wa aina fulani huzaliwa wajinga na wengine wa aina nyingine huzaliwa werevu. Mungu hakupanga hivyo kwani hana moyo wa kupendelea jinsia hii wala kuonea jinsia nyingine. Suala tunalokumbana nalo ni hili lifuatalo: «Kwa nini shule fulani tu ndizo zenye matokeo na maendeleo mazuri kila kukicha? » Ukaona kuwa wanafunzi wao hushinda vizuri, shule ina usafi na mengineyo. Jibu ni kwamba wanafunzi wote wa shule hizo huungana pamoja wavulana kwa wasichana. Mtanisamehe, leo, hakuna kufichana. Wahenga walisema "Mficha uchi hazai." Tuambiane ukweli ili tuweze kuyatatua matatizo tunayokumbana nayo. Katika shule hii unaona kuwa wavulana wameanza kujenga makundi yao na wasichana wakajenga yao. Ati hamwezi kusoma pamoja, msichana hawezi kuwa kiranja, mvulana hawezi kupiga deki au kufagia na mambo mengine mengi ya utovu wa nidhamu. Leo ninawahamasisha walimu kufuatilia karibu mambo hayo ili tuweze kwenda pamoja. "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu." Kazi anayoweza mvulana na msichana anaweza kuifanya au mvulana akafanya kazi zinazodhaniwa kuwa za kisichana. Mshikamano huu ndio utakaotuwezesha kuwa Wanyarwanda kindakindaki.

Kwa upande wa masomo wanafunzi nawakumbusha kwamba, "Mtaka cha uvunguni sharti ainame." Matokeo mazuri yatatokana na ustahamilivu, jitihada, mshikamano na kujitolea. Na wenzenu kutoka shule nyingine ndivyo wafanyavyo. "Ukiona vyaelea, vimeundwa." Shule yetu ina vifaa vya kutosha na walimu wazuri. Mimi nina imani kwenu na ninatumaini kwamba mtaweza kwa kuwa uwezo mnao na nguvu mnazo. Kuanzia asubuhi hii tupate uamuzi mmoja wa kushikamana sote vilivyo na sisi wenyewe tutavuna matunda yatakayotufurahisha. Na shule yetu na hata nchi yetu zitazidi kusonga mbele.

Nawashukuru kwa kunisikiliza na ninadhani kuwa maneno yangu hayajapita sikio hadi sikio. Asanteni.

## KAZI 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Hotuba hii ilikuwa ikitolewa na nani?
2. Madhumuni ya mkutano huo ni yapi ?
3. Mwandishi alikusudia nini aliposema « Jifya moja haliinjiki chungu? »
4. Ni tatizo gani walilokuwa wakikumbana nalo wanafunzi wa shule ya Mwangaza ?
5. Aliyekuwa akihutubu alieleza kuwa matokeo mazuri yatatokana na nini?

## 2.2. Msamiati kuhusu Hotuba

## KAZI 3

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

i) Wahenga
ii) Bandari
iii) Mshikamano
iv) Ustahamilivu
v) Kiranja

## KAZI 4

**Tunga sentensi kwa kutumia meneno yafuatayo:**

i) Deki
ii) Kufagia
iii) Jitihada
iv) Nidhamu
v) Kindakindaki

## 2.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno

**KAZI 5**

**Chunguza maneno yaliyokolea kisha ueleze mabadiliko utakayoyaona:**

i) Kagabo anapenda **kulima**.

ii) Kagabo ni **mkulima**.

iii) Kagabo anapenda **kilimo**.

iv) **Mtoto** yule anapenda amani.

v) **Kitoto** kile kinapenda amani.

vi) **Toto** lile linapenda amani.

vii) **Utoto** wake ulikuwa wa kupendeza.

viii) **Usafi** wa mazingira haya ni wa kupendeza.

iv) Kalisa anacheza **kitoto**.

- **Kulima** ni kitenzi
- **Mkulima**, **kilimo**: nomino zinazotoka kwenye kitenzi kulima.
- **Mtoto** ni jina.
- **Kitoto, toto, utoto**: ni majina yanayotoka kwenye jina mtoto.
- **Usafi**: ni jina linalotoka kwenye kivumishi safi.
- **Kitoto**: ni kielezi kinachotoka kwenye jina mtoto.

### Maelezo muhimu kuhusu uambishaji wa maneno

Katika somo la kwanza tulizungumzia kwa kina uambishaji kama mbinu ya kuzalisha maneno mapya kutoka maneno mengine. Mbinu hii hufanyika kwa kuongeza kwenye sehemu fulani (viini, mizizi au mashina) za maneno hayo viambishi mbalimbali mwanzoni au mwishoni. Katika somo hilo tuliona uambishaji wa vitenzi yaani uzalishaji wa vitenzi kutoka maneno mengine.

Katika somo hili tutaona:

- Uambishaji wa majina
- Uambishaji wa vielezi

- **Uambishaji wa majina**

Uambishaji wa majina ni uundaji wa majina kutoka maneno mengine. Kuna:

- Uambishaji wa majina kutoka majina mengine
- Uambishaji wa majina kutoka vitenzi
- Uambishaji wa majina kutoka vivumishi
- Uambishaji wa majina kutoka vielezi

**i) Uambishaji wa majina kutoka majina mengine**

Uambishaji wa majina kutoka majina mengine hufanyika kwa kuweka katika hali/dhana fulani. Hali/dhana hizo ni umoja, wingi, udogo, ukubwa na dhahania.

Kwa kawaida jina huundwa na sehemu mbili: kiambishi ngeli na shina. Kiambishi ngeli ni mofimu inayoonyesha ngeli ya jina. Viambishi ngeli vya majina ni **mu- (vitu vyenye uhai), wa-, mu- (vitu visivyo na uhai), mi-,ji-/Ø-, ma-, ki-, vi-, n-, n-, u-, u-, ku-, pa-, mu-, ku-.**

**Mifano:**

| Kiambishi ngeli | jina | Kanuni ya kimofolojia |
|---|---|---|
| Mu- | Mtu: mu-tu<br>Mwana: mu-ana | u → Ø/M-K<br>u → w/-I |
| Wa- | Watu: wa-tu<br>Wana: wa-ana | <br>a → Ø/-I |
| Mu- | Mti: mu-ti<br>Mwiko: mu-iko | u → Ø/M-K<br>u → w/-I |
| Mi- | Miti: mi-ti<br>Miiko: mi-iko | |
| Ji- /Ø- | Jicho: ji-cho<br>Jina: Ø-jina | |
| | Jino: ji-ino | i → Ø/-I |
| Ma- | Macho: ma-cho<br>Meno: ma-ino | <br>a+i → e |

| | | |
|---|---|---|
| **Ki-** | **Kiti: ki-ti**<br><br>**Cheo: ki-eo** | **i → y/I, ky → ch: kwa kuandika na katika matamshi** |
| **Vi-** | **Viti: vi-ti**<br><br>**Vyeo: vi-eo** | **i → y/I** |
| **n-** | **Ndoo (moja): n-doo**<br><br>**Nyumba (moja): n-umba** | **n → ny/-I** |
| **n-/Ø-** | **Ndoo (nyingi): n-doo**<br><br>**Nyumba (nyingi): n-umba**<br><br>**Mbao: n-bao**<br><br>**Mvi: n-vi**<br><br>**Kuta: Ø-kuta** | **n → ny/-I**<br><br>**n → m/b-**<br><br>**n → m/v-** |
| **u-** | **Ukuta: u-kuta**<br><br>**Waya: u-aya** | **u → w/-I** |
| **u-** | **Uzembe: u-zenbe** | |
| **Ku-** | **Kucheza:**<br><br>**ku-chez-a** | |
| **Pa-** | **Pahali: pa-hali** | |

**TANBIHI:** Hakuna majina kwenye ngeli ya **mu-** na **ku-.** Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili tunapachika kiambishi **–ni** nyuma ya majina ya kawaida.
**Mifano**:

- Meza**ni** **ku**na usafi.
- Chumba**ni** **m**na usafi.

**a) Hali ya umoja na wingi**

- Katika umoja viambishi ngeli ni **mu-, mu-, ji-/Ø-, ki-, n-, u-, u-, ku-, pa-, mu-, ku-.**
- Katika wingi viambishi ngeli ni **wa-, mi,-ma-, vi-, n-/Ø, ku-, pa-.**

**Mifano:**

| Hali ya umoja | Hali ya wingi |
|---|---|
| Mtu : m-tu | Watu : wa-tu |
| Mto : mu-to | Mito : mi-to |
| Kisu : ki-su | Visu : visu |

**KAZI 6**

**Weka majina yafuatayo katika wingi:**

- Mwanamke
- Mwanamume
- Chandarua
- Jembe
- Kabati
- Ufa
- Ujinga
- Ukurasa
- Wembe

**b) Hali ya udogo (Kudunisha)**

Uundaji wa majina ya hali ya udogo hufanyika kwa kupachika viambishi **ki-** na **vi-** mbele ya mashina ya majina ya kawaida.

| Hali ya wastani | Hali ya ukubwa | |
|---|---|---|
| | Umoja | Wingi |
| Mtoto | Kitoto | Vitoto |
| Darasa | kidarasa | Vidarasa |
| Gari | Kigari | Vigari |
| Mlima | Kilima | Vilima |

**TANBIHI:**

- **Majina yenye mashina ya silabi moja huchukua ji- nyuma ya ki- na vi-.**

**Mifano:**

Mtu: kijitu- vijitu

Mto: Kijito- vijito

- **Mashina yanayoanzwa na irabu huchukua ji- nyuma ya ki- na vi-.**

**Mifano:**

Mwana: Kijana- vijana

Mume: kijiume- vijiume

- **Majina ya ngeli ya Ki-/Vi- huchukua ji- nyuma ya ki- na vi-.**

**Mifano:**

Kitabu: Kijitabu- vijitabu

Kiboko: kijiboko- vijiboko

**c) Hali ya ukubwa (Kukuza)**

Uundaji wa majina ya hali ya ukubwa hufanyika kwa kupachika viambishi **ji-/Ø-** na **ma-** mbele ya mashina ya majina ya kawaida.

**TANBIHI:**

- **Kwa majina yenye mashina ya silabi moja ji- hurudi katika wingi.**

**Mifano:**

| **Hali ya wastani** | **Hali ya ukubwa** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Mtu | Jitu | Majitu |
| Kisu | Jisu | Majisu |
| Mto | Jito | Majito |

- **Majina yenye silabi mbili au zaidi huchukua kiambishi Ø- mbele ya shina katika umoja na ma- katika wingi.**

**Mifano:**

| **Hali ya wastani** | **Hali ya ukubwa** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Mguu | guu | maguu |
| Mtoto | Toto | Matoto |
| Mlima | Lima | Malima |

- **Majina ya ngeli ya Li-/Ya- huchukua ji- katika umoja na wingi.**

**Mifano:**

| **Hali ya wastani** | **Hali ya ukubwa** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Gari | Jigari | Majigari |
| Kabati | Jikabati | Majikabati |
| Jiwe | Jijiwe | Majijiwe |
| Jina | Jijina | Majijina |

- **Majina yenye mashina yanayoanzwa na irabu huchukua ji- katika umoja na ji- hii ikarudi katika wingi.**

**Mifano:**

| **Hali ya wastani** | **Hali ya ukubwa** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Mwana | Jana | Majana |
| Mwalimu | Jialimu | Majialimu |
| Nyumba | Jumba | Majumba |

**Tahadhari:** Wanafuzi wawe makini na matumizi ya dhana za udogo au ukubwa katika mawasiliano rasmi. Kwani ukubwa au udogo unaojitokeza hapa mara nyingine huwa sio wa kupendeza.

**d) Hali ya dhahania**

Uundaji wa majina ya hali ya dhahania hufanyika kwa kupachika kiambishi **u-** mbele ya mashina ya majina ya kawaida. Majina haya hayana wingi

**Mifano:**

| **Hali ya wastani** | **Hali ya dhahania** |
|---|---|
| Mtoto | Utoto |
| Mwalimu | Ualimu |
| Mbwa | Ubwa |
| Mwizi | Wizi |
| Mke | Uke |
| Mume | Uume |

## KAZI 7

**Jaza jedwali lifuatalo**

| Wastani | Udogo | Ukubwa | Dhana ya dhahania |
|---|---|---|---|
| Mbuzi | | | |
| | | | Utoto |
| | | Majialimu | |
| Ng'ombe (wengi) | | | |
| | Kikapu | | |

### ii) Uambishaji wa majina kutoka vitenzi

Uundaji wa majina kutoka vitenzi hufanyika kwa kupachika viambishi ngeli mbele ya mizizi au mashina ya vitenzi na viishio nyuma ya mizizi au nyuma ya mashina. Viishio vinavyotumiwa ni **aji**-, **u-**, **e-**, **i-, o-** na **a-**

**Mifano:**

- Kufuga: mfugaji, ufugaji
- Kutenda: tendo, utendaji
- Kusoma: msomi, somo, msomaji
- Kufa: kifo, mfu
- Kupinda: pindo, upinde

## KAZI 8

**Unda majina mawili kutoka vitenzi vifuatavyo:**

- Kurekebisha
- Kupigana
- Kupika
- Kulala
- Kula

### iii) Uambishaji wa majina kutoka vivumishi

Uundaji wa majina kutoka vivumishi hufanyika kwa kupachika viambishi ngeli mbele ya mashina ya vivumishi.

**Mifano:**

- safi: usafi
- refu: mrefu, urefu
- pana: upana
- nene: unene, mnene
- zuri: uzuri

**KAZI 9**

**Unda majina kutoka vivumishi vituatavyo :**

- Fupi
- Baya
- Embamba
- Kaidi
- Halali

**iv)Uambishaji wa majina kutoka vielezi**

Uundaji wa majina kutoka vielezi hufanyika kwa kupachika viambishi ngeli mbele ya vielezi.

**Mifano:**

- Sawa: usawa
- Mbali: umbali

**KAZI 10**

**Tafuta mifano mingine ya majina yanayoundwa kutokana na vielezi.**

- **Uambishaji wa vielezi**

Uambishaji wa vielezi ni uzalishaji wa vielezi kutoka maneno mengine. Kuna:

- Uambishaji wa vielezi kutoka majina
- Uambishaji wa vielezi kutoka vivumishi.

**i) Uambishaji wa vielezi kutoka majina**

Uambishaji wa vielezi kutoka majina hufanyika kwa kupachika kiambishi ki- mbele ya shina la jina. Vielezi vinavyoundwa kwa namna hii ni vielezi vya namna.

**Mifano:**

| Jina | Kielezi | Sentensi |
|---|---|---|
| Mtoto | Kitoto | Walicheza **kitoto**. |
| Mume | kiume | Amejikaza **kiume**. |
| Mnyama | kinyama | Wahalifu waliua watu **kinyama**. |
| Masai | Kimasai | Amevaa nguo za **kimasai** |
| Sabuni | Kisabuni | Kujikaza **kisabuni** kunavunja moto. |

**KAZI 11**

**Unda vielezi vitano vinavyotoka kwenye majina kisha uvitumie katika sentensi.**

**ii) Uambishaji wa vielezi kutoka vivumishi**

Uambishaji wa vielezi kutoka vivumishi hufanyika kwa kupachika viambishi **ki-** na **vi-** mbele ya shina la kivumishi. Vielezi vinavyoundwa kwa namna hii ni vielezi vya namna na vile vya kiasi.

**Mifano:**

| Kivumishi | Kielezi | Sentensi |
|---|---|---|
| Dogo | Kidogo | Anafanya kazi **kidogo** (namna)<br><br>Alipata fedha **kidogo** (kiasi) |
| Zuri | Vizuri | Mwanadamu anapaswa kuishi **vizuri** (namna). |
| Kali | Vikali | Kwa kutafuta amani ya kudumu, wanajeshi wetu walipigana **vikali** na waasi (namna). |

**KAZI 12**

**Toa mifano mingine ya vielezi vingine kutoka vivumishi kisha uvitumie katika sentensi.**

## 2.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Ufupisho

**KAZI 13**

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

**Maelezo muhimu: Maana ya ufupisho**

Ufupisho ni taaluma ya kufanya muhtasari wa habari iliyoandikwa au iliyosimuliwa bila kupotosha wazo au mawazo ya awali ya msemaji au mwandishi. Ufupisho ni hali ya kufanya muhtasari au kupunguza urefu.

Ili mtu aweze kufanya ufupisho vizuri anapaswa kuzingatia taratibu zifuatazo:

- Kusoma habari au kusikiliza habari husika zaidi ya mara moja ili kuweza kuielewa.
- Ni lazima kuzingatia mawazo makuu na kuyaandika.
- Kuchagua au kuteua mambo muhimu au kiini cha habari huku tukijiepusha na maelezo ya ziada, mifano, vielezi au tamathali za usemi.
- Hakikisha kwamba maneno yote ya maana yaliyokusudiwa na makala au habari ya awali yamebaki.
- Hakikisha pia kwamba ufupisho wako una urari au mfuatano mzuri wa mawazo.
- Zingatia urefu wa muhtasari unaohitajika.
- Kuandika kwa mtiririko mambo muhimu uliyoyateua.
- Usiige lugha ya mwandishi au msimuliaji. Ni kusema kuwa unapaswa kutumia maneno yako unapofanya ufupisho.

Ufupisho mzuri hauna budi kuwa na sifa zifuatazo:

- Unapaswa kuwa na mawazo makuu yanayoeleweka.
- Unapaswa kuwa si zaidi ya theluthi moja ya kifungu cha habari chote au habari uliyosikia.
- Lugha inayotumiwa ni lazima iwe lugha fasaha.
- Unaweza kuwa katika aya moja au nyingi.
- Unapaswa kumwezesha msikilizaji au msomaji kupanua msamiati.

**Jibu maswali haya :**

1. Unadhani ni kwa sababu gani ufupisho hutegemea sana mbinu za ufahamu?
2. Ni nini umuhimu wa ufupisho?

## 2.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 14**

**Jikumbushe habari uliyosikia, uifupishe kisha uwasilishe mbele za wenzako.**

## 2.6. Kuandika

**KAZI 15**

**Fanya ufupisho wa hotuba uliyosoma hapo juu katika mistari mitano.**

**Tathmini ya Mada ya Kwanza**

1. Ufahamu ni nini?
2. Ni hatua zipi zinazofuatiliwa katika ufahamu?
3. Ni nini umuhimu wa ufahamu?
4. Ufupisho ni nini ?
5. Unadhani ni kwa sababu gani ufupisho hutegemea sana mbinu za ufahamu?
6. Ni nini maana ya uambishaji?
7. Unda vitenzi kutoka maneno yafuatayo :

- Imara
- Tata
- Erevu
- Adhabu
- Karibu

8. Jaza jedwali lifuatalo :

| Wastani | Udogo | Ukubwa |
|---|---|---|
| | | Jibwa |
| | Vijanavijike | |
| Kiti | | |
| | | Majoka |
| | Kigombe | |

# MADA YA 2

# UTUNGAJI WA BARUA RASMI

## Uwezo mahususi

Kuandika barua rasmi kwa ufasaha

- **Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya barua rasmi,
- Kutaja sehemu kuu za barua rasmi,
- Kubainisha mahali tofauti pa kutumia barua rasmi,
- Kuonyesha umuhimu wa barua rasmi,
- Kutambua nafasi ya kiwakilishi rejeshi -po- katika kitenzi.

## Kidokezo

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali ya hapo chini**



**Maswali**

1. Watu wanaoonekana kwenye mchoro huu wanafanya nini?
2. Jadili sababu zinazoweza kuwa chanzo chao kufanya hivyo.
3. Je, wewe umewahi kufanya hicho kinachofanywa na watu hao? Kwa sababu gani?
4. Kama hujawahi kufanya, hivyo nini kinachoweza kukusababisha na wewe kufanya hivyo?

# SOMO LA 3: MWONGOZO WA KUTUNGA BARUA RASMI/KIKAZI

## 3.1. Kusoma na Ufahamu: Baruaya Kuomba Kazi

**Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

Kijiji cha SAVE
Tarafa ya SAVE
Wilaya ya GISAGARA
Nambari ya Simu:
0783765490
11/01/2020

Meya,

Wilaya ya Gisagara

S.L.P. 1111 Gisagara

Tovuti: www.gisagara.gov.rw

Barua pepe: gisagaradistrict@minaloc.gov.rw

Ndugu,

**KUH. OMBI LA KAZI YA KUFUNDISHA**

Napenda kutuma ombi langu la kazi ambayo nimeitaja kwenye kichwa cha habari cha hapo juu.

Mimi ni kijana mwenye umri wa miaka kumi na nane. Nimemaliza masomo yangu mwaka 2019 katika chuo cha Ualimu cha Save na kupewa cheti cha ualimu wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari.

Natuma ombi langu la kazi ya kufundisha kwako ili niwe mmoja kati ya wale watakaofikiriwa kupewa kazi ya kufundisha katika Wilaya ya Gisagara.

Nyaraka zote zinazohitajika nimeziambatisha kwenye barua hii kama viambatisho.

Ni matumaini yangu kuwa ombi langu litakubaliwa.

Wako mtiifu,

~~Uwamwiza~~

UWAMWIZA Zawadi

**KAZI 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

a) Ni nani ambaye ameandika barua hii?
b) Anaishi wapi?
c) Amemwandikia nani?
d) Madhumuni ya barua ni yapi?
e) Mwandishi huyu ni mtu gani?

## 3.2. Msamiati kuhusu Barua

**KAZI 2**

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

- Chuo :
- Stashahada:
- Mtiifu :
- Watakaokubaliwa:
- Kiambatisho:

**KAZI 3**

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

- Ombi:
- Umri:
- Vitambulisho:
- Tovuti:
- Matumaini:

## 3.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi rejeshi -po-

**KAZI 4**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha ueleze matumizi ya kiambishi kilichopigiwa mstari.**

- Vijiko vi<u>**po**</u> mezani.
- Pale pali<u>**po**</u>jengwa panatisha.
- Majengo mengi ya<u>**po**</u> mlimani.
- Mvua itaka<u>**po**</u>nyesha tutalima.
- Mvua isi<u>**po**</u>nyesha hatutalima.

### Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya kiambishi –po-

Kiambishi rejeshi **–po-** kinaweza kutumiwa kwa njia mbili. Njia ya kwanza **–po-** inarejelea mahali. Kwa njia ya pili **–po-** huonyesha wakati.

- **Matumizi ya –po- ya mahali**

Kiambishi **-po-** kikisimamia mahali kinakuwa **–o** rejeshi iliyotumiwa katika ngeli ya **PA-M-KU**. Kinapotumiwa ndani ya kitenzi kinasimamia maneno "**mahali ambapo."** Ni kusema kuwa **–po-** hii inapatikana tunapoondoa **"amba"** katika sentensi.

**Mifano:**

- <u>**Mahali ambapo**</u> anaishi ni pazuri: Mahali ana**po**ishi ni pazuri.
- <u>**Pale (Mahali) ambapo**</u> palijengwa panatisha: Pale pali**po**jengwa panatisha.

- **<u>Mahali ambapo</u>** tutapanda miti ile ni pale milimani: Mahali tutaka**po**panda miti ile ni pale milimani.

  - **Matumizi ya –po- ya wakati**

Kiambishi **–po-** kikionyesha wakati hutumiwa kwa kuonyesha tendo hutendeka, lilitendeka au litatendeka na kufuatwa na jingine.

**Mifano:**

- Mvua ili**po**nyesha tulikimbia.
- Mvua nyingi ina**po**nyesha watu wengi huogopa.

**Tanbihi:**

  - Katika wakati ujao kiambishi **–po-** huenda pamoja na kiambishi **–ka-.**

**Mifano:**

- Atakapofika tutampokea vizuri.
- Nita**kapo**pewa kazi ya kufundisha nitafundisha ipasavyo.
  - Kuna kiambisi **–po-** kinachotumiwa pamoja na **–si-** tukikanusha vitenzi vyenye kiambishi **ki-** na **–takapo-.**

**Mifano:**

| **Hali yakinishi** | **Hali kanushi** |
|---|---|
| **Itakapo**nyesha tutalima. | **Isipo**nyesha hatutalima. |
| A**takapo**pata ajira atajenga nyumba. | A**sipo**pata ajira hatajenga nyumba. |
| U**ki**omba utapewa | U**sipo**omba hutapewa. |
| U**ki**pewa kazi  jenga nyumba. | U**sipo**pewa kazi usijenge nyumba. |

## KAZI 5

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia –po-:**

i) Barabara ……………….jengwa hurahisisha huduma za kibiashara.

ii) Chumvi …..kosekana, chakula hupoteza ladha.

iii) Ujanja …..zidi basi watu wote watagutuka.

iv) Maji ….mwagika hayazoleki.

v) Yeye ….choma msitu aliadhibiwa.

## KAZI 6

**Unganisha sentensi hizi ukitumia -po- ili upate sentensi moja mwafaka.**

i) Walitutisha. Wakapewa onyo.

ii) Mvua ilinyesha. Tukalima.

iii) Mlitutafuta. Mkapata mlichokitaka.

iv) Ulinisaidia. Nikafurahi.

v) Walifanya bidii. Wakafaulu.

## 3.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Uandishi wa Barua Rasmi

## KAZI 7

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini**

### i) Maana ya Barua

Barua au waraka ni maandishi yaliyopangwa kwa utaratibu na mtiririko maalum kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe fulani. Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo.

Barua huandikwa kwa madhumuni mbalimbali kama kuarifu, kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa; kuagiza bidhaa, n.k.

### ii) Aina za barua

- **Barua za kirafiki**: ni zile ambazo huandikiwa na mtu au watumbalimbali walio na uhusiano wa karibu na anayeandika; k.v. rafiki, mzami, ndugu, n.k.
- **Barua za mwaliko** zenye lengo la kumwalika mtu katika sherehe au sikukuu fulani
- **Barua rasmi/ za kikazi** zenye madhumuni ya kazi. Kwa kawaida barua rasmi huandikwa kwa makusudi mbalimbali kama vile, kutoa taarifa za tukio fulani, kuomba kazi, kuagiza vifaa au vitu, kumwalika kiongozi katika shughuli maalumu, kutoa taarifa ya kushindwa kufika mkutanoni na kadhalika. Barua hizi zina utaratibu wa kuziandika.

### iii) Sehemu za barua rasmi

Sehemu za baruwa rasmi zinakaribia kufanana na zile za barua ya kirafiki lakini kuna tofauti kidogo. Ifuatayo ni mifano wa mipangilio ya barua za kuomba kazi.

***Barua ya kuomba kazi kwa mara ya kwanza**

Anwani ya mwandishi

Tarehe

Anwani ya mwandikiwa

KICHWA CHA HABARI

Ujumbe kamili wa barua

Hitimisho la barua

Sahihi ya mwandikaji

Jina la mwandikaji

*** Barua ya mtu anayetaka kazi akiwa na kazi nyingine**

Anwani ya mwandishi

Tarehe

Anwani ya mwandikiwa

K.K

Anwani ya mkuu wa kazi atakayepitisha barua ya mwombaji

KICHWA CHA HABARI

Ujumbe kamili wa barua

Hitimisho la barua

Sahihi ya mwandikaji

Jina kamili la mwandikaji

### iv) Maelezo

#### 1. Anwani ya ya mwandishi na tarehe

Anwani hii huandikwa upande wa juu mkono wa kulia wa barua na chini yake kunawekwa tarehe.

#### 2. Anwani ya mwandikiwa

Anwani hii inaandikwa upande wa kushoto wa karatasi chini kidogo ya anwani ya mwandishi. Katika sehemu hii jina la mwandikiwa haliandikwi isipokuwa cheo chake; hata ikiwa mnazoeana kwa kiasi fulani ni lazima kuandika cheo chake.

#### 3. Kichwa cha habari

Hili ni kusudi la barua. Kichwa cha habari huwa chini ya anwani ya mwandikiwa. Kichwa hicho huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari chini.

#### 4. Ujumbe wa barua

Ujumbe wa barua huandikwa chini ya kichwa cha barua. Katika barua za kikazi ni mambo muhimu yanayoandikwa tu. Ujumbe huu unatanguliwa na sentensi inayorejerea kwenye kichwa cha habari.

**Tanbihi:**

- Uandishi wa barua za kikazi unahitaji uangalifu sana na lugha iliyo wazi kwa sababu kama kuna matatizo barua hiyo huwa ni shahidi wako na inaweza kukuokoa au kukuponza.
- Hakuna sehemu ya salamu kwa mwandikiwa katika barua hizi. Mambo hayo ya salamu ni ya barua za kirafiki.

#### 5. Hitimisho la barua

Hitimisho/Mwisho wa barua huwa ni tamko la heshima la kumalizia barua. Mara nyingi mwisho unaotumika katika barua rasmi ni kama vile :

- Wako mtiifu,
- Wako mwaminifu,
- Wako katika ujenzi wa taifa,
- Wako katika kazi,
- Na kadhalika.

#### 6. Sahihi na jina la mwandikaji

Jina la mwandishi huandikwa likifuata sahihi yake. Jina huwekwa chini ya sahihi si juu yake.

**TANBIHI:**

Kama barua rasmi inatoka ofisi ikienda nje au inatoka nje ikingia ofisini, kuwa sehemu nyingine zinazoweza kuonekana kwenye barua hiyo. Sehemu hizo ni kama kumbukumbu namba, kupitia kwa na nakala.

**1. Kumbukumbu namba**

Kumbukumbu namba zinaandikwa mara nyingi kwenye upande wa kushoto wa karatasi. Kumbukumbu hii husaidia kurahisisha kutafuta barua katika majalada. Kwa hiyo ni muhimu kutaja kumbukumbu namba ya barua unapojibu na kuandika barua iliyo na uhusiano nayo. Zaidi ya kumbukumbu namba, barua nyingine zinakuwa na namba ya simu chini yake.

**2. Kupitishwa kwa (kwa kifupi: KK)**

Kuna wakati mwandishi wa barua hupitisha barua yake kwa kiongozi mwingine kabla ya kuifikisha kwa mwandikiwa. Inapojitokeza haja hiyo, huandika KK chini kidogo ya anwani ya mwandikiwa na chini yake cheo cha huyo kiongozi, ukitarajia kwamba atatia saini yake kuhakikisha kwamba amekuwa wa kwanza kujua maombi yako.

Kwa mfano, iwapo mwandishi wa barua ameajiriwa na anaandika barua binafsi kwa mkuu mwingine wa kazi ili kuomba kazi, kuuliza mambo ya kikazi na kadhalika, inambidi apitishe barua hiyo kwa mkuu wake wa kazi mahali anapofanyia kazi.

**3. Nakala mbalimbali**

- Iwapo kuna watu zaidi ya yule unayempelekea barua ambao unataka wapashwe habari ya jambo uliloandika, basi ni lazima kuwatumia nakala ya barua hiyo unayoandika. Jambo hilo pia litamjulisha mwandikiwa kuwa barua hiyo inasambazwa kwa watu wengi.
- Orodha ya watu wanaopelekewa nakala ya barua huonyeshwa upande wa kushoto wa karatasi. Kichwa cha nakala hulingana na sahihi ya mwandikaji.

Jibu maswali yafuatayo:

1. Barua rasmi huandikwa kwa minajili ipi ?
2. Barua rasmi hutofautiana vipi na barua ya kirafiki ?
3. Taja sehemu muhimu ziundazo barua rasmi

## 3.5. Kusikiliza na kuzungumza

**KAZI 8**

***Jadilianeni tofauti iliyopo kati ya barua ya kirafiki na barua rasmi.***

## 3.6. Kuandika

**KAZI 9**

**Andika barua ya kikazi kwa meneja wa shirika la wakalimani nchini Rwanda ukimwomba kazi ya ukalimani. Makao makuu ya shirika yawe Mjini Kigali, Wilaya Nyarugenge.**

# SOMO LA 4: MIFANO YA BARUA RASMI

**KAZI 1**

**Jibu maswali yafuatayo :**

Unaelewa nini kuhusu barua rasmi ?

Taja mfano wa barua rasmi

## 4.1. Kusoma na Ufahamu: Barua ya Kuomba Ruhusa

**Soma barua ifuatayo hapo chini kisha ujibu maswali yanayofuata**

Chuo cha Ualimu
S.L.P 1000,
**MUHANGA**
30/11/2020

Mkurugenzi,
Chuo cha Ualimu,
S.L.P 100
**MUHANGA**

Ndugu,

**KUH: KUOMBA RUHUSA YA KUPUMZIKA**

Kichwa cha habari cha hapo juu chahusika. Ninaandika barua hii ili kuomba ruhusa ya kukosa kuhudhuria masomo yote ya leo.

Jana sikuweza kuja chuoni kwa sababu niliamka nikijihisi mgonjwa. Mama alinipeleka hospitalini ambapo nilipata matibabu. Walipopata vipimo waligundua kuwa ninaugua malaria. Nilipata dawa lakini bado sijapata nafuu. Ninaomba uniruhusu siku tatu nimalize dawa kisha nikipata nafuu nitarejea shuleni. Samahani sana kwa kutosema hili mapema.

Ninaambatisha na ripoti ya daktari.

Ninatumai ombi langu litakubaliwa.

Asante.

Wako mwaminifu,

**marym**

Mary Mutoni

**KAZI 2**

**Jibu maswli yafuatayo:**

1. Barua uliyoisoma ni ya aina gani ?
2. Mwandikaji wa barua hii ni nani?
3. Mwadikiwa ni nani ?
4. Mwandikaji alikuwa na shida gani ?
5. Lengo la kuandika barua hii ni lipi?

## 4.2. Msamiati kuhusu Barua ya Kuomba Ruhusa

**KAZI 3**

**Husisha maneno kutoka sehemu ya A na maelezo yake katika sehemu ya B.**

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| 1. Barua rasmi | a) Kitu anachopewa mgonjwa mfano vidonge , maji au unga ili kutibu ugonjwa |
| 2. Ruhusa | b) Dawa na huduma inayotolewa kumtibu mgonjwa |
| 3. Matibabu | c) Idhini au ikibali |
| 4. Dawa | d) Kurudi tena mahali ulipokuwa baada kuondoka kwa muda. |
| 5. Kurejea | e) Barua ihusianayo na shughuli za kikazi |

## KAZI 4

**Tafuta majina matano ya magonjwa kwenye mraba huu**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H | O | M | A | F | U | A | O | K |
| K | | A | | K | K | H | P | I |
| I | W | L | K | I | I | V | F | S |
| H | | A | A | K | M | R | S | U |
| A | H | R | S | O | W | A | M | K |
| R | O | I | W | H | I | Z | I | A |
| U | D | A | E | O | A | O | G | R |
| S | B | T | N | Z | N | K | O | I |
| I | U | I | D | I | M | P | O | Z |
| P | R | W | E | B | O | L | A | O |

## 4.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi Rejeshi -PO-

## KAZI 5

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha ueleze matumizi ya kiambishi-po- katika sentensi hizo.**

- Alipofika mjini Kigali alishangaa kuona majumba mazuri yenye usafi.
- Mgeni ali**po**wasili aliwakuta wanafunzi wakifanya kazi za ujenzi wa taifa.
- Kitabu hiki kili**po**letwa kilionekana kuwafaa wanafunzi wanaosomea ualimu.
  - Kiambishi **- po-** hutumika kuonyesha wakati wa tendo.
  - Kiambishi **-po-** hutumika kuonyesha mahali.

## KAZI 6

**Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia –po- ili upate sentensi moja mwafaka**

1. Alinisalimia. Nikamwitikia.
2. Mtatualika. Tutahudhuria.
3. Alinidharau. Sikumsamehe tena.
4. .Nitamwomba. Atanipa.
5. Mawingu yalianuka. Tulipanda miti.

## KAZI 7

**Kanusha sentensi zifuatazo:**

1. Utakapofika darasani mapema utasoma somo la Kiswahili.
2. Ukuta ulipojengwa hapa wezi walipungua.
3. Miti itakapokatwa ukame utatushambulia.
4. Ukifika tutaondoka.
5. Ukifika waniamshe.

## 4.4. Matumizi ya Lugha : Mifano ya Barua Rasmi

## KAZI 8

**Soma maelezo yafuatayo kuhusu aina za barua ya kikazi na barua itakayofuata kisha ujibu maswali yatakayotolewa baadaye.**

Barua rasmi zipo za aina nyingi, lakini zote zinapatikana kulingana na minajili yake. Barua hizo zinaweza kuwa:

- Barua ya kuomba kazi
- Barua ya kutoa taarifa
- Barua ya kuomba ruhusa
- Barua ya huduma
- Barua ya kuomba nafasi katika shule fulani
- Barua ya kuomba msamaha
- Barua ya shukrani
- Barua ya malalamiko
- Barua kwa mhariri
- Barua ya mapendekezo
- Barua ya uteuzi
- Barua za kuagiza au kupokea bidhaa/vitu
- Barua ya kusimamisha kazi
- Barua ya kusimamishwa au kufutwa kazi

Chuo cha Ualimu cha Byumba

Wilaya ya Gicumbi

S.L.P: 01 BYUMBA

4/12/2019

Mkurugenzi,
Chuo Kikuu cha Rwanda
S.L.P: 1234 KIGALI
K.K
Mkurugenzi,
Chuo cha Ualimu cha Byumba
SLP: 01 BYUMBA
Ndugu,

YAH: NAFASI YA MASOMO

Kichwa cha habari cha hapo juu chahusika. Ninakuandikia barua hii kuomba nafasi ya kujiunga na Chuo kikuu cha Rwanda chenye sifa na umaarufu mwaka wa masomo ujao.

Kwa mintarafu ya masomo yangu, mimi nilisoma katika Chuo cha Ualimu cha Byumba, wilayani Gicumbi. Nilimaliza masomo yangu mwaka jana na nikafaulu vizuri sababu kiasi kwamba nilipewa zawadi na serikali ya kuchagua chuo chochote kile nipendacho ili niendeleze masomo yangu.

Ni matumaini yangu kwamba utanipa fursa ya kusajiliwa ili nithibitishe uwezo na ukakamavu wangu.

Vitambulisho vyangu pamoja na matokeo ya mtihani wa taifa utayasoma kwenye stashahada yangu iliyoambatishwa kwenye barua hii.

Asante sana !

Wako mwaminifu,

~~karemjon~~

KAREMERA Joni

Nakala:

- Waziri wa Elimu
- Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Elimu

Jibu maswali yafuatayo:

1. Ni madhumuni gani yanayoweza kumfanya mtu aandike barua rasmi.
2. Ni nini tofauti, katika mpangilio, iliyoko baina ya barua ya kuomba ruhusa na barua ya kuomba nafasi ya masomo.

## 4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 9**

**Tunga barua ya kuomba kazi ya kufundisha kisha wasomee wenzako darasani ukizingatia matamshi sahihi na kusikika vema.**

## 4.6. Kuandika: Utungaji

**KAZI 10**

**Andika barua kwa Meneja wa Mbuga za Wanyama ya Akagera ukimwomba awaruhusu (nyinyi wanafunzi wa mwaka wa tatu) kutembelea mbuga hiyo.**

**Tathmini ya Mada ya Pili**

1. Eleza maana ya barua rasmi.
2. Taja sehemu muhimu za barua rasmi.
3. Tunga barua ya kuomba kazi ya kufundisha katika shule za chekechea.
4. Tumia kiambishi –po- katika sentensi zifuatazo:

a) Mwalimu……………tutaanza masomo (fika).

b) Jua ………walifua nguo zao na kuzianika. (waka).

c) Kalisa ……..mti mmoja yeye hupanda miwili (kata).

d) Mume na mkewe ………..familia yao husonga mbele (shirikiana).

e) ………………….kuhusu magonjwa ya zinaa, hatutapata madhara kutoka kwa magonjwa hayo (elimisha).

# MADA YA 3

## UTUNGAJI WA INSHA

### Uwezo mahususi

Kutunga insha zenye urefu wowote kwa kuzingatia kanuni za utungaji.

- **Malengo ya Ujifunzaji**

- Kueleza maana ya insha na aina zake,
- Kubainisha mbinu au taratibu za kutunga insha,
- Kutaja aina za insha,
- Kubainisha sifa za insha ya masimulizi na ya kubuni,
- Kuchunguza sifa za sehemu kuu za insha,
- Kupanga mawazo kwa mfuatano mzuri,
- Kutumia kwa ufasaha alama za vituo kulingana na kanuni za matumizi kwa kila alama,
- Kutunga aina mbalimbali za insha,
- Kutoa maana ya mnyambuliko na mnyumbuliko,
- Kueleza tofauti iliyopo kati ya mnyambuliko na mnyumbuliko wa maneno,
- Kunyambua na kunyumbua maneno ya Kiswahili.

## Kidokezo

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini**




1. Wahusika wanaoonekana kwenye mchorohuu wanafanya nini?
2. Wahusika hawa wako wapi?

# SOMO LA 5: MAANA YA INSHA

## 5.1. Kusoma na Ufahamu: Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu

**Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini**

Kanuma ni kijana ambaye alikuwa na tabia ya uvivu hasahasa darasani. Kila wakati mwalimu alikuwa akimuadhibu kwa vuruguvurugu na kuwa na tabia ya kusinzia darasani. Isitoshe, Kanuma hakuandika maandishi darasani na kila mwalimu alipokuwa akiacha kazi za nyumbani za kufanya alikuta Kanuma hajaanza wala kuandika maswali. Wakati wa mitihani na majaribio, Kanuma alikuwa na tabia ya kunakili na kumuuliza aliyekuwa akikaa karibu naye. Mara nyingine alikuwa akileta vikaratasi alivyotumia kwa kuandika majibu na alikuwa akivificha dawatini ili vimsaidie kunakili.

Wazazi wake walijaribu kumfunza tabia ya kuwa na bidii kwani siku zote bidii huzaa matunda. Walipenda kumuonya ili aweze kuweka njia za kuepukana na tabia hizo mbaya za kotopenda kufanya kazi lakini yeye hakusikia. Wazazi wake walijaribu kushirikiana na walimu wake kumfanya awe mtu mwenye kujitegemea katika siku za baadaye kwa kumpa mfano wa ndugu yake mdogo aliyempita na ambaye alikuwa chuoni wakati huo. Kilichokuwa kinaaibisha ni kuwa Kanuma alikuwa angali katika kidato cha pili shule za sekondari kwa miaka yake kumi na sita.

Kanuma aliendelea na tabia zake mbaya na kutia pamba masikioni kwa kukataa mashauri ya wazazi wake. Wakati wa kufanya mtihani wa taifa alitaka kunakili. Alipokamatwa na walimu, polisi waliitwa na hivyo akakamatwa na kupelekwa katika kituo cha kurekebisha maadili. Walimu na wanafunzi wenzake walipomuona na kukumbuka maonyo aliyopewa kutoka kwa wazazi wake na hata kwa walimu; walisema kuwa, “asiyesikia la mkuu huvunjika guu.”

Kanuma alipofika katika kituo cha kurekebishia maadili alikutana na vijana wengine waliofanya makosa mengi kama ubakaji, uvutaji wa bangi, utumiaji wa dawa za kulevya, wizi, mauaji na kadhalika. Hapo alipolinganisha kosa lake na makosa ya wenzake, alianza kujutia matendo aliyoyafanya. Kituoni alikutana na rafiki mmoja aliyeitwa Kimasa. Kila siku Kimasa alikuwa akimsimulia namna ambavyo alitiwa nguvuni kwa kosa la ubakaji. Wakati wote, Kimasa alikuwa akimwambia kuwa alionewa. Siku moja Kimasa alitaka kumlawiti Kanuma lakini Kanuma akakataa kwa sababu alikumbuka kuwa tendo hilo ni tendo la aibu. Alipowazia makosa ya Kimasa, alikumbuka kwamba mwalimu wake alimfundisha kwamba ulawiti ni njia nyofu ya kuambukizana magonjwa ya zinaa hasa UKIMWI. Hapo aliona kwamba ilikuwa lazima atengane na Kimasa.

Mbali na kurekebishwa kimaadili, Kanuma alifundishwa mambo mengi sana kituoni. Kwanza alifundishwa kucharaza gitaa akageuka mwimbaji hodari. Na wakati wa usiku yeye pamoja na vijana wenzake walikuwa wakiwaliwaza wenzao kwa nyimbo.

Alipotoka kituoni aliwakuta wanafunzi wenzake wakiwa na kazi nzuri; wengine walikuwa katika vyuo vikuu, akajuta. Wakati huu, mdogo wake alikuwa daktari. Mtegemea cha nduguye hufa maskini. Kanuma aliona kuwa ilikuwa lazima ajitegemee ili asije akawa mzigo kwa mdogo wake. Ndipo alianza kazi ya kuimba vilabuni, hotelini, harusini na katika hafla nyingine. Kuanzia wakati huo pesa zilianza kumiminika, akaajiri waimbaji wengine wakaunda bendi kubwa iliyovuma nchini mwao na kuvuka mipaka. Nyimbo nyingi za bendi hii zilikuwa zikiwahimiza vijana kuwa na mienendo mizuri. Bendi hii inasifika sana kwa kuwa imeundwa na vijana chipukizi waliokuwa na mienendo mibaya hapo kabla.

## KAZI 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Zipi ni tabia mbaya ambazo Kanuma alikuwa nazo?
2. Kanuma alitumia njia gani ili aweze kushinda mitihani?
3. Je alifanikiwa na njia yake? Eleza.
4. Mbali na kurekebishiwa maadili, ni ujuzi gani mwingine alioupata alipokuwa katika kituo?
5. Kanuma alifanya nini ili asije akageuka mzigo kwa mdogo wake?

## 5.2. Msamiati kuhusu kifungu

## KAZI 2

**Eleza maneno yafuatayo:**

- Vuruguvurugu
- Kunakili
- Kuaibisha
- Kulawiti
- Iliyovuma

## KAZI 3

***Ziba mapengo kwa kutumia maneno yafuatayo: akajuta, kumbaka, magojwa ya zinaa, kituo cha kurekebishia maadili, bendi, kilabu, dawa za kulevya, kumiminika.***

1. Ukitumia.............utatiwa nguvuni.
2. ...........................cha Gitagata kiko katika Wilaya ya Bugesera.
3. Alipofanya mapenzi bila kondomu aliambukizwa.......................
4. Watu walianza............. ukumbini..................ya wanamuziki ilipoanza kuimba nyimbo za kuhamasisha umoja na maridhiano.
5. Rugabo alihukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kosa la.................. mtoto wa miaka miwili.

## 5.3. Sarufi: Matumizi ya Alama za Vituo

**KAZI 4**

***Chunguza sentensi zifuatazo kisha bainisha majina ya alama zilizopigiwa mstari chini.***

1. U hali gani?
2. Yeye anapenda kunywa maziwa.
3. Wao hufuga mbuzi, kondoo, kuku na ng'ombe.
4. Nyoa ndevu zako!

- Alama zilizopigiwa mstari chini huitwa alama za vituo au alama za uakifishaji.

**Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya alama za vituo/ uakifishaji**

Binadamu wanapozungumza, tunaweza kutambua jinsi wanavyopandisha sauti au kuishusha kwa ajili ya kutoa ujumbe fulani (kuuliza, kushangaa, kushtuka, n.k). Vilevile, wanapomaliza usemi wao mtu huweza kutambua kuwa usemi umefikia kikomo kwa kusikia sauti zao tu. Lakini katika uandishi, hakuna sauti. Badala ya sauti, zipo alama za vituo ambazo hutumiwa kuwakilisha sauti katika uandishi. Kutokana na alama hizo, tunatambua kama usemi umekwisha, kuulizwa swali, kushangaa na kadhalika. Pia, tunaposoma, tunajua wapi tunafaa kupumua kidogo, kushusha au kupandisha sauti na kadhalika.

Alama hizi huitwa pia **viakifishi.** Hivyo basi, viakifishi ni alama zinazotumiwa katika maandishi ili kuleta maana ikusudiwayo katika matini mbalimbali kama vile sentensi, aya, mtungo, barua, mialiko, matangazo, ilani na kadhalika.

**Mifano zaidi ya alama za vituo au viakifishi**

**1. Nukta (.)**

i) Huwekwa mwishoni mwa sentensi.

**Mifano:**

- Amechoka.
- Rais wetu hapendi wachokozi.

ii) Hutumiwa kuonyesha ufupisho wa maneno.

**Mfano:**

- S.L.P. ( Sanduku la Posta )

iii) Hutumika kubainisha saa na dakika au tarehe.

**Mifano:**

- 9.20: saa tisa na dakika ishirini
- 14.11.2019: tarehe kumi na nne, Novemba, mwaka wa elfu mbili na kumi na tisa.

**2. Kistari kifupi (-)**

i) Hutumiwa kuonyesha kuwa neno linakatwa kwa vile limefika ukingoni mwa mstari husika na bado linaendelea katika mstari unaofuatia.

ii) Hutumiwa kuunga maneno yanayojenga neno moja. Mtindo huu aghalabu hujitokeza katika maneno yenye asili ya kigeni.

**Mfano:**

- Idd-el-Fitri
- Dar-es-Salaam

iv) Huweza kutumiwa badala ya koma.

**Mfano**: Nyimbo za asili-hasa Rumba-zinapendwa na wengi.

v) Hutumiwa kutenga silabi au mofimu zinazojenga neno.

**Mifano:**

u-ku-li-ma

ha-zi-na

ku-end-a

ku-li-a

Hutumiwa pamoja na nukta mbili kabla ya orodha.

**Mfano**:Jumuiya ya Afrika Mashariki inaundwa na nchi hizi:

- Rwanda
- Tanzania
- Uganda
- Kenya
- Burundi

**3. Kistari kirefu(—)**

i) Hutumiwa wakati panapotokea badiliko la ghafla katika sentensi. Hapo kinachukua nafasi ya mkato au mabano.

**Mfano**: Wewe—nina hakika—hutaki kutusaidia.

i) Hutumiwa baada ya orodha tangulizi / kauli tangulizi, labda kuifafanua zaidi.

**Mfano**: Kiingereza, Historia, Kinyarwanda—haya ndiyo masomo yanayowavutia wengi—hayamo katika ratiba.

ii) Hutumiwa kabla ya maneno ambayo ni msisitizo wa dhana iliyotajwa.

**Mfano**: Uharibifu wa mazingira—mnaona jinsi ulivyozidi—unatia wasiwasi.

iii) Hutumiwa kuonyesha kauli isiyomalizika au kukatizwa kwa kauli.

**Mfano**: Kalisa alisema, "nita —"

iv) Hutumiwa badala ya neno mpaka au hadi.

**Mifano**: Hesabu kutoka 20—50.

Alianzia hapa—pale.

**4. Alama ya mshangao (!)**

i) Hutumiwa kuashiria mahangaiko ya moyo kama vile hasira, hofu, mshangao na kadhalika.

**Mifano:**

- Lo! Mwanafunzi ameangusha kitabu cha mwalimu matopeni!
- Wamefungwa mabao kumi kwa nunge!

**5. Alama ya kuulizia/kiulizi (?)**

i) Hutumiwa mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa sentensi hiyo ni swali.

**Mfano**: Unaitwa nani?

ii) Hutumiwa kuonyesha ukosefu wa uhakika kuhusu jambo kama vile mwaka.

**Mfano**: Shule hii ya Kigali ilianzishwa 1992?

**6. Mabano/parandesi ( )**

i) Hutumiwa kufunga maneno ya ziada katika sentensi.

**Mfano**: Nyamata (makao makuu ya Bugesera) inakua kwa kasi.

ii) Hutumiwa na mwandishi anapotaka kutoa ufafanuzi kwa lugha nyingine tofauti na ile anayoitumia.

**Mfano**: Wandishi (editors) waalikwa.

iii) Hutumiwa kufungia herufi za kuorodhesha.

**Mifano:**

(a) huelimisha, (b) huburudisha, (c) huonya.

**7. Mkwaju (/)**

i) Hutumiwa kwa kuandika kumbukumbu namba za barua.

**Mifano:** Kumb. Na 002/001/0012/KGL/002

Kumb. Na 112/012/0099/NY/012

Hutumiwa kwa kuandika tarehe.

**Mfano:** Leo ni terehe 12/07/2019

Hutumiwa badala ya neno « au », « ama ».

**Mifano:** Mbweha/mbwamwitu ni mkali sana.

Beberu / mbuzi dume yule ni mkongwe.

Hutumiwa kwa kuandika akisami.

**Mifano:**

2/3

3/4

4/9

**8. Mtajo: (" " au ' ')**

i) Hutumiwa kuonyesha maneno halisi ya mzungumzaji.

Kwa mfano: *"Nitafika kesho jioni," alisema mdogo wake.*

ii) Hutumiwa kwa kuonyesha maneno yaliyonukuliwa katika kitabu au maandishi mengine.

**Mfano**: Kama Kamusi ya Kiswahili Sanifu inasema, **"**boi ni mwanamume aliyeajiriwa kufanya kazi za nyumbani**"** (Uk30).

i) Hutumiwa kwa kurejerea anwani za makala mbalimbali katika maelezo.

**Mfano**: Kitabu cha **"**Darubini ya Sarufi**"** ni kizuri sana.

ii) Hutumia kuonyesha neno geni katika lugha au lenye maana au kazi maalum.

**Mifano**: Mimi sipendi **“**matoke**”**.

Tulikwenda mjini tukaona ma **“**lorries**”**mengi.

iii) Hutumiwa kuandika jina la gazeti.

**Mfano:** Mnapaswa kusoma « Imvaho Nshya » ili mjue habari za ulimwengu.

**9. Mkato**

i) Hutumika kwa kutenganisha sehemu mbili za tungo

**Mfano**: Mtoto anasoma Kiswahili, wazazi wanamtafutia karo.

ii) Hutumika kwa kutenganisha maneno yanayofuatana.

**Mfano:** Wao hufuga kuku, mbuzi, kondoo na ng’ombe.

**10. Ritifaa (’)**

i) Hutumiwa kwa kuonyesha sauti/ herufi fulani imeachwa.

**Mifano:**

’likukanya (nilikukanya)

’kawa (ukawa)

’siniudhi (usiniudhi)

’19 (2019)

ii) Hutumiwa kwa kuonyesha sauti za ving’ong’o.

**Mifano:**

Ng’ombe

kung’aa

Kung’oa

**11. Nukta za dukuduku (…)**

Hutumiwa:

i) Badala ya neno na kadhalika.

Mifano: Alinunua viazi vitamu, nyama, nyanya, …

ii) Kuonyesha mambo yasiyotajika katika sentensi.

**Mfano**: Niliamshwa alfajiri na mapema…

iii) Kuonyesha kukatizwa kwa kauli/ usemi.

**Mfano**: La …ki …kini una …unani … ni …penda.

## KAZI 5

***Tia alama za vituo mwafaka katika sentensi zifuatazo :***

a) tulisoma kitabu cha romeo and juliet juzi.
b) simama ukasafishe ubao mwalimu akaamrisha
c) kuanzia 2017 2019 nilikuwa shuleni
d) hafla hiyo ilihudhuriwa na wafuataо rais mawaziri wabunge nk
e) matendo yao yalitupendeza furahisha
f) matoke huliwa na wachina though i dont like it
g) kengele hulia saa 430 mchana
h) masuala yafuatayo yamegusiwa na mwandishi

Utu

Uzalendo

mshikamano

i) amina alitusomea aya tatu kutoka kitabu maisha katika kisiwa chenye hazina
j) mbwa mnyama ambaye kakangu alizoea kufuga hunisumbua

## 5.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu utungaji wa insha

## KAZI 6

***Soma maelezo muhimu yafuatayo, kisha ujibu maswali ya hapo chini***

- **Maana ya utungaji wa insha**

Utungaji ni neno linalotokana na kitenzi "kutunga". Kitenzi hiki kinamaanisha "kutoa mawazo kutoka ubongoni na kuyakusanya, kisha kuyadhihirisha kwa maandishi, kwa kusimulia, kwa kuyaimba au kwa muziki. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa, utungaji ni utoaji wa mawazo binafsi kutoka akilini mwa mtu kuhusiana na mambo mbalimbali katika jamii, kisha kuyaweka wazi kwa njia ya mdomo au maandishi. Insha ni mtungo wa maneno kwa mtindo wa nathari juu ya jambo fulani.

- **Sehemu za insha**

Insha huwa na sehemu kuu tatu ambazo ni:

- **Utangulizi (Mwanzo)**

Katika sehemu hii inampasa mwandishi atoe maelezo mafupi na maana ya habari aliyopewa.

- **Kiini cha insha (Kati/insha yenyewe)**

Sehemu hii ni insha yenyewe. Katika sehemu hii inamlazimu mwandishi afafanue kwa mapana mada anayoishughulikia huku akitoa mifano hai inayoendana na hali halisi. Kwa kawaida, sehemu hii hueleza kwa ukamilifu kila hoja iliyodokezwa katika utangulizi.

- **Hitimisho (Mwisho)**

Hii ni sehemu ya mwisho. Katika sehemu hii inampasa mwandishi kutoa mapendekezo (maoni) ya msingi au kusisitiza kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika habari yenyewe. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili.

- **Taratibu za kutunga insha**

Kwa kuweza kutunga insha vilivyo, huna budi kufuata taratibu zifuatazo:

- Kusoma kwa makini mada/kichwa/anwani uliyopewa zaidi ya mara moja, ili uielewe vizuri.
- Kufikiria mada/kichwa/anwani kwa muda.
- Kuandika mambo muhimu yatakayokuongoza katika kuiandika insha.
- Maelezo yote yatolewe kwa undani na kwa njia ya kuvutia.
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki.
- Kutumia msamiati mwafaka wa kutosha kwa kutegemea mada (kutorudiarudia maneno).
- Kutumia sentensi fupi.
- Kutumia vizuri alama za uakifishaji.
- Kutumia lugha safi na yenye adabu.
- Kuandika methali, misemo na nahau ambazo unadhania zinaweza kukufaa katika utungaji.

- **Aina za insha**

Insha ni za aina nyingi kulingana na namna zilivyoandikwa au kulingana na kusudi lake. Katika utungaji wa insha kuna insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za maelezo, insha za masimulizi, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

**Jibu maswali haya**

1. Kwa maoni yako nini maana ya insha ?
2. Kwa sababu gani katika utungaji wa insha ni lazima kuheshimu sehemu za insha ?
3. Andika sifa kuu tano za insha.

## 5.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 7**

***Tunga matini fupi ukisifu jambo/kitu/mtu fulani kisha uwasomee wenzako.***

## 5.6. Kuandika

**KAZI 8**

***Tunga insha ya wasifu kuhusu mada hii "Shule yangu."***

# SOMO LA 6: INSHA ZA MASIMULIZI

**KAZI 1**

**Tazama mchoro hapa chini kisha ujibu maswali yatakayofuata.**




1. Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro huu.
2. Wahusika hao wako wapi na wanafanya nini?

## 6.1. Kusoma na Ufahamu: Mafanikio ya Kudumu

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini**

Masengesho ni, kijana aliyezaliwa mwanapekee katika familia yake. Hakubahatika kulelewa na wazazi wake kwani walifariki angali mdogo kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Baada ya wazazi wake kufariki, alichukuliwa na kulelewa na shangazi yake. Wakati huo, alikuwa katika shule za sekondari. Alipomaliza masomo yake katika shule za sekondari, alipata cheti cha kuhitimu masomo hayo akiwa na alama nzuri. Jambo hili liliwafurahisha watu wengi wakiwemo walimu na majirani zake. Ndiyo maana ilikuwa tafrija ya kijiji kizima. Hii ni siku tuliposherehekea kupata tuzo kwa kijana hodari ambaye aliyamudu maisha yake kiasi cha kuigwa na vijana wengine.

Wengi waliompongeza siku hiyo walimletea zawadi nyingi. Alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule ya chekechea hadi kiwango alichofikia. Muda mfupi baadaye, alijiunga na vijana wenzake kufuata masomo ya muda mfupi yaliyokuwa yakitolewa kijijini hapo.

Masomo hayo yaliwalenga vijana wote waliokuwa wamemaliza masomo yao ya shule za sekondari na yalilenga kuwawezesha kuandaa miradi midogo midogo ya kujiendeleza na jinsi ya kuifanikisha. Masomo hayo yaliwafurahisha vijana wengi na Masengesho aliyasoma kwa makini; jambo lililokuwa desturi yake.

Masengesho alikuwa msichana mwenye mawazo na mtazamo imara wa maisha kiasi kwamba watu walishangaa kutokana na tabia na mienendo yake. Mafunzo yalifanyika kwa muda wa mwaka mzima akapewa cheti katika fani ya maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo. Mwezi mmoja uliofuata, Taasisi ya Maendeleo ya Rwanda ilihitaji kuajiri vijana waliokuwa wamemaliza masomo yao ili wasaidie katika kazi za ukalimani na uongozaji wa watalii kwenye vivutio vya utalii. Masengesho alipeleka ombi lake na baada ya muda mfupi akaitwa kwa mtihani na kuufaulu. Kazi ilipoanza, aliifanya kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake, wakampenda kwa uwezo wake wa kuzungumza lugha tofauti na bidii aliyokuwa akionyesha kazini.

Alifungua akaunti kwenye benki moja na kuanza kuhifadhi sehemu ya mshahara wake. Alipoona akaunti yake ilikuwa na pesa za kutosha, aliamua kuomba mkopo ili aweze kuzalisha mali katika shamba lake kubwa ambalo mpaka wakati huo lilikuwa halijatumiwa vizuri. Shamba hili lilikuwa kwenye mwinuko wa mlima na lilikuwa likiharibiwa na mmomonyoko wa ardhi. Kwa kupambana na tatizo hili, alitengeneza mifereji ya maji na kupanda miti mbalimbali karibu na shamba hilo. Aliandaa vizuri mradi wa kilimo na ufugaji, akajenga vibanda vya mifugo yake, akawaajiri baadhi ya vijana waliokuwa pamoja katika mafunzo ya muda ule mfupi, kila mmoja akapewa jukumu lake. Pamoja na kazi yake ya ukalimani, Masengesho alifuata vizuri mradi wake akanunua vifaa vilivyohitajika pamoja na gari lililokuwa likitumia umeme. Alinunua gari hili ili apunguze moshi unaochafua mazingira. Mwaka mmoja baadaye, alikuwa ameishapata mali nyingi na kuanza kujulikana nchini kote kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu.

Serikali ya Rwanda ilipotoa tuzo kwa watu waliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine, Masengesho alikuwa miongoni mwa watu waliochangia kuyaboresha maisha ya majirani zao. Kila mtu katika kijiji chetu aliitikia mwaliko wake na wengi tulikuwa tunajivunia kuwa na kijana mwerevu kama yeye. Kwa sasa ameanza kuendelea na masomo yake katika Chuo kikuu cha Rwanda ambapo anatarajia kupata shahada yake ya kwanza katika uwanja wa Ukalimani. Masengesho amekuwa mfano mzuri kwa vijana wengine wengi ambao wanapoyakumbuka maisha yake, huyaamini yaliyosemwa na wahenga kwamba" Mchumia juani hulia kivulini" na "mvumilivu hula mbivu". Wema kwa kila mtu, utulivu na upendo ni baadhi ya sifa zinazomtambulisha kijana huyu ambaye amewashangaza wengi wanaofahamu alipotoka.

## KAZI 2

**Jibu maswali haya:**

1. Eleza hali ya maisha ya Masengesho alipokuwa mtoto mdogo.
2. Kwa nini Masengesho alipewa zawadi nyingi baada ya kumaliza masomo yake ya shule za Sekondari?
3. Masomo ya muda mfupi aliyoyafuata yalihusu nini?
4. Kwa nini Masengesho alipewa tuzo?
5. Umepata funzo gani kutokana na kifungu hiki?

## 6.2. Msamiati kuhusu Mafanikio ya kudumu

## KAZI 3

***Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo. Chunguza matumizi yake katika kifungu cha habari hapo juu.***

1. Mafanikio
2. Akaunti
3. Tafrija
4. Mradi
5. Kukata tamaa

## KAZI 4

**Husisha maneno kutoka sehemu A na maana yake kwenye sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| **1. Mkalimani** | a) Malipo ya mwezi anayopewa mwajiriwa kwa kazi aliyofanya. |
| **2. Utalii** | b) Cheti maalumu chenye hadhi ya chini kuliko shahada. |
| **3. Shahada** | c) Mali inayotumika kuanzishia au kupanulia biashara au shughuli yoyote ya kuzalisha mali. |
| **4. Mshahara** | d) Matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara. |
| **5. Yatima** | e) Mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria mahali. |
| **6. Stashahada** | f) Mtu afasiriye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. |
| **7. Mtaji** | g) Kuendelea kuishi au kuwepo kwa muda wote. |
| **8. Mwaliko** | h) Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo kikuu. |
| **9. Tabia** | i) Mtoto ambaye amefiwa na wazazi. |
| **10. Kudumu** | j) Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |

## 6.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Maneno

## KAZI 5

***Chunguza maneno yaliyokolea kisha ueleze mabadiliko unayoyaona.***

- Yeye anapenda **kucheza**.
- Yeye **anacheza** mpira.
- Yeye **alichezewa** mpira.
- Yeye ni **mchezaji**.
- Wao ni **wachezaji**.
- **Mchezo** huu unapendeza.

- **Kucheza** ni kitenzi.
- **Anacheza**, **alichezewa** ni vitenzi vilivyoundwa kutokana na kitenzi kucheza.
- **Mchezaji, mchezo** ni majina yaliyoundwa kutokana na kitenzi kucheza.
- Ndani ya maneno hayo yote kuna mofimu ambayo haibadiliki **"chez."** Mofimu hii huitwa "**mzizi.**"
- Mbinu inayotumiwa kwa kupata maneno haya huitwa "**mnyambuliko"** au **uambishaji."**

**Maelezo muhimu kuhusu mnyambuliko wa maneno**

Katika mada ya kwanza tuliona kuwa mnyambuliko au uambishaji ni mbinu ya kuzalisha maneno mapya kutoka maneno mengine. Mbinu hii hufanyika kwa kuongeza kwenye sehemu fulani (viini, mizizi au mashina) za maneno hayo viambishi mbalimbali mwanzoni au mwishoni. Katika sarufi ya lugha ya Kiswahili kuna:

- Mnyambuliko wa vitenzi
- Mnyambuliko wa nomino
- Mnyambuliko wa vielezi

- **Mnyambuliko wa vitenzi**

Mnyambuliko wa vitenzi ni uundaji wa vitenzi kutoka maneno mengine. Tunaweza kupata :

- Vitenzi kutoka vitenzi
- Vitenzi kutoka majina
- Vitenzi kutoka vivumishi
- Vitenzi kutoka vielezi

- **Vitenzi kutoka vitenzi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kuongezea viambishi mbalimbali katika mzizi wa kitenzi. Viambishi hivi vinaweza kuja mwanzoni au mwishoni mwa mzizi huu.

**Mifano:** Kucheza: wanacheza- mtachezea-ulichezwa-litachezeshwa

Kupenda: wanapendana-unapendwa-zilipendwa-yanapendeza

- **Vitenzi kutoka majina**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kuongezea viambishi mbalimbali katika shina la jina. Viambishi hivi vinaweza kuja mwanzoni au mwishoni mwa shina hilo.

**Mifano:** Haya: kutahayari-wametahayarishwa-tulitahayaria-vilitahayarika

Dhuluma: kudhulumu-walidhulumiwa-hawakudhulumiwa-watadhulumiana

- **Vitenzi kutoka vivumishi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kuongezea viambishi mbalimbali vya shina la kivumishi. Viambishi hivi vinaweza kuja mwanzoni au mwishoni mwa shina hilo.

**Mifano:** Laini: kulainisha-vililainishwa-mtalainisha-yamelainika

Pana: kupanua-vilipanuka-mlipanua-yalipanuliwa-pamepanuliwa

- **Vitenzi kutoka vielezi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kuongezea kielezi au sehemu ya kielezi viambishi mbalimbali. Viambishi hivi vinaweza kuja mwanzoni au mwishoni mwa mzizi huu.

**Mifano:** Sawa: kusawazishwa-kumesawazishwa-watasawazishiana-hayakusawazishika

Karibu: Kukaribiana-watakapokaribishwa-tulipokaribishwa-yanavyokaribiana

## KAZI 6

**Unda vitenzi kutoka maneno au mofimu zifuatazo :**

- Fedheha
- Tajiri
- Fifi
- -cheka
- Zaidi
- Haraka
- Duni
- -ua
- -oa
- kali

- **Mnyambuliko wa majina**

Mnyambuliko wa majina/nomino ni uzalishaji wa majina mapya kutoka maneno mengine. Tunaweza kupata :

- Majina kutoka majina mengine
- Majina kutoka vivumishi
- Majina kutoka vitenzi
- Majina kutoka vielezi

- **Majina kutoka majina**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kubadilisha ngeli za kawaida za majina. Jambo hili linaweza kufanyika kwa kutia jina katika umoja au wingi, kwa kulidunisha, kulikuza au kulitia katika dhana ya dhahania.

**Mifano:**

| **Wastani** | | **Udogo** | | **Ukubwa** | | **Dhahania** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** | |
| Mtoto | Watoto | Kitoto | Vitoto | Toto | Matoto | Utoto |
| Mbwa | Mbwa | Kijibwa | Vijibwa | Jibwa | Majibwa | Ubwa |
| Mtu | Watu | Kijitu | Vijitu | Jitu | Majitu | Utu |
| Ng'ombe | Ng'ombe | Kigombe | Vigombe | Gombe | Magombe | Ugombe |
| Kiongozi | Viongozi | Kijiongozi | Vijiongozi | Jiongozi | Majiongozi | Uongozi |

**KAZI 7**

**Jaza jedwali lifuatalo:**

| **Wastani** | | **Udogo** | | **Ukubwa** | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| Mbuzi | | | | | |
| | | | | | Mavijana |
| | | Kijumba | | | |
| Kiti | | | | | |
| | Miji | | | | |

- **Majina kutoka vivumishi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kupachika kiambishi ngeli mbele ya shina la kivumishi.

**Mifano:** -embamba : wembamba

- rembo: urembo
- ovu: ovu, maovu, uovu
- hodari: uhodari

- **Majina kutoka vitenzi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kutia viambishi ngeli vya majina mbele ya mzizi wa kitenzi na viambishi tamati (viambishi vya kauli, viishio) nyuma ya mzizi huo. Viishio vinavyotumiwa ni –a, -e, -o, -i, -u na -aji

**Mifano**: - dunda: mdundo

- lima: mkulima-kilimo-kilimio
- pika: mpishi-upishi
- andika: mwandishi-wandikaji- uandishi

- **Majina kutoka vielezi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kupachika kiambishi ngeli mbele ya kielezi.

**Mifano:** Sawa: usawa

Mbali: umbali

Karibu: ukaribu

**KAZI 8**

**Unda nomino kutoka maneno, mashina au mizizi ifuatayo :**

- - goma
- - tamu
- -nyoa
- Sawa
- -epesi

- **Mnyambuliko wa vielezi**

Mnyambuliko wa vielezi ni uzalishaji wa vielezi kutoka maneno mengine. Tunaweza kuwa na :

- Vielezi kutoka majina
- Vielezi kutoka vivumishi

- **Vielezi kutoka majina**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kupachika kiambishi ki- mbele ya shina la nomino. Vielezi hivi ni vya namna.

**Mifano**: Mume: kiume (Ijapokuwa alipata shida alijikaza kiume.)

Mke: kike (Kabarisa anapenda kuvaa nguo za kike.)

Upuuzi: kipuuzi (Usitamke mambo ya kipuuzi mbele ya watu wazima.)

Marekani:kimarekani (Vitabu hivi vilinunuliwa kwa dola hamsini za kimarekani)

- **Vielezi kutoka vivumishi**

Mnyambuliko huu hufanyika kwa kupachika viambishi ki- na vi- mbele ya shina la kivumishi. Vielezi hivi ni vya namna au vya kiasi.

Mifano: - dog: kidogo- Kutokana na homa anatamka kidogo (namna).

Mwaka huu tumepata mvua **kidogo** (kiasi).

- zuri: vizuri- Amefanya **vizuri** katika mtihani.
- vyake: kivyake - Kila mtu anaelewa mambo **kivyake**.
- gumu: vigumu – Kwa kuwa ana masikio mazito yeye anasikia **vigumu**.

**KAZI 9**

**Unda vielezi kutoka maneno yafuatayo kisha uvitumie katika sentensi:**

- -kali
- Mnyama
- Urusi
- -ema
- Magharibi

## 6.4. Matumizi ya lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Insha za Masimulizi

**KAZI 10**

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

Insha za masimulizi ni aina ya insha ambazo ndani yake mwandishi anasimulia au anaeleza tukio fulani maalum la kweli au la kubuni kwa njia ya kisanaa.

Kama insha nyingine, insha ya masimulizi huwa na kichwa cha habari cha insha ambacho ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha. Insha ya masimulizi huwa na utangulizi ambao ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

Kiini cha insha ya masimulizi ni sehemu tunayoweza kusema kwamba ni insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua. Baada ya kiini, huja hitimisho, yaani sehemu ya mwisho ya insha ya masimulizi ambayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake. Anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

Katika kuandika insha ya masimulizi, mwandishi atazingatia mambo haya: Atabaini ni mada gani ya kuandikia na kuielewa vema. Atapanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki, atatumia mtindo unaoendana na kusudi la insha ya masimulizi. Kwa mfano, mtindo wa masimulizi unafaa kwa hadithi au insha nyingine za kisanaa. Atatumia lugha fasaha na inayoeleweka, atafuata kanuni za uandishi, kwa mfano matumizi ya alama za uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo. Mwandishi atapanga insha katika muundo wake, yaani kichwa, utangulizi, kiini na hitimisho.

**Maswali:**

1. Insha ya masimulizi ni nini?
2. Kwa sababu gani utangulizi mzuri ni muhimu katika insha?
3. Jadili sehemu kuu za insha ya masimulizi.
4. Jadili mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za masimulizi.

## 6.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 11**

***Tunga insha kuhusu kisa ulichosikia kisha uiwasilishe darasani***

## 6.6. Kuandika

**KAZI 12**

***Tunga insha ya masimulizi na sentensi ifuatayo ije mwishoni:***

... kuanzia siku hiyo ndipo nilipokubali kwamba wahenga hawakukosea waliposema « Mtegemea cha nduguye hufa maskini. »

# SOMO LA 7: INSHA ZA KUBUNI

## KAZI 1

**Tazama mchoro hapa chini kisha ujibu maswali yatakayofuata.**



a) Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro huu.

b) Wahusika hao wako wapi? Wao wanafanya nini?

c) Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

## 7.1. Kusoma na Ufahamu: Kioja katika Mbuga ya Mwangaza

**Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini**

Siku ya mazishi ya Mzee Ngedere ilikuwa siku tukufu kwa wanyamapori wote wa Mbuga ya Mwangaza. Waliamua asindikizwe kwa sherehe maalum kwa sababu mbili. Kwanza, alikuwa mpatanishi wao mwenye busara. Mizozo ilipokuwa ikizuka mbugani alikuwa akiitatua bila kupendelea upande wowote. Pili, Mzee Ngedere alikuwa muuguzi bingwa wa kienyeji aliyeheshimika sana.

Baada ya kifo cha Mzee Ngedere, umoja wa Wanyama ulivunjika. Baadhi yao walikuwa wakipendekeza mganga huyu arithiwe na Bwana Chui na wengine wengi wakimpendekeza Bi Tembo. Siku hii ya mazishi, Mfalme Simba aliamua

kulifumbia jicho jambo hili la urithi wa uganga ili Marehemu asisindikizwe kwa zogo na vurumai.

Waombolezaji walimiminika kwa wingi: wafalme na raia kutoka mbuga jirani, viongozi wa kidini na raia wa Mbuga ya Mwangaza kwa ujumla. Wanyama walijaa uwanjani hata pasipatikane nafasi ya kuweka sindano. Kila raia wa Mwangaza alijiandaa kila iwezekanavyo kuifanikisha siku hiyo. Lakini wote walifanya hivi nyoyo zikisumbuka kwa majonzi ya kumpoteza mshauri na mganga wao.

Kabla ya sala ya wafu kuanza, waombolezaji walijipanga kwa mstari mrefu na kumuaga mpatanishi na tabibu wao kitamaduni kwa kuimba nyimbo za kuomboleza na kubeba mikoba yake ya utabibu pamoja na mgwisho wake wa uungwana. Gunia lenye maiti lilibebwa kutoka nyumba ya Mzee Ngedere hadi kaburi lililokuwa karibu na kasri la Mfalme Simba.

Baada ya msafara huo, mpanga ratiba, ambaye ni Binti Sungura alimkaribisha Kasisi Nyati kuongoza sala. Wasemaji wote waliopewa fursa walikariri sifa za marehemu. Kipindi cha sifa kilipomalizika, jua lilikuwa likiwaka sana. Kila kiumbe kilikuwa kikitokwa na jasho. Wakati wa kufundisha Neno la Bwana ulipofika, kasisi wa Mbuga ya Mwangaza, Mzee Nyati, alichukua fursa akamsifu Mungu na kuwaomba wanyama wamshukuru Mungu wao. Yeye alisimama, akivaa miwani sawasawa na kufungua jarida la karatasi. Baada ya kusafisha koo lake alianza kuzungumza. Alizungumza na kuzungumza hadi wanyama wengine waanze kuota mizizi kwa sababu ya kukaa na wengine kusimama kwa muda mrefu. Bwana Chui alimwamrisha Kasisi Nyati kumaliza maneno yake wakamzike Mzee Ngedere.

Bwana Chui alisema haya huku akipanga kumrithi Mzee Ngedere kwa sababu alikuwa makamu wake. Aliposikia hayo, Bi Simba alilia kwa kwikwi huku akimwomba Mungu amrudishe mpatanishi wao kwa sababu Bwana Chui alikuwa akiogopwa na wanyama wengi kwa ukatili wake. Alikuwa hawapokei vizuri walipokuwa wakimpelekea malalamiko yao.

Kimya kizito kilitawala kati ya wanyamapori. Kitambo, wingu jeusi lilipita na kuwatisha wote waliokuwa hapo. Kunguru moyo ulimdundadunda na kujitayarisha kukimbia akisema kuwa shetani kapita. Kusikia hayo Mfalme Simba alimshauri kutowatisha kwa kusema mambo ya kishenzi.

Mara gunia lilianza kutikisika na kuonyesha dalili ya kuwa ndani mlikuwamo kiumbe hai. Kasisi Nyati alipoona hayo alianza kutokwa na jasho kubwa hadi mwili mzima ukalowa maji. Lo! Wanyama wengi walitimuka na kutawanyikia vichakani na porini. Kasisi Nyati naye hakuweza kuhimili kioja hicho. Bila ya kuvua joho lake naye alitimka mbio na kufuata wafuasi wake. Mfalme Simba na Bwana Chui walijizatiti na kubaki pale ili wajionee kilichokuwa kikijili hapo huku wakiwashauri wenzao kutokimbia.

Baada ya muda mfupi walimwona Mzee Fuko, mke na watoto wake wawili wakijitokeza chini ya gunia wakidai kuja kumzika Mzee Ngedere. Bi Fuko alipotaka kujua sababu iliyowafanya wanyama kutimuka, alielezwa kwamba labda walidhani kwamba Mzee Ngedere amefufuka. Bada ya hapo, Bwana Chui alitumwa kuwarudisha wanyama kwa sababu kulikuwa hakuna jambo la kuwafanya wakimbie.

Baada ya kupata taarifa, wanyama walirudi na kumzika mganga na mpatanishi wao mpendwa. Mazishi yalipomalizika, Bi Tembo alichaguliwa kuwa mpatanishi. Nafasi ya makamu akapewa Binti Sungura. Bwana Chui alipotaka kuzusha ghasia alionywa kuwa angefunguliwa mashtaka kwa kosa la uchochezi wa ghasia. Kwa kusikia hayo, aliomba msamaha, akaahidi kugeuka mzalendo mwema. Aliwaambia wafuasi wake kutimiza masharti ya Mfalme Simba. Tangu siku hiyo hali ya utulivu ilirudi. Upendo na amani ikatawala katika Mbuga ya Mwangaza.

**KAZI 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja sifa mbili muhimu za Marehemu Mzee Ngedere.
2. Ni waombolezaji gani waliokuwa hapo?
3. Kasisi Nyati alikuwa akivaa namna gani?
4. Ni nani aliyesema kwamba shetani alipita?
5. Unafikiri ni kwa sababu gani gunia lilikuwa likitikisika?

## 7.2. Msamiati kuhusu Kifungu

**KAZI 3**

***Toa maana ya maneno yafuatayo:***

1. Kioja
2. Mazishi
3. Waliamua
4. Majonzi
5. Kasri

## KAZI 4

***Toa neno jingine lililotumiwa katika kifungu lenye maana sawa na ya lile lililopigiwa mstari chini.***

1. Leo ni siku **nzuri sana**.
2. Bwana Kagabo alikuwa **tabibu** **mashuhuri**.
3. Baada ya kifo cha Maria watoto wake walilia kwa **simanzi**.
4. Miongoni mwa vitambulisho vya mfalme wa kijadi mlikuwamo **usinga**.
5. Si vizuri kama mtu awe **ibilisi** wa mwenzake.

## 7.3. Sarufi: Mnyumbuliko wa Vitenzi

## KAZI 5

**Chunguza maneno yafuatayo kisha ueleze mabadiliko unayoyaona.**

1. Maria ana hamu ya **kuongoza** wenzake.
2. Si vizuri **kuongozwa** kwa mabavu.
3. Kalisa anafanya kazi ya **kuongozea** watoto majirani wanapoenda shuleni.
4. Kwa kuwa dereva alikuwa amelewa chakari alilazimishwa **kuongozewa** gari.
5. Raia mwema anapoongozwa vizuri anashauriwa kukubali **kuongozeka**.
6. **Kuongozana** njiani ni ishara ya heshima na adabu.
7. Kalisa na Joni hupenda **kuongozeana** magari.

- **Kuongoza:** ni kitenzi
- **Kuongozwa, kuongozea, kuongozewa, kuongozeka, kuongozana, kuongozeana:** ni vitenzi vilivyoundwa kwa kutoka kitenzi "**kuongoza.**" Kusema kuwa kitenzi hiki "**kuongoza**" kimerefushwa kwa kuongezewa viambishi mbalimbali na kupata maana mpya. Mbinu hii inayotumiwa kwa kurefusha kitenzi huitwa "**mnyumbuliko**".

## Maelezo muhimu kuhusu mnyumbuliko

### Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini

Mnyumbuliko wa kitenzi ni mbinu ya kurefusha kitenzi. Mbinu hii hufanyika kwa kuongezea mzizi wa kitenzi viambishi tamati. Kiambishi tamati ni mofimu yoyote inayokuja baada ya mzizi wa kitenzi. Viambishi tamati vinavyotumiwa katika mnyambuliko ni viambishi tamati vya kauli. Viambishi tamati vya kauli ni viambishi vinavyoongezea mzizi wa kitenzi maana mpya yenye kauli fulani. Kuna:

- **Kauli ya kutendea: -il-**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za Kimofolojia |
|---|---|---|
| Kuenda | Kuendea: ku-end-il-a | l → Ø/I-I, i → e/Ze- |
| Kucheza | kuchezea :ku- chez-il-a | l → Ø/I-I, i → e/Ze- |
| Kulima | Kulimia: ku-lim-il-a | l → Ø/I-I |

- **Kauli ya kutendesha: -ish - ,- z-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za Kimofolojia |
|---|---|---|
| Kuenda | Kuendesha: ku-end-ish-a | i → e/Ze- |
| Kucheza | kuchezesha :ku- chez-ish-a | i → e/Ze- |
| Kulima | Kulimisha: ku-lim-ish-a | l → Ø/I-I |
| Kulala | Kulaza: ku-lal-y-a | l+y → z |
| Kuoa | Kuoza: ku-ol-y-a | l+y → z |

- **Kauli ya kutendana: -an-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko |
|---|---|
| Kupenda | Kupendana: ku-pend-an-a |
| Kupiga | Kupigana: ku-pig-an-a |
| Kuona | Kuonana: ku-on-an-a |

- **Kauli ya kutendwa: -w-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko |
|---|---|
| Kupenda | Kupendwa: ku-pend-w-a |
| Kupiga | Kupigwa: ku-pig-w-a |
| Kuona | Kuonwa: ku-on-w-a |

- **Kauli ya kutendewa: -iw-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za kimofolojia |
|---|---|---|
| Kulima | Kulimiwa: ku-lim-iw-a | - |
| Kupiga | Kupiwa: ku-pig-iw-a | - |
| Kutenda | Kutendewa: ku-tend-iw-a | i → e/Ze- |

**Hali ya kutendeka: -ik-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za kimofolojia |
|---|---|---|
| Kukata | Kukatika: ku-kat-ik-a | - |
| Kupika | Kupikika: ku-pik-ik-a | - |
| Kula | Kulika: ku-li-ik-a | i → Ø/-I |

**Kauli ya kutendua: -ul-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za kimofolojia |
|---|---|---|
| Kufunga | Kufungua: ku-fung-ul-a | l → Ø/I-I |
| Kupanga | Kupangua: ku-pang-ul-a | l → Ø/I-I |
| Kufumba | Kufumbua: ku- fumb-ul-a | l → Ø/I-I |

- **Kauli ya kutendelea dumishi: -il-il-/-ang-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko | Kanuni za kimofolojia |
|---|---|---|
| Kupiga | Kupigilia: ku-pig-il-il-a | l → Ø/I-I |
| Kufinya | Kufinyanga: ku-finy-ang-a | - |

- **Kauli ya kutendama: -am-**

**Mifano:**

| Kitenzi cha asili | Kitenzi cha mnyumbuliko |
|---|---|
| Kificha | Kufichama: ku-fich-am-a |
| Kupinda | Kupindama: ku-pind-am-a |

## KAZI 6

**Jibu maswali haya**

1. Mnyumbuliko ni nini?
2. Mnyumbuliko unatofautianaje na mnyambuliko?
3. Tumia vitenzi vifuatavyo huku ukizingatia kauli ya vitenzi.

a) Kamana alim............simu mamake (piga).
b) Moto huu uli............na nani (washa)?
c) Barua hii ita.............na katibu wetu (andika).
d) Samaki hawa wame............katika Ziwa Rweru (vua).
e) Biharusi yule ame..........veli zuri (vaa).

## 7.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Insha za Kubuni

## KAZI 7

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

**Maelezo Muhimu kuhusu Insha za Kubuni**

Insha za kubuni ni aina ya insha ambazo hutungwa kuhusu mawazo yanayozuliwa na ambayo si matukio ya kawaida.

Kama insha nyingine, insha ya kubuni huwa na kichwa cha habari cha insha ambacho ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, sehemu ya katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha. Insha ya kubuni huwa na utangulizi ambao ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

Kiini cha insha ya kubuni ni sehemu tunayoweza kusema kwamba ni insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua. Baada ya kiini, huja hitimisho, yaani sehemu ya mwisho wa insha ya kubuni ambayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake. Anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

Insha za namna hii humhitaji mwandishi kujiweka kimawazo katika hali fulani ya kubuni na kutunga insha katika hali hiyo. Kwa hivyo, ili mwandishi afaulu katika uandishi wake, ni sharti awe na uwezo wa kubuni mawazo kwa undani na pia kuweza kuyaeleza mawazo hayo kwa njia ya kuaminika kwa wasomaji.

***Tanbihi:*** *Kuwepo kwa insha za kubuni hakuondoi ukweli unaosema kwamba insha zote hutokana na ubunifu wa mwandishi. Hivi ni kwa sababu aina zote za insha huwa zinaandikwa kwa mawazo yanayobuniwa na akili ya mwandishi.*

**Jibu maswli yafuatayo:**

1. Kifungu cha habari ulichosoma hapo juu kuhusu *Kioja katika Mbuga ya Mwangaza* ni aina gani ya insha? Kwa sababu gani?
2. Ni jambo gani mwandishi wa insha ya kubuni anapaswa kuzingatia kabla ya kuandika?
3. Ni mambo gani yanayojitokeza katika insha ya kubuni na insha nyingine?

## 7.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 8**

***Sikiliza hadithi kwenye redio halafu utunge insha ya kubuni kisha uwasomee wenzako.***

## 7.6. Kuandika

**KAZI 9**

***Soma jinsi insha hii ilivyoanza na kuendelea kubuni mpaka ikamilike.***

Mwezi Mahakamani

Wakati wa kesi ya Mwezi ulipowadia, viumbe na wanyama wote walijitayarisha vilivyo ili waende kusikiliza kesi hiyo. Ndege, wanyama wa baharini, wanyamapori na hata mifugo, walikuwa wamealikwa. Mwezi ulikuwa ukishitakiwa kwa kosa la kuchoma msitu wa Pambano na kusababisha ukame mbugani.

Siku hiyo ilikuwa tofauti na siku nyingine. Asubuhi ya siku hiyo kulitokea maajabu yaliyofanya nyoyo za viumbe wote wa hapo mbugani na majirani kudundadunda kwa hofu. Kwanza, jua halikuchomoza kutokea Mashariki kama kawaida yake bali lilionekana likiwa Magharibi. Kwa kuona hayo Mzee Jogoo aliwika na ...

## Tathmini ya mada

1. Sehemu kuu za insha ni zipi?
2. Taja aina za insha
3. Ni nini tofauti kati ya kunyumbua na kunyambua?
4. Alama zifuatazo huitwa namna gani na hutumiwa wapi?
   ! ,...,
5. Unda vitenzi kutoka maneno au sehemu za maneno zifuatazo:

- - nono
- neno
- -kali
- sawa
- Jitihada

6. Jaza jedwali lifuatalo

| Kutenda | Kutendea | Kutendwa | Kutendesha | Kutendana | Kutendeka |
|---|---|---|---|---|---|
| vaa | | | | | |
| | | | | | lika |
| | letea | | | | |
| | | vuliwa | | | |
| | | | laza | | |
| | | | | oana | |

# MADA YA 4

# HOTUBA

## Uwezo mahususi

Kuandaa hotuba na kuisimulia hadharani

- **Malengo ya ujifunzaji**

- Kubainisha sehemu kuu za hotuba,
- Kueleza mwongozo wa kutunga hotuba nzuri,
- Kuonyesha tofauti iliyopo kati ya hotuba na aina mbalimbali za insha,
- Kueleza tofauti kati ya usemi wa asili na usemi wa taarifa.

## Kidokezo

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyo hapo chini yake**



1. Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro hapo juu wanaweza kuwa katika shughuli gani?
2. Mhusika aliyesimama unafikiri anafanya nini katika shughuli hiyo?

# SOMO LA 8: MAANA YA HOTUBA

## 8.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Afisa wa Umoja na Maridhiano wilayani kwa Wananchi

**Soma hotuba ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini:**

Ndugu zangu wananchi, ndugu zangu wazalendo na ndugu zangu wazawa. Hamjambo!

Ninasimama mbele zenu leo hii ili tuzungumzie kuhusu umoja wa Wanyarwanda. Hebu tujitazame leo tunaishi vipi? Je, tunaishi kwa umoja kama Wanyarwanda?

Kabla sijasonga mbele, ningependa tukumbushane historia ya nchi yetu kuhusu umoja. Hapo zamani za kale, katika enzi za ufalme, Wanyarwanda walikuwa na umoja thabiti. Wote walikuwa wakimheshimu mfalme kwa pamoja bila ya ubaguzi wowote. Mizozo midogo midogo ilipokuwa ikitokota ilikuwa ikitatuliwa kidugu katika familia au katika vikao vya waungwana. Matatizo hayo yalikuwa yakihusiana na kama vile mifugo au mashamba. Matatizo magumu yalikuwa yakitatuliwa na viongozi na hata mfalme mwenyewe.

Wakati huu, umoja wetu ulikuwa ukirutubishwa na sherehe au hafla mbalimbali. Mtu alipokuwa akitaka kujenga nyumba, majirani walikuwa wakimpa msaada "umuganda" kwa Kinyarwanda. Aliyekuwa na harusi, majirani walikuwa wakimpa msaada kama vile kazi za nyumbani zihusuzo matayarisho ya shughuli za harusi, pombe, n.k. Kwa kuonyesha urafiki wa hali ya juu, Wanyarwanda walikuwa wakichanganya damu na kuzawadiana mifugo hasa ng'ombe. Wakati wa vita, Wanyarwanda walikuwa wakipigania usalama wa nchi yao kwa pamoja bila ubaguzi wowote. Kwa upande wa malezi, mtoto alikuwa akikanywa na mtu mzima yeyote yule katika jamii.

Ndugu zangu wananchi, wakati wa enzi za ukoloni, umoja wa Wanyarwanda ulivunjika. Kwanza, wakoloni hawa walidunisha ufalme na watu wengi wakaanza kugoma. Walivunja nguzo zote zilizokuwa zikishikilia umoja wa Wanyarwanda. Kitu kibaya mno walichotufanyia na ambacho hatuwezi kukisahau, walituletea makabila. Makabila haya yalipofika yalitenganisha watu: ndugu, mzazi na mtoto, mke na mume, walianza kuangaliana kwa kijicho na husuda.

Baada ya uhuru, mambo yaligeuka balaa zaidi. Wanyarwanda wengi walianza kuuawa na Wanyarwanda wenzao. Hawa wa nyuma waligawana mashamba yao na mifugo yao, walichoma nyumba zao na kuwakimbiza hadi nchi jirani. Uvunjikaji huu wa umoja wetu ndio uliotufikisha kwenye mauwaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yaliyotokea nchini mwetu mnano mwaka wa 1994.

Afisa: Umoja oyee!

Wasikilizaji: Oyee! Oyee!

Afisa: Amani oyee!

Wasikilizaji: Oyee! Oyee!

Afisa: Utengano zuu!

Wasikilizaji: Zuu!

Ndugu wananchi wenzangu, wahenga walisema yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Yaliyopita yalipita lakini yalituachia kovu kubwa. Yawe somo kwetu. Siku hizi tunapaswa kusimama kidete na kuendelea na safari yetu ya kuendeleza nchi. Safari hii si ya mtu mmoja pekee bali ni safari ya sisi sote Wanyarwanda. Kwa hiyo, ninawaomba tuungane mikono. Serikali yetu ilipewa jina zuri "Serikali ya Umoja wa Wanyarwanda." Umoja huu unapaswa kuwa uti wa mgongo wa maisha yetu kama Wanyarwanda. Tuishi kwa umoja, tusaidiane vilivyo kwa lolote lile. Haya yatakapotendeka, nchi yetu inakuwa paradiso ya Afrika na majirani zetu watatumezea mate.

Ninawashukuru kwa kunitegea masikio na nina imani kuwa kuanzia leo mnakwenda kuimarisha umoja wetu zaidi ya sasa.

Asanteni!

## KAZI 1

**Jibu mwaswali yafuatayo:**

1. Hotuba hii ilitolewa na nani?
2. Mantiki ya hotuba hii ni ipi?
3. Taja mambo matatu yaliyokuwa yakionyesha umoja wa Wanyarwanda katika enzi za ufalme.
4. Kitu kibaya kilicholetwa na wakoloni ni kipi?
5. Kitu hiki kilikuwa chanzo cha nini?

## 8.2. Msamiati kuhusu Hotuba

**KAZI 2**

**Eleza maana ya maneno yafuatayo:**

- Enzi
- Thabiti
- Ikizuka
- Akikanywa
- Kugoma

## 8.3. Sarufi: Kueleza Tofauti kati ya Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa

**KAZI 3**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha ueleze mabadiliko unayoyaona:**

a) « Mwanafunzi huyu ni mtiifu, » mwalimu alisema.

b) Mwalimu alisema kuwa mwanafunzi huyo/yule alikuwa mtiifu.

c) "Tuishi kwa pamoja na tusaidiane vilivyo," Afisa aliwaambia wanakijiji.

d) Afisa aliwaambia/ aliwaonya wanakiji kuishi kwa umoja na kusaidiana vilivyo.

**Maelezo muhimu: Maana ya usemi wa asili na usemi wa taarifa**

- **Usemi wa asili**

Ni yale maneno yanayotamkwa na mtu katika **hali ya kwanza** .

- **Usemi wa taarifa**

Iwapo mtu anataka kuwaambia wengine maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila kupotosha, kupunguza au kuongeza maana ya jambo analotaka kulitolea maelezo, basi maneno hayo anayoyasema ni ``**usemi wa Taarifa**.``

- **Mambo muhimu katika usemi wa taarifa**

Wakati wa kuandika usemi wa taarifa kuna mambo muhimu ya kuzingatiwa ili usemi huo uwe wa taarifa sahihi.

1. Nafsi ya kwanza hubadilika na kuwa nafsi ya tatu

**Mimi** hugeuka kuwa **yeye**

**Sisi** hugeuka kuwa **wao**

**Mfano:**

- "Mimi ninasoma kwa bidi," mtoto alisema.
    - Mtoto alisema kuwa yeye alisoma kwa bidi.
- "Sisi tulisoma kwa bidi," watoto walisema.
    - Watoto walisema kuwa wao walisoma kwa bidi.

2. Badala ya kutumia wakati uliopo, wakati uliopita –li- ndio hutumika.

**Mfano**: Nina kazi nyingi ofisini.

- Alisema kwamba alikuwa na kazi nyingi ofisini.

3. Alama za kufunga na kufungua maneno **hazitumik**i kwenye usemi wa taarifa .
4. Alama za kuuliza na kushangaa hazitumiki kwenye usemi wa taarifa
5. Katika usemi wa taarifa mahali penye wakati ujao -**ta**- kwenye usemi wa asili hugeuka kuwa -**nge**-

**Mfano: "Nitaondoka kuelekea Kigali," shangazi alisema.**

- Shangazi alisema kuwa angeondoka kuelekea Kigali.

6. Baadhi ya maneno hubadilisha nyakati yanapotumika katika usemi wa taarifa .

kama :

**Hapa** huwa **hapo**

leo huwa ---siku hiyo/ile

wakati huu ------------wakati huo

kwetu -------kwao

kwangu ------kwake

sasa -----wakati huo/ule

**Mfano:**

- "Nitaondoka sasa," mgeni alisema.
    - Mgeni alisema kuwa angeondoka wakati huo/ule.

- "Tutacheza leo uwanjani," wanafunzi walisema.
    - Wanafunzi walisema kuwa wangecheza siku hiyo/ile uwanjani.

7. Mojawapo ya maneno yafuatayo hutumika katika usemi wa taarifa

   Kuwa----kama ----kwamba

**Mfano:** -" Utanikuta mjini jioni hii, "Juma alimweleza rafiki yake.

- Juma alimweleza rafiki yake kuwa angemkuta mjini jioni ile.

**KAZI 4**

**Weka sentensi hizi katika usemi wa taarifa**

1. **"**Mnapaswa kwenda shuleni leo,"Alisema mwalimu**.**
2. "Leo kazi ni nzito" Alisema mkuu wa vibarua.
3. "Ulipanda miti mingapi," Mwalimu aliniuliza.
4. "Ni nani atafagia kesho?" Kiranja aliuliza.
5. "Tunapaswa kuungana mikono ili kuendeleza nchi yetu," Waziri alinena.

## 8.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Hotuba

**KAZI 5**

***Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini***

### Hotuba

**i) Maana ya hotuba**

Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya kundi la watu. Hotuba inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kutaka kuhimiza kazi, kufanya kampeni fulani, kutoa taarifa fulani kwa watu.

**ii) Aina za hotuba**

a) **Mahubiri**: Ni hotuba za mafundisho ya kidini, zinazotolewa makanisani, misikitini, n.k.

b) **Hotuba za kisiasa**: Ni hotuba zihusuzo taarifa ya serikali kama vile kuwahimiza watu na kuwaalika kutenda jambo fulani, n.k.

c) **Mihadhara**: Ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi na hasa wanafunzi wa vyuo vikuu.

### iii) Sifa za hotuba

- Ukweli wa habari na taarifa
- Kujua vizuri aina ya watu unaowatolea hotuba, umri wao, kazi zao, n.k.
- Ufasaha wa lugha ili iweze kupendeza na kueleweka vizuri
- Nidhamu au adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu
- Mantiki nzuri au mfuatano mzuri wa mawazo
- Sauti ya kusikika vizuri
- Kuvaa vizuri.

### iv) Tofauti kati ya hotuba na insha

#### A) HOTUBA

- Hotuba hutoa maneno halisi ya mzungumzaji/hatibu/kiongozi anapozungumzia hadhira kuhusu jambo fulani.
- Mwandishi wa hotuba hatakiwi kuweka alama za kunukuu anapoanza hotuba yake
- Mara nyingi hotuba huwa katika nafsi ya pili
- Hotuba inaweza kutolewa na kiongozi wa kisiasa, utawala, kidini, kikundi, shirika fulani, daktari, n.k
- Hotuba huanza kwa kutambua hadhira (waliohudhuria mkutano)
- Waliohudhuria mkutano hutajwa kwa vyeo vyao kuanza kwa yule wa cheo cha juu hadi wa chini k.m: Waziri wa Elimu, Mkuu wa Wilaya, mabibi na mabwana,……..
- Hatibu akiwa anawazungumzia hadhira isiyomjua, lazima ajitambulishe
- Katika hotuba, hatibu hutoa mapendekezo
- Mwisho wa hotuba humalizika kwa shukurani.

#### B) INSHA

- Mwandishi wa insha anaweza kunukuu yaliyosemwa na wengine
- Insha inaweza kuwa na mada ambayo mwandishi anatakiwa kutetea au kupinga
- Katika insha mwandishi hataji vyeo vya hadhira
- Katika insha nyingi, mwandishi hatoi mapendekezo
- Mwisho wa insha hupangwa katika aya na haumaliziki kwa shukurani

**Maswali**

1. Eleza maana ya hotuba
2. Hotuba hutolewa kwa lengo gani?
3. Taja aina za hotuba
4. Eleza sifa muhimu za hotuba

## 8.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 6**

**Jadili kuhusu "Umuhimu wa hotuba"**

## 8.6. Kuandika

**KAZI 7**

**Wewe ni mwakilishi wa wanafunzi wa mwaka wa tatu chuoni kwako. Tunga hotuba kuhusu mada ya usafi wa mazingira.**

# SOMO LA 9: MUUNDO WA HOTUBA

**KAZI 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

**a)** Unaelewa nini kuhusu neno hotuba?

b) Ni hotuba gani uliyoisikiliza ikakufurahisha?

## 9.1. Kusoma na Ufahamu: Kazi ni Kazi

**Soma hotuba ya Katibu mtendaji wa wilaya katika harakati za uzinduzi wa elimu ya kujitegemea kwa vijana « Kazi ni Kazi » katika Tarafa ya Amani wilaya ya Tujitegemee**

Katibu: Kazi oyee !

Vijana: oyee ! Oyee ! Oyee !

Katibu: Uzembe zii !

Vijana: Zii !

Mheshimiwa Katibu Mtendaji wa Tarafa ya Amani,

Waheshimiwa wakurugenzi wa shule na vyuo

Waheshimiwa vijana,

Mabwana na mabibi mliokusanyika hapa,

Hamjambo?

Vijana ni nani ambaye hapendi kuishi? Sote tunapenda kuishi tena bila shaka kwa raha. Licha ya hivyo, ili tuishi maisha ya raha mstarehe tunahitaji kufanya kazi. Kazi ndio msingi wa uhai wa binadamu. Mtu asipofanya kazi hawezi kuyapata mahitaji yake ya kila siku.

Kazi siyo adhabu kwani binadamu ameumbwa ili afanye kazi; ndiyo maana ana akili, mikono, miguu, na viungo, vingine vya mwili. Viungo vyote hivi lazima vifanye kazi ili maisha yawe mazuri. Mtu anahitaji kula, kuvaa na kuishi mahali pazuri. Lakini ili kuyapata mahitaji yote, ni lazima afanye kazi. Hivyo basi, tunalazimika kufanya kazi kwa kuwa kazi ni kitendo cha maendeleo. Maendeleo ya mtu huletwa na kazi. Binadamu hupiga hatua za kwenda mbele kimaendeleo akifanya kazi kwa bidii. Bila kufanya kazi, maendeleo ya nchi husimama ama hurudi nyuma.

Kazi ni za aina nyingi. Kuna kazi zinazotolewa na serikali au makampuni fulani na kazi za kujitegemea. Kazi zote hizo ni kama vile kilimo, ufugaji, ujenzi, uchukuzi, ulindaji wa usalama, ufanyabiashara na kadhalika. Kazi hizi zote zipo ili kujenga nchi yetu. Hii ni kwa sababu nchi yetu itajengwa na mikono ya wananchi wake. Siku hizi kuna wale wanaochagua kazi na kupuuza nyingine ati si kazi za heshima. Msemo wa Kinyarwanda unasema « Hakuna kazi mbaya isipokuwa kuiba na kuroga. » na Waswahili husema « Kazi mbi si mchezo mwema.»

Siku hizi kuna ongezeko la wasomi. Ongezeko hili halilingani na kazi zinazotolewa na serikali yetu au makampuni na mashirika ya kibinafsi. Ndiyo maana tunahimizwa sisi wenyewe kujitengenezea kazi za kibinafsi (kujiajiri). Sote hatuwezi kukaa ofisini. Tuna mikono na akili, tengeneza kazi na usitegemee wengine kwani « Mtegemea cha nduguye hufa maskini. »

Kazi ni wajibu wa kila mtu. Kila mtu analazimika kufanya kazi ili atoe mchango wake katika maendeleo ya jamii. Mtu ni sehemu ya jamii. Kama mtu hafanyi kazi hulegeza maendeleo ya jamii na matokeo yake ni kwamba jamii hukumbwa na umaskini. Vijana, mnataka nchi yetu iendelee kuitwa maskini? Hapana! Nchi yetu inapaswa kusonga mbele kama nchi nyingine zilizoendelea. « Mkiona vyaelea vimeundwa. » Nchi zile zilizoendelea zilifikia kwenye kiwango kile kutokana na juhudi, uzalendo na bidii ya raia wao. Kwa hiyo fukuzeni uvivu, ugoigoi na uzembe. Saidieni serikali yetu katika kazi za « umuganda.»

Vijana kumbukeni kuwa kazi ni bakora ya kuondosha umasikini maishani. Ili kuwa na maisha bora, ni lazima kufanya kazi. Kumbuka kuwa hakuna mtu mwingine atakayekufanyia kazi. Aidha, kumbuka kuwa jamii isiyofanya kazi ni jamii yenye watu waliokufa. Kwa hiyo, kila mmoja akumbuke kutimiza wajibu wake. Msemo wa Kinyarwanda unasema « Asiyefanya kazi hapaswi kula. »

Leo ningependa nitie nanga hapa. Ninawashukuru kwa kunitegea masikio. Kuanzia leo tuzidi kuchapa kazi ipasavyo. Hii ni kwa kuwa "Kazi ni kazi, la muhimu mtu amudu maisha."

Asanteni!

**KAZI 2**

**Maswali ya Ufahamu**

1. Nani aliyekuwa mgeni rasmi kwenye hotuba hii ?
2. Mkutano ambamo kulitolewa hotuba hii ulifanyikia wapi?
3. Taja watu waliokuwepo katika mkutano huo.
4. Ili binadamu aweze kuishi vizuri yampasa kufanya nini?
5. Maneno « kazi ni kazi » yanamaanisha nini katika kifungu cha habari
6. « Kazi ni wajibu wa kila mtu ». Eleza maana ya msemo huu.
7. Kwa nini binadamu analazimika kufanya kazi ?

## 9.2. Msamiati kuhusu Hotuba ya Katibu Mtendaji

**KAZI 3**

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kutoka kifungu cha habari:**

1. Hotuba
2. Kujitegemea
3. Kazi
4. Mkutano

## KAZI 4

**Husisha maneno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B**

| A | Neno | B Maana ya neno |
|---|---|---|
| 1. | Hotuba | a) Shughuli anayoifanya binadamu katika kumudu maisha |
| 2. | Kujitegemea | b) Hali ya mtu kuwa tayari kufia nchi yake |
| 3. | Raha | c) Mtu/ mwanadamu /kiumbe hai mwenye akili |
| 4. | Kazi | d) Hali ya kutokuwa na shida au usumbufu |
| 5. | Binadamu | e) Mkusanyiko wa watu |
| 6. | Uzalendo | f) Kujitosheleza katika mahitaji |
| 7. | Jamii | g) Maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya watu |

## 9.3. Sarufi: Tofauti kati ya Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa

## KAZI 5

**Eleza tofauti iliyoko baina ya usemi wa asili na usemi wa taarifa.**

**Maelezo Muhimu**

Usemi wa asili ni yale maneno yanayotamkwa na mtu katika hali ya kwanza lakini usemi wa taarifa ni kurudia maneno yaliyosemwa na mtu kwa njia nyingi bila kupotosha maana ya kwanza. Usemi wa asili hutumia alama za mtajo, kuuliza na kushangaa lakini usemi wa taarifa huishia kwa nukta. Katika usemi wa taarifa nyakati na nafsi za vitenzi vilivyotumiwa katika usemi wa asili hubadilika.

## KAZI 6

**Geuza sentensi zifuatazo katika usemi wa asili au wa taarifa**

1. “Tungepanda miti mingi mvua ingenyesha” Wanakijiji walisema.
2. Katibu mtendaji aliwaambia vijana kuwa wakiona vyaelea vimeundwa.
3. “Nitakapohitimu masomo yangu nitajitafutia mradi wa kuzalisha mali,” Kalisa alieleza.

4. "Ugonjwa wa UKIMWI una dalili gani?" Raia mmoja alimuuliza Daktari.
5. Kiongozi aliagiza vijana kutoa mikono mifukoni na kuchapa kazi.

## 9.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo muhimu Kuhusu Muundo wa Hotuba

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini.**

- **Muundo wa hotuba**

**Hotuba ina sehemu zifuatazo:**

1. **Anwani**: Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua mada ya hotuba. Hiki ndicho kichwa chake hotuba.

**Mfano:** Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda  katika Sikukuu ya Mashujaa.

2. **Utangulizi**: Mazungumzo katika utangulizi yanatoa mwangaza ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano. Wataje kwa majina au vyeo vyao kuanzia kwa yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana. Kumbuka kwamba huhitaji kuwasalimia. Kuwatambua kwa vyeo vyao vya pekee kunatosha.

**Mfano:** Waziri wa Elimu, Gavana wa Jimbo la Kusini, Mkuu wa Wilaya ya Nyanza, Wanachama wa kikundi hiki cha Elimu Bora, mabibi na mabwana. Ni matumaini yangu kwamba nyote mna afya nzuri.

3. **Mwili/Kiini**: Hakikisha kuwa kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisi wala si wa taarifa. Panga mawazo kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo muhimu lazima lianze kuzungumziwa kwa ukamilifu halafu lifuatiwe na mawazo mengine, nayo kwa kikamilifu.
4. **Mwisho**: Hapa mazungumzo yajumlishe mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha. Ni vizuri kwa hotuba kufungwa kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji.

- **Sifa za hotuba**

**Hotuba safi huzingatia mambo haya:**

- Ukweli wa habari na taarifa: Ni lazima mhutubi ahakikishe kuwa yale anayozungumzia yana uhusiano na ukweli.

- Ufasaha wa lugha: lazima mhutubi kutumia lugha fasaha, nzuri, safi na yenye kusikika vizuri kwa kila msikilizaji. Si vizuri kutumia lugha ya mafumbo.
- Mantiki nzuri: Ni lazima kuweka kwa mfuatano mzuri wa mawazo au fikra.
- Nidhamu: Yaani adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu.
- Sauti ya kusikia wazi pamoja na ishara zinazoeleweka na zinazohusiana na yasemwayo. -Ishara hizo si za lazima iwapo hotuba inatolewa kwa njia ya redio.
- **Umuhimu wa hotuba**

**Hotuba huwa na umuhimu kwa mhutubu na kwa wanaohutubiwa. Umuhimu huo ni kama vile:**

- Kujenga ushirikiano
- Kuheshimiana
- Huondoaa ubaguzi wa kijinsia
- Huhamasisha watu kuwa viongozi walio bora
- Huwahamasisha watu kukuza vipawa na kushiriki katika kuonyesha vipaji mbalimbali kama michezo ya kuigiza n,k kwa kusikiliza hotuba zitolewazo.

**Maswali**

1. Hotuba inatarajiwa kuwa na sehemu zipi?
2. Katika kuanza hotuba yake, mhutubi hufanya nini?
3. Habari yenyewe hutolewa katika sehemu gani? Kwa nini?
4. Mwisho wa hotuba una maumbile gani?

## 9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Hotuba

**KAZI 7**

**Tunga hotuba kulingana na mojawapo ya mada zifuatazo kisha uwasomee wenzako:**

a) Umoja wa Wanyarwanda
b) Usawa wa kijinsia
c) Kazi za umuganda katika ujenzi wa taifa

## 9.6. Kuandika: Ufupisho wa Hotuba

**KAZI 8**

***Soma hotuba ya Katibu mtendaji wa wilaya katika harakati za uzinduzi wa elimu ya kujitegemea kwa vijana wa Tarafa ya Amani na uifupishe katika aya moja yenye mistari kumi.***

**Tathmini ya mada**

1. Eleza kwa ufupi maana ya hotuba?
2. Ni hatua zipi utakazozizingatia katika kuifupisha hotuba?
3. Ni mambo gani ya kuzingatia katika hotuba?

# MADA YA 5

# UANDISHI WA RIPOTI

## Uwezo mahususi

Kuandika ripoti kuhusu mafunzo ya wanafunzi wanaojiandaa kumaliza masomo yao ya ualimu

### Malengo ya ujifunzaji

- Kutaja aina za ripoti na sifa zake muhimu,
- Kuonyesha mbinu na taratibu za kutunga ripoti za aina mbalimbali,
- Kubainisha mazingira mbalimbali ya kutolea ripoti,
- Kuonyesha vipashio vya tungo za Kiswahili.

### Kidokezo

***Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyo hapo chini yake***



1. Eleza kuhusu wahusika unaowaona kwenye mchoro hapo juu
2. Wahusika hawa wanafanya nini?
3. Ni vifaa gani unavyoona kwenye mchoro huu?

# SOMO LA 10: MAANA YA RIPOTI

## 10.1. Kusoma na Ufahamu: Ziara ya Kielimu

**Soma ripoti ifuatayo hapo kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

**Ripoti ya Ziara ya Kielimu Iliyofanywa na Wanachuo wa Mwaka wa 3 Chuo cha Ualimu Busara katika Majumba ya Makumbusho mnamo Tarehe 10/7/2019 hadi 12/7/2019.**

Katika mchakato wa ukufunzi na ujifunzaji, wakufunzi na wanafunzi huhitaji kufanya ziara za kielimu ili kunoa ujuzi wao. Ndiyo maana kuanzia tarehe 10/7/2019 hadi 12/7/2019 wanachuo wa mwaka wa tatu katika Chuo cha Ualimu Busara walifanya ziara ya kielimu katika majumba ya makumbusho yanayopatikana hapa nchini Rwanda. Lengo kuu la ziara hizi lilikuwa kuelewa zaidi historia na utamaduni wa Wanyarwanda. Ziara hizi ziliongozwa na Mkufunzi Steven Kabera.

**Majumba ya Makumbusho Yaliyotembelewa**

i) Jumba la Makumbusho la Rukali-Nyanza
ii) Jumba la Makumbusho la Huye
iii) Jumbala Makumbusho la Nyarugenge

Tarehe ya 10/7/2019 ndipo walianza ziara zao. Wanachuo na mkufunzi wao walianzia katika wilaya ya Nyanza, wakatembelea Jumba la Makumbusho linaloonyesha maisha ya wafalme. Katika jumba hilo, wanachuo walielezwa mengi kuhusu maisha ya wafalme walioongoza Rwanda. Hapo walionyeshwa vifaa tofauti vilivyokuwa vikitumiwa na wafalme hawa na Wanyarwanda kwa ujumla kabla ya ukoloni. Zaidi ya hayo, jumba hili la Rukali huhifadhi ng'ombe wa kupendeza macho "Inyambo" kwa Kinyarwanda na nyumba za kifalme.

Walipopewa fursa ya kuuliza, wanachuo waliuliza maswali mbalimbali yaliyopata majibu kutoka kwa wahudumu wa Jumba hili.

Kwenye tarehe ya 11/7/2019 ziara ya wanachuo ilielekezwa katika Wilaya ya Huye, katika jumba la makumbusho linalohusu maisha ya Wanyarwanda kwa ujumla. Katika jumba hili, wanachuo walitembezwa katika vyumba mbalimbali

vinavyounda jumba hili na kuonyeshwa vifaa vilivyokuwa vikitumiwa na Wanyarwanda. Mahali hapa, wanachuo walipewa maelezo ya kina kuhusu historia ya Wanyarwanda toka enzi za wafalme hadi utawala wa jamhuri.

Kwenye tarehe ya 12/7/2019 usukani ulielekezwa jijini Kigali katika Jumba la Makumbusho la Nyarugenge. Katika jumba hili, wanachuo walielezwa namma ambavyo wakoloni walikuwa wakiongoza nchi ya Rwanda. Zaidi ya hayo, wanachuo hawa walielezwa kuwa jumba hili lilikuwa ofisi ya kiongozi wa kwanza wa kikoloni Dkt. Richard Kandt. Pia, waliambiwa kuwa huyu ndiye aliyefanya Kigali kuwa mji mkuu wa Rwanda. Vilevile, wanachuo walionyeshwa nyoka mbalimbali na mamba wanaohifadhiwa katika jumba hili.

Ziara hizi zilipomalizika, wanachuo walikaa pamoja katika ukumbi wa chuo na kujadiliana kuhusu yale yote waliyoyaona. Kwa pamoja, waliamua kuwa wametosheka kabisa. Lakini walitoa mapendekezo yafuatayo:

- Wanaomba chuo kuandaa ziara za kielimu nyingine katika majumba mengine yaliyobakia kama Jumba la Makumbusho la Karongi (linahifadhi mambo ya kimazingira), Jumba la makumbusho la mapambano ya kujikomboa la Kimihurura, Handaki ya Mulindi wa Mashujaa (ku Mulindi w'Intwari), Jumba la Makumbusho la Mambo ya kisanaa la Kanombe, na kadhalika.
- Wanaiomba Serikali ya Rwanda, kupitia Bodi ya Maendeleo ya Rwanda (RDB) kutafuta mbinu thabiti za kulinda majumba haya ya makumbusho na kuhifadhi vitu na vifaa vyote vilivyomo humo.
- Wanawashauri Wanyarwanda kutembelea katika majumba haya ili kujua historia na utamaduni wao.

Imetayarishwa na.

Jina:  Steven Kabera

Cheo: Mkufunzi wa Kiswahili

Saini: Stevkabera

Tarehe: 13/7/2019

## KAZI 1

**Jibu Maswali Haya**

1. Ripoti hii inahusu nini?
2. Ziara zilizofanywa zilikuwa na lengo gani?
3. Ziara hizi zilifanyika lini?
4. Taja majina ya majumba yaliyotembelewa
5. Ni pendekezo gani waliloipa Serikali ya Rwanda?

## 10.2. Msamiati kuhusu Ripoti

## KAZI 2

**Tunga sentensi zako kwa kutumia maneno yafuatayo. Kabla ya kutunga, hakikisha umechhunguza matumizi yake katika kifungu cha ripoti ulichokisoma hapo juu:**

1. Ziara
2. Ripoti
3. Ukumbi
4. Kuandaa
5. Kuhifadhi

## KAZI 3

**Husisha maneno kutoka sehemu A kwenda sehemu B**

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| 1. Ziara | a) Watu wanaojifunza elimu au kazi fulani |
| 2. Mchakato | b) Rai au fikira inayotolewa na mtu kwenye mikutano au mijadala ili ijadiliwe au kutolewa uamuzi |
| 3. Pendekezo | c) Mfululizo wa shughuli unaosababisha jambo fulani kufanyika. |
| 4. Handaki | d) Mtu anayetoa mhadhara, mwalimu katika chuo |
| 5. Mhadhiri | e) Mtaro au shimo kubwa au refu linalochimbwa kwa madhumuni ya kujilinda wakati wa vita. |
| 6. Wanachuo | f) tendo la kuenda mahali fulani kwa sababu maalum |

## 10.3. Sarufi: Vipashio vya Tungo za Kiswahili

**KAZI 4**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha utaje aina na sehemu kuu zake.**

1. Kiranja ameandaa mkutano wa wanachuo.
2. Ziara ziliandaliwa na wanachuo walitembea.
3. Mvua iliyonyesha ilisababisha mafuriko.
4. Yeye alikuja tulipokuwa tukicheza.
5. Wao hupendana sana.
   - Sentensi ya 1 na ya 5: sentensi sahili
   - Sentensi ya 2: sentensi ambatano
   - Sentensi ya 3 na ya 4: sentensi changamano
   - Kwa kawaida sentensi huundwa na kiima na kiarifu/kiarifa/prediketa

**Maelezo muhimu kuhusu sehemu za tungo**

**i) Maana ya tungo**

Tungo ni fungu la maneno ambayo yanawakilisha nafsi, kitu kinachotendwa au jambo linalopasha habari kamili. Pengine tungo ni kipashio cha kimuundo kinachotokana na uwekaji pamoja wa vipashio sahili ili kujenga kipashio kikubwa zaidi. **Kipashio** ni kipande cha tungo ambacho huweza kujenga au kujengwa na tungo nyingine.

**ii) Aina za tungo**

Kiswahili kina tungo nyingi sana; nyingine ni fupi sana, nyingine ni ndefu sana. Ziko tungo zilizojengwa kwa neno moja tu, na nyingine kwa maneno mengi.

**Kwa mfano :**

- **Tunasoma.**
- **Masika yanakaribia.**
- **Mwana wao wa pekee aliwasaidia.**

Tungo za Kiswahili ni nyingi, lakini zinaweza kuwekwa katika makundi ya idadi ndogondogo kwa kufuata misingi fulani fulani ya kisarufi. Angalia mfano huu :

a) Msingi wa muundo wa tungo

b) Msingi wa maana za tungo

Kwa msingi wa muundo wa tungo, tungo hugawanyika katika aina kuu tano :

1. Tungo sahili (Mwanafunzi anafagia.)
2. Tungo tegemezi (Aliyefika)
3. Tungo changamano (Mwanafunzi aliyefika anafagia.)
4. Tungo ambatano (Kijana amekuja na ameondoka.)
5. Tungo shurtia (Mvua ingenyesha mapema tungepanda mahindi.)

**Kwa msingi wa wa maana za tungo, tungo hugawanyika pia katika aina nne**

1. Tungo sahili (Mwanafunzi amefika.)
2. Tungo tegemezi (Aliyefika)
3. Tungo nyofu: yenye maana moja tu. (Sipendi kunywa pombe)
4. Tungo tata: yenye maana zaidi ya moja (Sipendi kunywa bia [ tanbihi:bia humaanisha pombe au 'pamoja; kwa kushirikiana na mtu mwingine])

**KAZI 5**

**Taja aina za tungo zifuatazo:**

1. Mwanafunzi anaimba
2. Kijana aliyefika jana ni daktari
3. Mwanafunzi aliyekuja anaimba
4. Kijana amekuja na anaimba

**iii) Sehemu za tungo**

Kwa kawaida tungo ya Kiswahili inaundwa na sehemu mbili kubwa. Sehemu hizo ni **kiima na kiarifu/ kiarifa au prediketa**.

**Kiima** ni sehemu ya tungo inayoonyesha nafsi ya mtenda au mtendwa wa jambo linaloelezwa yaani kuarifiwa. Kiima huandikwa kushoto mwa kitenzi. Kiima ndiyo sehemu ambayo hutoa upatanisho wa kiambishi awali cha kitenzi.

**Kiarifu /kiarifa/prediketa** ni sehemu katika tungo ambayo huzungumza juu ya kiima. Ni kusema sehemu ya sentensi yenye kitenzi na vipashio vyake (shamirisho na chagizo).

**Mifano:**

- **Mwanafunzi huyu** *alichelewa.*

  Kiima Kiarifu

- **Mama** *amekwendashambani.*

  Kiima Kiarifu

- **Mwanafunzi mzuri** *hanakili majibu mtihanini.*

  Kiima Kiarifu

- **Bwana Jonas na mtoto wake** *wanakwenda sokoni.*

  Kiima kiarifu

- **Kamana** *alijenga jumba la kifahari mjini Butare.*

  Kiima kiarifu

**KAZI 6**

**Onyesha sehemu kuu za sentensi zifuatazo:**

1. Mvua ilinyesha jana usiku.
2. Rwanda ilipiga marufuku utumiaji wa mifuko ya plastiki.
3. Mwanafunzi ambaye anapanga kushinda hufuata darasa.
4. Ugonjwa wa Ebola unatisha sana.
5. Watu wanaoishi nchini Rwanda huishi kwa amani.

## 10.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu Kuhusu Ripoti

**KAZI 7**

**Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

### i) Maana ya Ripoti

Ripoti ni maelezo ya  kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea. Ni aina ya kumbukumbu ambazo huandikwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Ripoti inaweza kuwa ya uchunguzi wa utafiti kuhusu jambo fulani, inaweza kuwa ya polisi, daktari au ya tume fulani.

### ii) Namna ya Kuandika Ripoti

Kabla ya kuandika ripoti, lazima kuwe na ushahidi unaohusu suala au jambo linaloandikiwa ripoti hiyo. Kwa hiyo, ni lazima mtunzi afanye uchunguzi kwanza. Pia mtunzi anapaswa kufahamu kiwango cha elimu na uwanja wa mtu anayemwandikia ripoti hiyo. Kwa mfano kama ni polisi, daktari, mwanasheria, mfanyabiashara, n.k. Lugha atakayoitumia mwandishi au mtunzi izingatie muktadha wa matumizi. Lugha itegemee aina ya ripoti.

### i) Sehemu za ripoti

#### a) Kichwa cha ripoti

Kichwa cha ripoti hutambulisha kiini cha ripoti. Yaani ripoti inahusu nini, tarehe ya tukio au jambo linaloandikiwa ripoti na mahali palipotokea jambo hilo.

#### b) Utangulizi wa ripoti

Katika hatua hii mwandishi hueleza kwa muhtasari madhumuni ya ripoti.

#### c) Kiini cha ripoti

Katika sehemu hii mwandishi hueleza mambo aliyoyaona, chanzo chake na madhara au faida yake.

#### d) Hitimisho

Katika kuhitimisha ripoti mwandishi anaonyesha msimamo na mapendekezo yake. Baada ya hitimisho, mwandishi huandika au huonyesha aliyeandika ripoti, cheo chake (nafasi yake hasa katika ripoti hiyo) na tarehe ripoti hiyo ilipoandikiwa. Ikumbukwe kuwa aghalabu ripoti huandaliwa ili kutaka mageuzo fulani ya jambo.

### v) Aina za Ripoti

Ripoti ni za aina nyingi:

- Za kielimu
- Za mikutano
- Kiuchumi
- Kijamii
- Kisiasa
- Kiusalama

### vi) Sifa za Ripoti

Ripoti ni lazima iwe na mpangilio mzuri wenye mada zinazozungumziwa na labda hata mada ndogo ndogo zenye kuzingatia utaratibu wa nambari. Matumizi ya nambari husaidia kuipa ripoti mpangilio mzuri na wenye kueleweka kwa urahisi. Ripoti hazipaswi kuwa ndefu sana na zinapaswa kuwasilisha mambo muhimu kwa ufupi. Mwandishi wa ripoti hutumia mbinu za kufupisha lakini anahakikisha kuwa kila kitu kimezungumziwa. Ripoti hutumia sentensi fupi fupi zinazowasilisha mambo muhimu kwa uwazi. Ni vyema lugha inayotumiwa katika ripoti iteuliwe kwa uangalifu na isiwe na hisia au sifa ya kuathiri vibaya wanaoisoma.

**Jibu maswali yafuatayo :**

1. Ripoti ni nini?
2. Taja angalau mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandika ripoti.
3. Taja sehemu za ripoti

## 10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**KAZI 8**

**Sikiliza kipindi kwenye redio kinachohusiana na usawa wa jinsia, ukifanyie ripoti kisha uwasilishe darasani.**

## 10.6. Kuandika

**KAZI 9**

**Tunga ripoti kuhusu mojawapo kati ya mada zifuatazo:**

1. Ziara moja ya kimasomo uliyoifanya kuhusiana na uhifadhi wa mazingira.
2. Kiwango cha umoja na maridhiano chuoni kwako.

# SOMO LA 11: MAANDALIZI YA RIPOTI



## KAZI 1

**Tazama mchoro hapo juu kisha jibu maswali yafuatayo:**

- Wahusika unaowaona kwenye mchoro huu wanafanya nini?
- Unafikiri wahusika hao wako wapi ?
- Kwa nini unafikiri au haufikiri kuwa kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo juu?

## 11.1. Kusoma na Ufahamu: Ripoti ya Maandalizi ya Mafunzo ya Elimu Jumuishi

**Soma ripoti ifuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini:**

**Ripoti ya Maandalizi ya Mafunzo ya Elimu Jumuishi Yaliyofanyika tarehe 2/11-15/11/2019 katika chuo cha TUENDELEZE ELIMU.**

Mnamo tarehe 2/11/2019 hadi 15/11/2019 yalifanyika mafunzo kuhusu elimu jumuishi. Mafunzo haya ili yaweze kufanikiwa, yalihitaji ufasaha wenye maandalizi ya kutosha yaliyochukua wiki mbili. Ilifanyika hivi ili wakufunzi waweze kufanikisha kuandaa mada husika . Kufanikiwa kwa maandalizi hayo ni kutokana na juhudi za wakufunzi wenyewe kuwa na moyo wa kujituma, na ushirikiano mkubwa ulioonyeshwa na jopo la uongozi wa chuo cha Ualimu"TUENDELEZE ELIMU" kilichopo wilayani ya Matumaini.

Wakufunzi tulifurahia ushirikiano kutoka chuo "TUENDELEZE ELIMU" kwani kila kitu tulichohitaji ili kufanikisha mafunzo yetu kilitolewa na uongozi wa chuo bila tatizo lolote. Ushirikiano wao ulikuwa katika vifaa vya maandalizi, chakula na malazi, posho kwa ajili ya kujikimu na usafiri. Hayo yote yalikuwa changamoto kwa wahadhiri na washiriki wa mafunzo.

**Utoaji wa mafunzo**

Mafunzo yalifanyika kwa muda wa siku tano saa nane zilitumika kwenye mafunzo na saa mbili zilitumiwa kwenye majadiliano, kwa ajili ya chakula na mapumziko kwa wakufunzi, walengwa na uongozi.

Zifuatazo ni mada mbalimbali zilizotolewa kwenye mafunzo haya:

**1. Njia Shirikishi katika Ujifunzaji**

Njia shirikishi katika kujifunza ilipewa kipaumbele katika muda wote wa mafunzo. Njia hii ilihamasisha wanachuo kushiriki zaidi katika mazoezi na kwa kiwango fulani iliwasaidia pia kushiriki katika kujifunza. Njia hii ilileta msukumo katika kutafuta majibu na kuunganisha pamoja taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, badala ya kumtegemea tu mkufunzi kuongoza vipindi vyote vya masomo. Kwa sababu elimujumuishi si dhana rahisi ambayo inaweza kutumika kwa namna moja, katika sehemu zote, wanachuo katika mafunzo ya elimujumuishi wanapaswa kupewa mwongozo wa kutafuta na kupata habari sahihi na kutafuta njia bora ya kusonga mbele kwa kuanzia sehemu walizopo. Zaidi ya mazoezi yaliyokuwa yamepangwa kwenye ratiba, ushirikishwaji katika kujifunza ulifanywa pia katika majadiliano ya nje wakati wa mapumziko, na katika maktaba ndogo ambamo washiriki huweza kupata nafasi ya kujisomea katika muda wa ziada.

## 2. Umuhimu na sifa za mafunzo haya

Mafunzo yalilenga kuendeleza dhana kwamba hupaswi kujifanya mjuaji zaidi wa elimu jumuishi kwa kufanya peke yako matendo ambayo unadhani yanaifanya elimu iwe jumuishi zaidi. Kila mmoja ana mawazo na uzoefu wake ambapo yote ni muhimu katika kuendeleza mfumo wa elimu jumuishi na jamii nzima.

## 3. Stadi za mawasiliano

Ingawa kulitumiwa uwasilishaji wa mada au kazi za vikundi, tulihitaji stadi maalum za mawasiliano. Tunapaswa kuwaelezea watu kuhusu sisi wenyewe, kazi zetu, uzoefu wetu au mawazo yetu, na mara kwa mara tunahitaji uwezo wa kufanya hivi kwa muda mfupi. Ni kawaida kwa wanachuo kukosa ujuzi na/au kutojiamini katika mawasiliano. Hii inaweza kuathiri maendeleo na matokeo ya mafunzo hasa ukizingatia kwamba wanachuo wanatarajiwa kuchangia hoja na uzoefu na siyo kuwa wasikilizaji.

## 4) Hitimisho

Katika kuhitimisha ripoti waandaaji wa mafunzo walitoa shukrani zao kwa jopo zima la chuo na uongozi na watendaji wake kwa ushirikiano wao mzuri waliouonyesha kwa mijadala yao mizuri iliyowawezesha kujua tatizo lipo wapi na pia kuibua uzoefu uliopo na hatimaye kwa pamoja kuweza kutambua udhaifu upo wapi. Hatua hii itasaidia kutoa uzoefu wa namna ya kurekebisha ambapo hapakwendeka vizuri.

### KAZI 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Elimu jumuishi ni nini?
2. Ni njia zipi zitumikazo katika kufanikisha elimu shirikishi kwa wanachuo?
3. Ni mambo gani hutolewa zaidi ya masomo yaliyopangwa kwenye ratiba?
4. Eleza tabia moja ya mafunzo jumuishi
5. Ni mwenendo upi wanachuo wanatakiwa waonyeshe katika mafunzo ya elimu jumuishi?

## 11.2. Msamiati kuhusu Mfano wa Ripoti ya Mafunzo Jumuishi

### KAZI 3

Tunga sentensi zako kwa kutumia maneno yafuatayo. Chunguza matumizi yake katika kifungu cha ripoti ulichosoma hapo juu.

- Mafunzo
- Chuo
- Ripoti
- Umuhimu
- Elimu

### KAZI 4

**Husisha maneno kutoka sehemu A kwenda sehemu B**

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| 1. Mafunzo | a) mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni,vyuoni, maishani; taaluma |
| 2. Chuo | b) uhodari au ufundi mkubwa wa kutenda jambo fulani |
| 3. Ripoti | c) uzuri au ubaya wa mtu au kitu |
| 4. Stadi | d) shule inayotoa mafunzo maalumu ya kazi fulani |
| 5. Umuhimu | e) Upashanaji habari kwa njia mbalimbali simu,barua au telegramu |
| 6. Hitimisho | f) Mpango unaotolewa kwa mdomo au maandishi kuwaelekeza watu wengine kutekeleza kazi fulani |
| 7. Mawasiliano | g) Hali inayofanya kitu au jambo fulani lihitajike katika jamii, |
| 8. Mwongozo | h) jambo linalosemwa na kuandikwa mwisho |
| 9. Sifa | i) Maelezo juu ya mtu, kitu, tukio au jambo fulani, taarifa, habari |
| 10. Elimu | j) Mambo anayofundishwa mtu kwa muda fulani, masomo |

## 11.3. Sarufi: Vipashio vya tungo

**KAZI 5**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha utaje sehemu zake na vipashio vya kila sehemu.**

1. Mwalimu anakwenda shuleni.
2. **Mwanafunzi aliyekuja aliimba.**
   - Katika sentensi ya 1: **Mwalimu** ni kiima (nomino) na **anakwenda shuleni** ni karifu ( kitenzi+ nomino).
   - Katika sentensi ya 2: **Mwanafunzi aliyekuja** ni kiima (nomino+ kishazi) na **aliimba** ni kiarifu (kitenzi).

**Maelezo muhimu kuhusu vipashio vya tungo**

**KAZI 6**

**Soma maelezo muhimu haya kisha ujadiliane na wenzako.**

**Kipashio**

**Kipashio** ni neno moja au kifungu cha maneno chenye kazi maalum katika tungo. Vipashio hivi ndivyo ambavyo huungana pamoja na kujenga sehemu kuu za tungo yaani kiima na kiarifu.

- **Vipashio vya kiima**

Kiima kinaweza kuundwa na vipashio vya aina mbili: neno moja au fungu la maneno.

**a) Neno moja katika kiima**

i) Nomino (N): **Kazi** ni uhai.

ii) Kiwakilishi (W): **Yeye** hapendi kushiriki ngono.

- **Huyu** ni kiranja wetu.

iii) Kitenzi-jina: **Kuimba** kunapendeza.

iv) Kishazi: **Atakayevuta bangi** ataadhibiwa.

**b) Fungu la maneno katika kiima**

i) Nomimo mbili (N+N): **Baba na Mama** wanafanya kazi za Umuganda.

ii) **Bwana Kagabo** ni mcheshi.

iii) Nomino na kivumishi (N+V): **Mwanafunzi hodari** hana wasiwasi.

iv) Kiwakilishi na kivumishi (W+V): **Huyu hodari** hana wasiwasi.

v) Nomino na kishazi: **Mwanafunzi atakayevuta bangi** ataadhibiwa.

- **Vipashio vya kiarifu**

Kiarifu kinaweza kuundwa na vipashio vya aina mbili: neno moja na fungu la maneno

**a) Neno moja katika kiarifu**

i) Kitenzi (T): Mama **analima**.

**b) Fungu la maneno katika kiarifu**

i) Kitenzi na Kitenzi (TS+T): Yeye **anapenda kucheza**.

ii) Kitenzi na shamirisho (T+SH (N)): Yeye **anacheza mpira**.

(T+SH(W)): yeye **anapenda yule**.

iii) Kitenzi na chagizo (T+CH (E)): Yeye **anacheza vizuri**.

(T+CH(HU)): Yeye **alienda kwa mganga**.

iv) Kitenzi na kishazi: Yeye **anacheza tunapolala.**

## KAZI 7

**Onyesha sehemu kuu na vipashio vyake katika sentensi zifuatazo:**

1. Wanafunzi wale wanapenda kusafisha nguo zao.
2. Mwananchi mwema analinda mazingira.
3. Mtu aliyepata UKIMWI anaonywa kutopoteza matumaini.
4. Mwizi alivamia nyumba yetu jana.
5. Jua kali linasababisha ukame nchini.

## 11.4. Matumizi ya Lugha: Maandalizi ya Ripoti

**KAZI 8**

**Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha ufanye ujibu maswali ya hapo chini.**

- **Taratibu za kufuatilia wakati wa kuandaa ripoti**

Unapoandika ripoti unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Hakikisha kuwa umeelewa shughuli inayohusika
- Hakikisha unajua urefu unaohitajika na masuala unayopaswa kuyagusia
- Kusanya maelezo yote unayohitaji kuhusiana na ripoti hiyo.
- Yapange maelezo yako vizuri. Zipitie hoja zako ili uondoe mawazo ambayo yanaweza kuwa yamerudufishwa au yamerudiwa.
- Yaangalie mawazo yako ili kubainisha ni yapi ambayo yanapaswa kutangulia na yanafuatwa na yapi.
- Unapoandika ripoti yako hakikisha kuwa unaitumia lugha yako. Usiridhike tu na maneno unayoyapata wakati wa uchunguzi wako. Kuandika ripoti kwa lugha na maneno yako huonyesha kuwa umeielewa.
- Unaweza kuuboresha uwezo wako wa kuandika ripoti kwa kujitahidi kuyaelewa maelezo yanayohusika na kujitahidi kuyaeleza kivyako.
- Baada ya kuandika nakala ya kwanza ya ripoti unaweza kuiboresha kwa kupunguza mambo ambayo siyo muhimu katika ripoti hiyo.
- Lugha inayotumiwa katika uandishi wa ripoti lazima izingatie wasomaji wa ripoti inayohusika. Kwa mfano, ikiwa wasomaji ni wanafunzi wa shule lugha yake haipaswi kuwa na ugumu au utata wa kisayansi.

- **Mifano ya mazingira ya kutolea ripoti**
- Kila jambo mtu analofanya kila mara nyingi huomba kutolewa ripoti. Kwa mifano:

- Mwanafunzi anaweza kutumwa kuwakilisha chuo chake katika kongamano la vilabu mbalimbali akatoa ripoti baadaye.
- Mwanfunzi anaweza kuenda kujizoeza kufundisha katika chuo fulani, anapomaliza akaombwa kutoa kuripoti kwa chuo chake.
- Mtangazaji wa habari anaweza kufanya utafiti kuhusu jambo fulani kisha akatoa ripoti kwa yale aliyoyaona.

- Mtafiti fulani anaweza kutumwa kuchunguza mambo fulani (ukiukaji wa haki za kibinadamu, kuenea kwa ugonjwa fulani, kiwango cha hongo, n.k) kisha akatoa ripoti.
- Maafisa wa kiserikali wanaweza kufanya utafiti kuhusu maisha ya jamii (uchumi, kilimo, ufugaji, …) wakatoa ripoti kwa serikali.
  - Mazingira ya kutolea ripoti ni mengi mno, ripoti zinaweza kutolewa katika mikutano, darasani, kwenye televisheni, redioni, katika hafla, katika vikao vya dharura, katika makongamano na kadhalika.

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Uboreshaji wa ripoti hufanyika namna gani?
2. Kwa sababu gani mwandishi wa ripoti analazimishwa kuzingatia vizuri lugha anayoitumia?
3. Taja mazingira matatu ya kutolea ripoti.

## 11.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 9**

**Tunga ripoti kuhusu mada za hapo chini kisha uwasilishe hadharani.**

1. Ripoti kuhusu mchango wako kama mwanachuo  katika kuendeleza umoja na maridhiano.
2. Ripoti kuhusu klabu za ukimwi  chuo zipatikanazo katika maeneo ya shule jirani.

## 11.6. Kuandika

**KAZI 10**

**Fanya utafiti kuhusu elimu shirikishi katika chuo chako kisha uandike ripoti.**

## Tathmini ya mada

1. Ripoti ni nini?
2. Taja angalau mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandika ripoti.
3. Taja sehemu za ripoti
4. Uboreshaji wa ripori hufanyika namna gani?
5. Kwa sababu gani mwandishi wa ripoti anapaswa kuzingatia vizuri lugha anayotumia?
6. Onyesha vipashio katika sentensi zifuatazo
   i) Watu wanapaswa kuishi kwa usafi.
   ii) Yeye alitunukiwa zawadi aliposhinda.
   iii) Wanyarwanda wengi wanalala katika nyumba safi.
   iv) Mtu anayetegemea cha nduguye atakufa maskini.
   v) Mwalimu huyu anafundisha vizuri.

# MADA YA 6

# UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

## Uwezo mahususi

Kuelezea aina za fasihi simulizi na kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi simulizi

**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya uhakiki,
- Kubainisha taratibu au mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi simulizi,
- Kuonyesha umuhimu wa kuhakiki kazi za fasihi,
- Kujadili maana ya uhakiki na mwongozo wake,
- Kuhakiki hadithi za masimulizi mbalimbali,
- Kutoa mapendekezo juu ya kazi za fasihi zilizohakikiwa,
- Kukuza falsafa tofauti zinazojidhihirisha kutoka ujumbe wa kazi za fasihi simulizi,
- Kuainisha aina za maneno katika Kiswahili.

### Kidokezo



**Tazama mchoro wa hapo juu kisha ujibu maswali yafuatayo:**

- Unaona nini kwenye mchoro huo?
- Wahusika wanaoonekana kwenye mchoro wanafanya nini?
- Wahusika hawa wako wapi?

# SOMO LA 12: MAANA YA UHAKIKI

## 12.1. Kusoma na Ufahamu: Siku Njema Huonekana Asubuhi

**Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini.**

Ilikuwa Jumatatu asubuhi wakati mwalimu wetu wa Kiswahili Bibi Amina alipotuchekesha sana. Mwalimu huyu kwa kawaida yake alikuwa mcheshi na mwenye kupenda utani. Ilikuwa ni ajabu mno kumwona amekunja uso. Wanafunzi wote walikuwa wakimpenda na hata wagonjwa walikuwa wakijikaza kiume ili wawahi somo lake. Alikuwa mnene kiasi, macho mazuri kama gololi yaliyokuwa yakicheza katika vidimbwi vya machozi. Alipokuwa akicheka, vishimo vidogovidogo vilikuwa vikionekana kwenye mashavu yake. Sauti yake ilikuwa ikituvutia sana. Alikuwa akifundisha na wanafunzi sote tukatoka tukisema kuwa tumetosheka.

Asubuhi hiyo, tulipofika shuleni tuliulizana habari mbalimbali. Kuna wale waliokuwa na habari za michezo na wengine walikuwa na habari zinazohusu maisha ya nchi yetu: uchumi, elimu, siasa, ufugaji, kilimo na kadhalika. Habari hizo zote tulikuwa tumezipata kutoka kwenye redio na nyingine kutoka kwenye runinga. Kwa kuwa nami nilikuwa sogora kwa kutia chumvi katika mazungumzo, kila siku wanafunzi walikuwa wakinizunguka kama nyuki wazengeavyo maua.

Kengele ya kwanza ilipolia, sote tulikusanyika karibu na mlingoti wenye bendera ya taifa na kuanza kuimba wimbo wa taifa. Tulipomaliza, Joni, mwalimu wa somo la ujasiriamali, alipanda jukwaani na kuanza kutuhutubia kuhusu mada ya "Ndi Umunyarwanda." Siku hiyo yeye alitilia mkazo kwenye umoja na maridhiano kati ya Wanyarwanda, uzalendo na mshikamano kama njia bora za kuendeleza nchi yetu. Alipomaliza, tuliingia madarasani na kuwasubiri walimu wetu.

Kengele ya pili ilipolia mwalimu wetu wa Kiswahili alijtokeza na kutuamkia kama kawaida yake. Alikuwa na mkoba begani na vitabu pamoja na boksi la chaki mikononi. Sisi sote tulikuwa na hamu ya kusikia mchapo aliokuwa ametuletea asubuhi ile. Bila ya kusema neno lolote aliweka vifaa vyake mezani akaangaza

macho kama aliyekuwa akishuku jambo baya fulani darasani. Sisi sote tulitulia tuli kama maji mtungini. Hayawi hayawi huwa. Alipomaliza ukaguzi wake alituuliza majina ya wale ambao hawakuhudhuria shule lakini sote tulikuwa hapo. Alitabasamu na kuanza somo lake.

Kwanza alituuliza maswali kuhusu somo lililopita. Somo hilo lilikuwa vipengele vya fasihi simulizi. Tuliposonga mbele alituomba kumwonyesha kazi ya nyumbani aliyotupatia. Kazi hiyo ilikuwa uchambuzi wa hadithi. Sote tulikuwa tumejaribu kwa uwezo wetu. Alituuliza mbinu tulizotumia katika uchambuzi wetu, kila mtu akataja zake. Alitukagua kitambo kidogo, akatupongeza na kusema kuwa "Kweli siku njema huonekana asubuhi." Mara hii alichukua chaki na kuandika neno "**UHAKIKI**" ubaoni. Nasi tukaanza kunong'onezana kwa kuwa ilikuwa mara ya kwanza kuona neno hilo. Tulishangaa sana kwa kuona kuwa hakuandika jaribio kama desturi yake ya kutuuliza kila alipokuwa akiingia darasani. Alipotangaza kuwa neno hilo lilikuwa somo la siku ile sote tulitega masikio.

Pili, alitugawa katika makundi. Kila kundi lilikuwa limeundwa na wavulana na wasichana, na wanafunzi wenye matatizo maalum ya kielimu. Kila kundi lilipewa kitabu. Kabla hatujafungua vitabu, alituomba kukagua vema kama kila kundi lilipewa vitabu vya Kiswahili. Alituonya hivi huku akitwambia kuwa kulikuwa na mtu mmoja aliyeingia mgahawani bila kuuliza habari wala kusoma, akatia pilipili hoho nyingi kwenye chakula akidhani kwamba ni supu. Alipokula chakula hicho, aliwashwa na machozi yalimlemgalenga. Katika kujaribu kupoza koo lake, akashika na kunywa sabuni ya kunawia mikono akifikiri kwamba ni juisi. Sisi sote tulishika mbavu. Alituagiza kufungua vitabu na kuzungumzia kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi simulizi. Tulipomaliza kuzungumza, kila kundi liliwasilisha.

Tuliona kwamba uhakiki ni kazi ya kutathmini, kufasili na kuainisha kazi za fasihi. Ni kazi ya kusoma maandishi au kusikiliza mambo fulani kwa kuyachambua na kuyafafanua ili kupata ukweli wa mambo hayo.

Zaidi ya hayo, tulisoma kuwa kwa kuhakiki maandishi au masimulizi, tunachunguza na kufafanua vipengele vya fani na maudhui. Katika fani kama sura ya nje ya maandishi au masimulizi, tunachunguza wahusika, muundo, mtindo na mengineyo. Kimaudhui, tunachunguza dhamira, ujumbe, migogoro, itikadi, falsafa na hata mtazamo. Wakati huu, mambo yaliyokuwa yakitushinda, mwalimu alikuwa akitusaidia ili tuyaelewe zaidi.

Isitoshe, baada ya kuona maana ya uhakiki, mwalimu alituomba kueleza umuhimu wa uhakiki tukagundua kwamba uhakiki una umuhimu wa kumwezesha mhakiki kuchambua na kuelewa kazi ya fasihi au sanaa kwa ujumla, kuwezesha kulinganisha kazi tofauti na mengine mengi.

Lakini katika uchambuzi wetu, tuligundua kuwa uhakiki una matatizo fulani kwa sababu ni sayansi ngumu inayoomba bidii, ukakamavu wa mhakiki, uwezo wake na mienendo ya jamii. Hili linatulazimisha tufanye mazoezi mengi ili tuweze kupevuka katika kazi hii. Tena tuliona kuwa, wakati mwingine, wahakiki hawakubaliani kwa kuwa kila mmoja ana namna yake ya kuona na kuelewa mambo.

Somo lilipokaribia kutia nanga, sote tulikuwa tumeelewa kwamba uhakiki lilikuwa si somo geni kwa kuwa kila siku tunajaribu kuchambua yale tunayosoma au tunayoambiwa. Kutokana na weredi wa haraka tuliokuwa nao ndipo nilipokumbuka kuwa "Siku njema huonekana asubuhi." Kabla ya kutuaga mwalimu alitupa kazi ya nyumbani ya kuhakiki hadithi.

**KAZI 1**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Taja majina ya walimu wanaoelezwa katika kifungu hiki?
2. Mwalimu wa Kiswahili alikuwa nani?
3. Msimuliaji ni nani katika kifungu hiki?
4. Unafikiri ni kwa sababu gani mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa siku njema huoneka asubuhi?
5. Je, kichwa cha kifungu kinahusiana na yaliyomo?

## 12.2. Msamiati kuhusu Kifungu

**KAZI 2**

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

- Amekunja uso
- Walijikaza kiume
- Mshikamano
- Kutathmini
- Kufasili

**KAZI 3**

**Tunga sentensi zenye maneno yafuatayo:**

- Mkoba
- Vidimbwi
- Mashavu
- Uzalendo
- Juisi

## 12.3. Sarufi: Aina za Maneno ya Kiswahili

**KAZI 4**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha utaje aina za maneno yaliyopigiwa mstari.**

- **Kamikazi** **ni** mwanafunzi wa chuo cha **ualimu**.
- Rwanda **itajengwa** na wananchi **wake**.
- **Wao** husaidiana katika kujenga **familia** yao.
    - **Kamikazi**, **ualimu**, familia ni nomino/majina
    - **Ni**, **itajengwa** ni vitenzi
    - **Cha**, **wake** ni vivumishi
    - **Wao** ni kiwakilishi

### Maelezo Muhimu Kuhusu Aina za Maneno

**KAZI 5**

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali yatakayotolewa**

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina nane za maneno. Aina hizo ni kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kihusishi, kielezi, kiunganishi na kihisishi. Katika somo letu tutagusia aina nne: nomino, kivumushi, kiwakilishi na kitenzi.

- **Nomino/ jina**

**a) Maana ya nomino**

Nomino au jina ni neno linaloita kitu chenye uhai au kisicho na uhai kwa kukitofautisha na vingine.

**b) Aina za nonino**

- **Nomino za pekee**: Butare, Rusizi, Kamana, Ibilisi, Mukungwa, Akanyaru,
- **Nomino za kawaida:** barabara, gari, kuku, kiongozi, nchi, …
- **Nomino za dhana au za dhahania:** maridhiano, uzalendo, utoto, utu, upendo, …
- **Nomino za jamii/ za makundi**: jamii, jamaa, baraza, genge, kikosi, …
- **Nomino za wingi:** mawese, maji, mafuta, mamlaka, madaraka, …
- **Nomino za kitenzi-jina:** kuishi kwa amani kunapendeza. **Kuimba** ni kuzuri. **Kufurahi** kwako kunatutuliza. (kuishi, kuimba na kufurahi ni vitenzi-jina katika sentensi hizi)

**KAZI 6**

**Weka majina yafuatayo katika wingi:**

| **Umoja** | **wingi** |
|---|---|
| Mkristo | |
| Kabati | |
| Waya | |
| Uso | |
| Umoja | |

- **Vivumishi**

**a) Maana ya Kivumishi**

Vivumishi au visifa ni maneno yanayotuelezea zaidi kuhusu nomino. Aghalabu vivumishi hutanguliwa na nomino.

**b) Aina za vivumishi**

- **Vivumishi vya sifa**

**Mifano:**

- Mke **mrefu** yule ni **mtulivu**.
- Tunapaswa kujenga jamii **nzuri**.

- Sauti **nzuri** humtoa nyoka **mkali** pangoni.

- **Vivumishi vimilikishi**

Vivumishi hivi hutumika kuonyesha umiliki wa nomino. Mizizi ya vivumishi hivi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali. Mizizi hiyo ni : -angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao.

**Mifano :**

- Nyumba **yangu** haina mlango.
- Familia **yake** inaishi vizuri.

- **Vivumishi vya idadi**

Hutueleza zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi.

a) Idadi kamili - hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino.

**Mifano:**

- Mmomonyoko wa ardhi ulibomoa nyumba **kumi** katika vijiji **viwili**.
- Ili kupunguza uhasama unaotokana na ukewenza mume **mmoja** analazimishwa kuoa mke **mmoja**.

b) Idadi Isiyodhihirika - huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili.

**Mifano:** Chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani.

**Mifano:**

- Watoto **kadhaa** waligeuka mayatima wakati wa mauaji ya kimbari dhidi ya Watusi yaliyotokea mnamo mwaka wa 1994.
- Mvua **nyingi** ilinyesha na kusababisha mafuriko.

- **Vivumishi viulizi**

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza swali.

-ngapi?, -pi? wapi?, gani?

**Mifano:**

- Mtu mzima ana meno **mangapi**?
- Ni mbuga **gani** inayohifadhi sokwe nchini Rwanda?

- **Vivumishi viashiria / vionyeshi**

Vivumishi viashiria hutumika kuonyesha au kuashiria nomino kulingana na mahali.

**Karibu:** hapa, huyu, hiki, hili, huku, haya, ule, wale, pale.

**Mbali kidogo:** hapo, huyo, hiyo, hicho.

**Mbali zaidi**: pale, lile, kile.

**Mifano:**

- Safisha mahali **hapa**.
- Mwanafunzi **yule** ni mchezaji kabumbu.

- **Vivumishi visisitizi**

Husisitiza nomino fulani kwa kurudia rudia kivumishi kiashiria

**Mifano:**

- Anaishi pahali **papa hapa**.
- Mtu **yuyu huyu** anatuongoza vizuri.

- **Vivumishi virejeshi**

Hivi ni vivumishi ambavyo hurejelea nomino. Vivumishi hivi vinaweza kuwa vivumishi vya **O-/-ye** rejeshi au vivumishi viashiria vinapotumika kurejelea nomino.

**Mifano:**

- Mwanafunzi **ambaye** ataenda nje ya shule bila ruhusa ataadhibiwa.
- Wanyama **ambao** wametoroka mbuga hawapaswi kuuawa.

- **Vivumishi vya A-unganifu**

Vivumishi hivi hutuelezea zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha kitu kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha kiambishi cha nafsi/ngeli pamoja na kiambishi -a cha a-unganifu, kisha nomino.

**Mfano**: ch**a**, l**a**, kw**a, za, ya.**

- Dawa ya moto si moto.

## KAZI 7

**Pigia mstari vivumishi katika sentensi zifuatazo:**

a) Jua kali hili husababishwa na uharibifu wa mazingira yetu.
b) Maneno matamu yalimtoa nyoka yule pangoni mle.
c) Kofia hiyo imekufanya kuwa maridadi.
d) Rwanda itajengwa na sisi wenyewe.
e) Ni walimu wepi watakaofundisha somo la ujasiriamali?

- **Viwakilishi**

**a) Maana ya viwakilishi**

Viwakilishi vya nomino ni maneno yanayotumika badala ya nomino. Kiwakilishi hakiwezi kuambatanishwa na nomino inayorejelewa.

**b) Aina za viwakilishi**

- **Viwakilishi vya nafsi**

- **Viwakilishi nafsi huru:** Mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao.
- **Viwakilishi nafsi viambata :** Ni-, u-, a-, tu-, m-, wa-, mi-, li-, ya-, ki-, vi-, i-, zi-, ku-, pa-

- **Viwakilishi viashiria**

Viwakilishi viashiria (vionyeshi) hutumika badala ya nomino kwa kuonyesha nomino inayorejelewa bila kuitaja.

- **Hiki** ni chanzo cha maradhi.
- **Hao** wanataka maridhiano.

- **Viwakilishi visisitizi**

Hutumika kwa niaba ya nomino kwa kutumia kiashiria chake mara mbili mfululizo.

Kwa mfano: yuyu huyu, wawa hawa, kiki hiki, papo hapo, mumu humu, zizi hizi,

- Kiki hiki ndicho kinachonifurahisha,

- Yuyu huyu alitueleza matumizi ya viwakilishi visisitizi

- **Viwakilishi vya sifa**

Husimama badala ya nomino kwa kurejelea sifa yake.

**Kwa mfano:** -chungu, -eupe, -dogo, -zuri, -tamu, -embamba, -rembo, -gumu, -kali, ekundu.

- **Viwakilishi vya idadi**

Hutumika kusimama badala ya nomino kwa kurejelea idadi yake.

a) Idadi Kamili - hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino

- **Wawili** hugeuka **mmoja**.
- Alizaa **watatu** tu.

b) Idadi isiyodhihirika - huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili.

**Mifano:**

- Tutasikiliza maoni ya **wengi** kabla ya kuanzisha mradi huu.
- **Vichache** viliandikwa kuhusu maradhi ya UKIMWI.

- **Viwakilishi viulizi**

Viwakilishi viulizi hutumika kwa niaba ya nomino katika kuulizia swali.

Baadhi ya viwakilishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli.

**Mifano:**

- Unaenda **wapi**?
- Ulinunua **mangapi**?

- **Viwakilishi vimilikishi**

Viwakilishi hivi hurejelea nomino kwa kutumia vimilikishi.

- **Kwao** hakuna maji safi.
- **Yao** yameharibika tena kutokana na mvua kali.

- **Viwakilishi virejeshi**

Hutumia O-rejeshi kurejelea na kusimamia nomino.

**Kwa mfano**: ambaye, ambao, ambalo, ambacho, huyo, yule.

- **Ambao** walizaliwa mwaka huu watachanjwa.
- **Ambacho** kinahitajika kitatafutwa.

- **Viwakilishi vya A-unganifu**

Huwakilisha nomino kwa kutaja kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha **kiambishi** cha nafsi/ngeli pamoja na kiambishi -a cha a-unganifu.

**Kwa mfano**: ch**a**, l**a**, kw**a, za, ya**

- **Cha** mlevi huliwa na mgema.
- **La** kuvunja halina rubani.

**KAZI 8**

**Taja aina za viwakilishi vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo:**

- Wao hawajafika kwangu.
- Umwambiye yule mrefu aje hapa.
- La kuvunda halina ubani.
- Wengi walipanda miti kupambana na ukame.
- Mpiga ngumi ukuta hujiumiza mwenyewe.

- **Kitenzi**

**a) Maana ya kitenzi**

Kitenzi ni neno linaloeleza jambo linalotendwa au kufanywa na nomino au kiwakilishi chake.

**b) Aina za vitenzi**

- **Kitenzi halisi:** ni kitenzi kimoja kinachotumiwa katika sentensi.

**Mifano:**

- Wanafunzi **walipanda** miti michache.
- Rais **atafika** kesho.

- **Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi:** Wakati vitenzi viwili hutumika pamoja kueleza kitendo kimoja, kitenzi cha kwanza huitwa kisaidizi na cha pili ndicho kitenzi kikuu.

**Mifano:**

- Yeye alikuwa **akisoma**.
- Wao wanahitaji **kuishi** vizuri.

- **Vitenzi vishirikishi**: Vitenzi vishirikishi vina dhana ya kitenzi **kuwa** au **kuwa na.**

Vitenzi vishirikishi huwa vya aina mbili kuu:

- **Vitenzi vishirikishi vikamilifu:** hivi huchukua viambishi vya wakati na viambishi nafsi.

**Mifano:**

- Watoto **wangali** kitandani.
- Wao **wamekuwa na** uzembe.
    - Vitenzi vishirikishi vipungufu: hivi huchukua viambishi nafsi lakini havichukui viambishi wakati.
- Wezi **si** wazuri**.**
- Yeye **yu** mkweli**.**
- Sisi **ni** walimu**.**

**KAZI 9**

**Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatanyo**

- \- si
- \- mkitenda
- \- u
- \- vaa
- \- ni

## 12.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu Kuhusu Uhakiki wa Tanzu za Fasihi Simulizi

**KAZI 10**

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

**Ukakiki wa Tanzu za Fasihi Simulizi**

- **Maana ya Uhakiki**

Uhakiki ni utathmini, ufasili na uainishaji wa kazi ya fasihi. Ni uchambuzi wa ndani kabisa wa kitu au jambo ulioambatana na fikra za mchambuzi. Uhakiki ni kazi ya kusoma maandishi au kusikiliza mambo fulani kwa kuyachambua na kuyafafanua ili kupata ukweli wa mambo hayo.

Uhakiki ni sayansi maalum ya kuchambua na kudadisi au kupima ubora au udhaifu wa kazi ya kisanaa hasa fasihi. Uhakiki wa tanzu za fasihi huzingatia mambo mawili muhimu yaani fani na maudhui. Fani na maudhui ni mambo mawili ambayo hayawezi kutengana kwa sababu moja hutegemea jingine.

### i) Fani

Fani ni namna msanii anavyowasilisha maudhui yake kwa hadhira. Fani pia huweza kutazamwa kama umbo la nje la kazi ya sanaa yaani sura yake ya nje. Kuchunguza fani ni kuchunguza kiundani vipengele mbalimbali vya kifani na namna vilivyotumika ili kuwasilisha maudhui. Uchunguzi wa fani unazingatia vipengele vifuatavyo: wahusika, muundo, mtindo, mandhari, matumizi ya lugha.

- **Wahusika**

Wahusika ni watu, wanyama, vitu, hata viumbe vya kufikirika ambavyo msanii wa kazi ya fasihi hutumia ili kufanikisha ujumbe kwa jamii husika. Katika kazi za fasihi msanii huwagawa wahusika katika makundi mawili: wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wakuu ni wale ambao wanajitokeza kuanzia mwanzo mpaka mwisho na ndio huwa msingi wa kazi ya fasihi hasa hadithi. Wahusika wadogo ni wale wote ambao wanajitokeza mara chache au sehemu mbalimbali katika kazi ya fasihi na huwasaidia wahusika wakuu katika kubeba maudhui. Wahusika wadogo hawa wanaweza kuwa **watetezi** (wakimsaidia mhusika mkuu) au wakawa **wapinzani** (wakimzuia mhusika mkuu).

Wahusika wa kazi za fasihi wana tabia mbalimbali. Tabia ya kwanza ni **ubapa** yaani tabia ya kutobadilika kwa mhusika toka mwanzo hadi mwisho. Tabia ya pili ni **uduara** yaani tabia ya kubadilika kihulka, kimawazo na kisaikolojia kufuatana na mazingira mapya, wakati, hali, na kadhalika. Tabia ya tatu ni **ufoili.** Ni tabia inayojidhihirisha kati ya ubapa na uduara. Wahusika wenye tabia hii hawaonyeshi msimamo wao kama wanaweza kubadilika au kutobadilika.

**Mtindo**

Ni namna ambavyo msanii huipa kazi yake sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine hawezi kuipa hivyo hata kama jambo lizungumziwalo na wasanii hawa wawili ni lile moja. Mtindo ndio unaomwezesha msomaji, msikilizaji au mtazamaji wa kazi ya fasihi amtambue msanii wa kazi hiyo bila kuelezwa au kusoma jina la msanii huyo. Kuchunguza mtindo wa kazi ya fasihi ni kuangalia matumizi ya lugha katika kazi hiyo. Wakati wa kufanya kazi hiyo tunajiuliza maswali yafuatayo:

- Msanii anatumia lugha namna gani? Je kuna tamathali za usemi, mafumbo, methali, nahau,…
- Picha alizochora msanii zinaeleweka au zimesaidia kurahisisha katika maelezo yake?
- Msanii anatumia mbinu zipi? Mazungumzo, mijadala, hadithi ndani ya hadithi,… ?

- **Muundo**

Ni mpangilio wa kiufundi anaoutumia msanii katika kupanga kazi yake. Pia ni mpangilio na mtiririko wa visa na matukio. Katika muundo tunaangalia vipengele kama ploti. Ploti ni mtiririko wa kiusababishi wa visa na matukio. Aidha, katika muundo tunajiuliza mtiririko huu wa visa na matukio ni wa moja kwa moja au ni wa kiurejeshi? Kama ni wa moja kwa moja ni muundo wa msago. Kama unaenda mbele na kurudi nyuma ni muundo rejeshi.

- **Mandhari**

Mandhari ni sura ya mahali popote palipotumiwa na msanii kwa kukisimika anachokisimulia katika kazi ya fasihi. Kuna Mandhari halisi yaani mahali panapoweza kuonekana, panapojulikana waziwazi, panapopatikana (nchi fulani, wilaya, mkoa, mlima,…) na Mandhari pakubuni yaani mahali pa kujiundia, pa kindoto pasipopatikana (mbinguni, jahanamu, ahera, ujinini, ...)

- **Muktadha**

Muktadha ni mazingira au hali ambamo tukio au jambo fulani hutendeka. Ni kusema kuwa msanii huishi katika jamii na jamii huzungukwa na mazingira mbalimbali. Mazingira haya yanaweza kuonekana katika kazi ya fasihi. Mazingira haya yanaweza kuonekana kulingana na lugha iliyotumiwa, msamiati uliotumiwa, mawazo fulani ya msanii yanayolingana na wakati fulani. Kwa mfano kazi za fasihi simulizi za enzi za ufalme ni tofauti na kazi zilizopatikana baada ya uhuru wa Rwanda.

**ii) Maudhui**

maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumziwa na masanii katika kazi ya kifasihi. Haya ndiyo huwa yamemsukuma msaniii kuisana kazi yake hii. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi yake ya kifasihi. Uchambuzi wa maudhui huzingatia vipengele kama vile dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa na hata mtazamo.

- **Dhamira**

Dhamira ni wazo lililomo katika kazi za sanaa. Kwa kawaida, dhamira zinagawika katika makundi mawili, kuna dhamira kuu na dhamira ndogondogo.

a) **Dhamira kuu:** ni kiini cha wazo kuu la msanii ambalo linaongoza ujumbe autakao msanii kufikisha kwa jamii. Dhamira kuu huweza kuhusu jamii, magonjwa ya zinaa, siasa, uzalendo, uchumi, ushirikiano, umoja na maridhiano, usawa wa jinsia, malezi bora, mapenzi, mazingira na maendeleo endelevu, n.k.

b) **Dhamira ndogondogo:** ni dhamira zile mbalimbali zinazogusiwa na msanii ili kuendeleza dhamira kuu. Dhamira hizi husaidia dhamira kuu katika kujidhihirisha.

- **Ujumbe /Mafunzo**

Mafunzo ni masomo yanayopatikana katika kazi ya fasihi. Kila kazi ya sanaa huwa na ujumbe maalumu ambao msanii anataka uifikie jamii aliyoikusudia. Ujumbe katika kazi za kifasihi ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana ndani ya kazi hiyo. Katika kazi ya fasihi dhamira kuu hubeba ujumbe wa msingi wakati ambapo dhamira ndogondogo hubeba ujumbe ambao husaidia kuujenga au kuupa uzito zaidi ujumbe wa msingi.

- **Migogoro**

Ni hali ya kutokubaliana kimawazo, kimatendo kati ya wahusika. Migogoro hii inaweza kuwa kati ya wahusika binafsi na kizazi kimoja au kati ya kizazi na kingine. Pia inaweza kuwa kati ya watawala na watawaliwa, jamii na misukosuko (misukumano) ya kijamii au kimazingira iliyomo katika eneo fulani.

- **Falsafa**

Kimsingi, falsafa ni elimu ya asili; busara au hekima. Falsafa ya msanii hugusiwa kutokana na jinsi anavyoelewa matatizo ya jamii na jinsi anavyoyatolea suluhisho kwa njia ya busara, amani na utulivu. Katika kazi za fasihi simulizi hususani hadithi zile za paukwa pakawa, falsafa inayojitokeza ni ile isemayo kuwa maisha ni mapambano ya wema dhidi ya ubaya na daima wema huushinda ubaya.

**TANBIHI**

Katika kuhakiki kazi za fasihi simulizi, kila kazi ina mbinu mahususi katika kuichambua. Kwa mfano uchambuzi wa nahau, methali na misemo unatofautiana sana na uchambuzi wa hadithi au mashairi.

- **Umuhimu wa Uhakiki**

Mara nyingi fasihi huwa ngumu kuielewa. Kuna wakati mtu anaweza kusoma au kusikiliza kazi ya fasihi akashindwa kuelewa alichojaribu kueleza msanii. Hapa ndipo uhakiki unahitajika ili kumwongoza katika kuelewa kazi hiyo.

Kwa hiyo, uhakiki wa kazi za fasihi simulizi una umuhimu mkubwa. Baadhi ya umuhimu huo ni kama vile:

a) Kuwezesha kuelewa kazi ya fasihi na kuchunguza kama inatimiza sifa zote. Kila kazi ya fasihi ina sifa zake. Kwa hiyo uhakiki unatusaidia kugundua kwamba kazi ya fasihi inajaza sifa zake zote.

b) Kuwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi. Hapa uhakiki unatuwezesha kupima uzito na ulegevu wa utunzi wa msanii.

c) Kuwezesha kupanua lugha yetu kwa sababu katika kazi ya sanaa kunatumika msamiati, mifumo, semi na mambo mengine mengi yanayokuza lugha yetu.
d) Kuwezesha kuchambua na kumulika mafunzo na maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi. Maonyo na mafunzo hayo yanaweza kutumiwa kwa kujirekebisha au kuirekebisha jamii.

- **Matatizo ya uhakiki**

Hakuna jambo lisilokuwa na ila. Matatizo ya uhakiki ni mengi sana. Kwanza ni vigumu kwa wahakiki kukubaliana kuwa hivi ndivyo ilivyo maana ya kazi ya sanaa husika. Kila mhakiki huweza kusoma na kuelewa kazi hiyo kwa namna yake.

Pili, uhakiki wenyewe ni taaluma ngumu ambayo inahitaji kutumia bidii kubwa ya kuweza kuitawala. Wahakiki wengi wanafanya uchambuzi na uchambuzi huo ukichambuliwa ukaonekana bado una dosari. Jambo hili hutokana na mhakiki kuwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo zinaweza kuwa :

- Kutokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu sifa za utanzu unaohakikiwa,
- Kutawaliwa kwa mhakiki na hisia zake zinazoweza kuleta upendeleo fulani,
- Kutofuata misingi inayozingatiwa katika uhakiki.

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ni ipi maana ya uhakiki?
2. Ni mambo gani tunayochunguza kwa kuhakiki kazi ya fasihi?
3. Taja na ueleze tabia za wahusika.
4. Ni tofauti gani iliyoko baina ya mandhali na muktadha?

## 12.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 11**

***Sikiliza hadithi redioni, ujaribu kuihakiki kisha uwasilishe hadharani.***

## 12.6. Kuandika

**KAZI 12**

***Tunga matini fupi ukizingatia vipengele vya fani na maudhui.***

# SOMO LA 13: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI

## KAZI 1

***Tazama mchoro hapa chini kisha ujibu maswli yatakayofuata***



1. Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.
2. Wahusika hao wako wapi na wanafanya nini?

## 13.1. Kusoma na Ufahamu: Kobe na Kijumbamshale

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini**

Hapo zamani za kale palikuwa na Kobe na Kijumbamshale. Kobe alikuwa mnyamavu, mshindani pamoja na mpole. Kila wakati alikuwa hafanyi jambo lolote ovyo ovyo wala kwa pupa. Kwake, kila jambo lilikuwa na mpango wake kabla ya kulishughulikia kimatendo.

Kwa upande mwingine, Kijumbamshale alikuwa ndege mpinzani, mjuba, mpuuzi na mwenye majivuno. Mara nyingi alikuwa anafanya kazi bila mpango.

Siku moja Kobe na Kijumbamshale walikutana njiani wote wakipunga upepo huku wakielekea kwa kasri ya Malkia Tembo. Walisalimiana na kukaa chini kabla hawajaendelea na safari. Kwa hiyo, walipata fursa ya kuongea sana. Maongezi yao yalipokuwa yakiendelea, Kobe alishangaa sana kumwona Fisi amekuja akikimbia mno. Alikuwa amechelewa kuhudhuria sherehe ya mtoto wa Malkia Tembo. Kobe hakuamini macho yake na kumwonyesha Kijumbamshale, “Angalia pale jinsi Fisi

anavyokimbia kwa mwendo wa kasi. Anakimbia mbio kama umeme. Bila shaka hakuna mnyama hata ndege yeyote anayeweza kumshinda katika mashindano ya riadha." Fisi aliwapitia bila kuwasalimia wakashangazwa na adabu yake.

Kijumbamshale hakuridhishwa hata kamwe na maoni ya Kobe kuhusu Fisi. Mara moja alimgeukia na kumuuliza kwa dharau, "Je, una hakika kwa hayo yote ambayo umeyatamka? Nani aliyekuambia kuwa Fisi yule anaweza kuthubutu kunishinda mimi? Kama wewe ni mlemavu wa miguu na mabawa, usidhani kuwa sisi sote ni sawa nawe."

Kobe alijaribu kumsihi akisema, "Samahani rafiki yangu! Hii siyo sababu ya kukasirika kwa bure! Ukweli mtupu ni kwamba mimi ninaamini kwamba Fisi anaweza kunishinda katika zoezi la mashindano ya kukimbia. Lakini, wewe sahau hilo! Huwezi, huwezi na huwezi hata kamwe! Maishani mwangu wanyama wawili pamoja na ndege mmoja tu ndio niwaogopao katika mashindano ya namna hii. Hao ni Fisi, Sungura pamoja na Tai. Wengine hapana!"

Kijumbamshale alikunja uso na kumwambia mwenzake, "Huna haya kuhakikisha hayo mbele yangu? Kobe hakutaka jambo hili lipambe moto. Hivyo, aliamua kutoa suluhu la kimatendo. "Acha tukubaliane kwenye mashindano ya kukimbia kilomita mbili wakati wa dakika sitini. Atakayeibuka mshindi ndiye atakayekuwa mheshimiwa kati yetu." Kobe alipendekeza.

Bila kusita, Kijumbamshale alikubaliana na Kobe hivi wakiamua siku, mahali pamoja, na wakati wa mashindano. Baada ya kutoka katika sherehe, Kobe hakupata tena utulivu. Alianza kufikiria juu ya mbinu angetumia kujinyakulia ushindi dhidi ya Kijumbamshale.

Siku moja kabla ya mashindano kuwadia, Kobe alikaa peke yake na kufikiri. "Wazazi wangu kabla ya kuaga dunia, walinitolea maonyo ambayo sitayasahau hata siku moja. Wakati mmoja waliniambia 'Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako' na wakati mwingine 'bandubandu humaliza gogo." Kobe aliyakumbuka mashauri ya wazazi. Kutokana na haya, alijisemea kimoyomoyo, "Linalowezekana leo lisingoje kesho." Papo hapo, aliamua kuandaa safari na kuelekea kwenye uwanja wa mashindano asubuhi na mapema. Aliahidiana na jogoo kwamba angemwamsha.

Jogoo alipowika alfajiri, Kobe alikuwa ameishatoka nyumbani kwake kuelekea mahali pa mashindano. Njiani aliwakuta wanyama wengi waliokuwa wakisafisha mbuga yao na kuwasalimu. Walipomuuliza sababu ya safari yake, aliwaeleza kwamba alikuwa katika shindano la kukimbia. Isipokuwa nyani aliyempa motisha kwa kumpa ndizi, wanyama wengine walishika mbavu kwa vicheko kwa kuwa walikuwa wakijua uwezo wake wa kukimbia. Lakini yeye hakukata tamaa akaendelea na safari yake.

Kobe alitembea, akatembea na kutembea. Saa nane mchana, Kobe alikuwa amesogelea mti mkubwa ambapo alikuwa amekubaliana na Kijumbamshale kuwa kikomo cha mashindano. Wakati huo ndipo Kijumbamshale alikumbuka kuwa siku hiyo ilistahili kuwa siku ya mashindano kati yake na Kobe. Alishtuka kwa ghafla na kuruka haraka kwa mwendo usio wa kawaida. Aliruka na kuruka! Lahaula! Alipokuwa umbali wa mita karibu mbili, Kobe alikuwa amejinyakulia ushindi, hivi akishangilia kwa furaha tele.

Kijumbamshale alipomwona Kobe alipoteza nguvu za kuendelea kuruka na kuanguka chini. Kobe alisikia huruma moyoni na kumsogelea Kijumbamshale, "Pole sana ndugu yangu. Katika mashindano ni lazima kuwepo mshindi na anayeshindwa. Lakini siyo mwisho wa dunia. Somo kubwa kutokana na mashindano haya ni kwamba uwezo mkubwa wa kuruka pekee hautoshi, jambo muhimu zaidi ni maandalizi, akili na maarifa ya kufanikisha lengo lolote".

Kijumbamshale aliona haya na kufunga mdomo wake. Baada ya dakika chache, alizinduka na kumwambia Kobe, "Leo nimeona kuwa kila kitu kinawezekana maishani. Sina budi kukubali ushindi wako kwa sababu asiyekubali kushindwa si mshindani. Nimepiga saluti kwa heshima zako mheshimiwa." Na huu ndio mwisho wa hadithi.

**KAZI 2**

**Jibu maswli yafuatayo:**

1. Kifungu hiki ni cha aina gani?
2. Taja wahusika wote wanaozungumziwa katika kifungu cha habari.
3. Fananisha tabia za wahusika wakuu waliozungumziwa hadithini.
4. Kwa nini Kobe alijinyakulia ushindi dhidi ya Kijumbamshale?
5. Ni somo gani unalopata kulingana na kifungu hiki?

## 13.2. Msamiati kuhusu Kobe na Kijumbanshale

**KAZI 3**

**Eleza maneno yafuatayo:**

- Kijumbamshale
- Riadha
- Mjuba
- Malkia
- Kamwe

## KAZI 4

**Tumia maneno yafuatayo kwa kujenga sentensi:**

- Kusita
- Dhidi
- Gogo
- Kumotisha
- Tele

## KAZI 5

**Tafuta majina matano ya michezo kwenye mraba huu.**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | G | O | N | G | O | N |
| R | A | A | D | H | A | W | E |
| I | R | S | A | D | Z | Y | T |
| K | A | B | U | M | B | U | I |
| M | A | T | V | B | E | J | B |
| K | I | K | O | N | B | G | O |
| D | R | A | F | T | I | W | L |
| N | U | N | D | O | N | D | I |

## 13.3. Sarufi: Aina za Maneno ya Kiswahili

**KAZI 6**

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha utaje aina za maneno yaliyopigiwa mistari.**

- Kobe **na** Kijumbamshale walikaa **chini ya** mti.
- **Lo**! Umemwona fisi yule!
- Kijumbamshale alishindwa na Kobe **katika** riadha.
- Linalowezekana **leo** lisingoje **kesho**.
  - **Na**: ni kiunganishi
  - **Chini ya**, **katika**: ni vihusishi
  - **Lo**!: ni kihisishi/kiingizi
  - **Leo**, **kesho**: ni vielezi

**Maelezo Muhimu kuhusu Aina za Maneno**

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina nane za maneno. Aina hizo ni kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kihusishi, kielezi, kiunganishi na kihisishi. Katika somo letu tutagusia aina nne yaani kihusishi, kihisishi, kiunganishi na kielezi.

- **Viunganishi**

Viunganishi ni maneno yanayofanya kazi ya kuunganisha. Huonyesha uhusiano baina ya neno na neno, fungu moja la maneno na fungu jingine au sentensi na sentensi.

**Mifano:**

- Unataka maji **au** juisi?
- Anasoma kitabu **badala ya** kupiga ubwana.
- Kufanikiwa maishani si bahati **bali** ni kujishughulisha **na** kujitolea.
- Alishinda mtihani **ijapokuwa** alipatwa na ugonjwa mkali.
- Alienda shuleni **bila** kupata chakula.

## KAZI 7

**Tumia viunganishi vifuatavyo kwa kutunga sentensi:**

- Halafu
- Kisha
- Ili
- Ingawa
- Kama

- **Vihisishi**

Vihisishi ni maneno ambayo yanaonyesha hisia za mtu za ndani kwa mujibu wa hali na muktadha. Yanaonyesha hangaiko la moyo ama kudokeza mguso wa moyo ama hata wa akili. **Mifano**:

- **Mtume**! Umefika asubuhi hii!
- **Lo**! Mvua imenyesha!
- **Salaa**! Inawezekana mtu kunywa chupa ishirini za juisi!

## KAZI 8

**Tunga sentensi kwa kutumia vihishi vifuatavyo:**

- Mungu wangu!
- Mama wee!
- Ng'o!
- Barabara!
- Masalale!

- **Vielezi**

Vielezi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu kitendo kilivyofanyika. Pia vielezi hutoa habari zaidi kuhusu hali, vivumishi na vielezi vingine.

Kuna vielezi vya namna, vielezi vya wakati, vielezi vya mahali na vielezi vya kiasi.

**Mifano:**

- Mwanafunzi yule ameshinda mtihani **vizuri**.
- Mvua itanyesha **kesho**.

- Wanyama huishi **misituni**.
- Mvua ilinyesha **mara mbili** kwa mwezi.

## KAZI 9

***Onyesha na utaje aina za vielezi vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo:***

- Simba akitaka kupata windo hutembea kimya.
- Baba anavaa kizungu, wewe kichina.
- Jina lake lilitajwa mara kadhaa.
- Pipa hili limejaa pomoni.
- Imenyesha usiku kucha.

- **Vihusishi**

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano baina ya watu au vitu viwili au zaidi. Kuna vihusishi vya mahali na vya wakati.

**Mifano:**

- Nitakutembelea **baada ya** masomo .
- Alisafiri **nje ya** nchi.
- Ng'ombe hulala **ndani ya** zizi.
- Amefika hapa **kabla ya** mvua kunyesha.
- Wao wanaishi pamoja **kwa** amani.

## KAZI 10

***Tumia vihusishi vifuatavyo kwa kujaza mapengo: katika, kabla ya, mbele ya, baada ya, ndani ya.***

- Nafasi ya Kalisa darasani iko................. nafasi ya Maria.
- .................mvua kunyesha unaona dalili zake.
- Watu wengi waliangamia ..............vita vikuu vya dunia vya pili.
- ...............dhiki faraja.
- Hakuna Mnyarwanda anayeishi..........nyumba ya msonge siku hizi.

## 13.4. Matumizi ya Lugha: Maelezo Muhimu kuhusu Uhakiki wa Hadithi za Masimulizi

**KAZI 11**

***Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini***

***Uhakiki wa hadithi za masimulizi***

Uhakiki wa hadithi za masimulizi ni kazi au kitendo cha kuchambua na kufafanua vipenge vya fani na maudhui katika hadithi hizo. Vipengele vya fani na maudhui ni pamoja na wahusika, muundo, mtindo, dhamira, migogoro na ujumbe.

- **Fani katika Hadithi za Masimulizi**

Ikumbukwe kuwa fani ni ufundi au mbinu anayoitumia msanii wa fasihi ili kutoa au kufikisha maudhui kwa watu aliowakusudia. Tunapohakiki hadithi ya masimulizi kifani, tunachunguza wahusika, mtindo, muundo, mandhari, na mengineyo.

**1. Wahusika**

Wahusika ni watu, wanyama, vitu, hata viumbe vya kufikirika ambavyo msanii wa hadithi hutumia ili kufanikisha ujumbe kwa jamii husika. Katika hadithi msanii huwagawa wahusika katika makundi mawili: wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wadogo wanaweza kuwa watetezi au wakawa wapinzani.

Wahusika katika hadithi za masimulizi hutegemea aina ya hadithi simulizi. Kwa mfano:

- **Ngano**: Hadithi ambayo wahusika wake ni mchanganyiko wa wanyama, wadudu, mizimu, miungu, miti, watu, na viumbe visivyo na uhai kama mawe, miamba, n.k.
- **Hekaya**: Hadithi ambayo wahusika wake kwa kawaida ni binadamu tu.
- **Hurafa**: Hadithi ambazo wahusika wake huwa ni wanyama wanaopewa tabia na vitendo vya kibinadamu.
- **Visasili**: Hadithi hizi zinazohusu asili ya mambo fulani.
- **Soga**: Hizi ni hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli. Wahusika wake ni watu wa kubuni lakini wanapewa majina ya watu walio katika mazingira hayo.
- **Visakale au Mighani**: Ni hadithi ambazo wahusika wake ni watu waliotenda matendo ya kishujaa na wanaosifiwa katika jamii fulani.

**Tabia za wahusika katika hadithi za masimulizi**

Wahusika katika hadithi simulizi hupewa tabia za aina mbalimbali. Hawa wanaweza kuwa na tabia ya:

- **Ubapa**: tabia ya kutobadilika
- **Uduara**: tabia ya kubadilika
- **Ufoili**: tabia ya kutoonyesha msimamo

Kwa upande mwingine, katika hadithi za masimulizi tunatumia wanyana kwa mara nyingi. Wanyama hawa huwakilisha binadamu katika jamii waishimo. Hili ni kwa sababu utumiaji wa majina halisi ya watu unaweza kuzua ugomvi katika jamii. Wanyama wanaotumiwa sana katika hadithi za masimulizi ni kama:

- **Sungura**: Mara nyingi Sungura hupewa tabia za ujanja, ndiyo sababu huonekana mahali pengi kama Sungura-mjanja. Kwa hiyo, Sungura huwakilisha watu wenye ujanja kwa madhumuni ya kula jasho la wengine, kuwaangamiza adui zao au kuwaangusha mtegoni pamoja na kuwategua wanyama wakubwa kama vile simba.
- **Simba**: Mnyama huyu hutumika mara nyingi kama kiongozi au mfalme. Katika jamii ya wanadamu huwakilisha watu wenye ukali ambao wakiongea husikika na huogopewa sana.
- **Fisi**: Mnyama huyu huonekana kama mhusika mwenye tamaa na ulafi ambaye fikra zake zimetawaliwa na tamaa yake. Pia fisi hupewa tabia ya uchoyo, woga pamoja na ujinga. Fisi hutumika kuwakilisha wanadamu waroho, woga, wazembe na wajinga, wasiopenda kufikiria sana kwani mawazo yao yametawaliwa na tamaa zao.
- **Nyani:** Katika hadithi, nyani hudhihirisha hekima na uwezo wa kufanya uamuzi wa busara. Hutumika sana kama hakimu na huwakilisha viongozi wenye hekima katika jamii.
- **Nyoka**: Mnyama huyu hupewa tabia ya hila na huwakilisha watu wenye hila/ udanganyifu katika jamii.
- **Kobe**: Huwakilisha watu wanyamavu, ambao japo wanajua kufanya kitu, hawapendi kuchangia, lakini mwisho huibuka washindi; watu wasiokimbilia kufanya mambo.
- **Ndovu:** Huwakilisha watu wenye kimbelembele, ambao hujisifu na kujitafutia umaarufu. Watu wa aina hii hupenda kuwa katika mstari wa mbele japo huenda hawana ujuzi wa kutosha katika jambo hilo.
- **Chui:** Chui ni mnyama mkatili sana. Katika hadithi yeye huwakilisha tabia ya uharifu.
- **Kinyonga**: Huyu huwakilisha tabia ya ugeugeu. Watu wenye tabia ya aina hii hawaonyeshi msimamo mmoja.
- **Kunguru**: Huyu ni ndege mwoga sana. Katika hadithi yeye huwakilisha watu ambao ni waoga.

## 2. Mtindo

Mtindo ni mbinu ya kipekee kwa kila msanii katika ufundi wake wa kifasihi. Kwa mfano, namna msanii anavyotumia lugha (nahau, misemo, methali, tamathali za usemi) na anavyoteua msamiati wa msingi. Hii ni kwa sababu lugha ndiyo wenzo mkubwa wa msanii katika kazi za fasihi. Isitoshe kwa kuchunguza mtindo tunachunguza namna msanii anavyosimulia hadithi yake (anaweza kutumia nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu, anaweza kutumia nyimbo kwa ajili ya burudani, n.k.). Kwa kutunga hadithi ya masimulizi msanii anaweza kutumia majina ya watu au akatumia wanyama, wadudu, ndege, miungu na kadhalika.

## 3. Muundo

Ni mpangilio wa kiufundi anaoutumia msanii katika kupangilia zoezi lake, mpangilio na mtiririko wa hadithi, kwa upande wa visa na matukio. Msimuliaji anaweza kufuatanisha matukio moja kwa moja (Msago) au akasimulia kwa kurukaruka hatua, yaani msimuliaji anaweza kuanzia katikati, akaja mwisho na kumalizia na mwanzo (urejeshi).

Isitoshe, hadithi za masimulizi au za paukwa pakawa huwa na mipangilio maalum. **Hadithi hizi huwa na fomula yake katika utangulizi na mwisho wake.**

- **Mianzo ya hadithi za kimapokeo**

i) **Mtambaji:** Paukwa!

**Hadhira**: Pakawa!

**Mtambaji**: Paukwa!

**Hadhira**: Pakawa!

**Mtambaji**: Kaondokea chanjagaa

Kajenga nyumba kakaa

Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Cha kujengea kikuta

Na vilango vya kupitia

Atokeani!

**Hadhira:** Naam twaibu!

**Mtambaji**:Hapo zamani za kale………………….

ii) **Mtambaji:** Paukwa!

**Hadhira**: Pakawa!

**Mtambaji**: Sahani!

**Hadhira**: Ya mchele!

**Mtambaji**: Giza!

**Hadhira**: La mwizi!

**Mtambaji**: Baiskeli!

**Hadhira**: Ya mwalimu! n.k.

**Mtambaji**: Hadithi hadithi!

**Hadhira**: Hadithi njoo!

**Mtambaji**: Hadithi hadithi!

**Hadhira**: Hadithi njoo!

**Mtambaji**: Hapo zamani za kale palikuwepo na ...............................

**iii)** **Msimulizi:** Atokaeni!

**Hadhira**: Naam Twaibu!

**Msimulizi**: Kaondokea chanjagaa, n.k.

- **Hadithi huwa pia na miisho yake**

Hadithi ikimalizika tunasema: "***Huu ndio mwisho wa hadithi***" au "***Hadithi inakomea hapa***."

### 1. Mandhari

Ni sehemu ambayo matukio ya hadithi au masimulizi hutokea. Mandhari huweza kuwa **halisi** kama vile nyumbani, baharini, njiani, msituni, kijijini, mjini lakini vyote vinavyojulikana au ya **kufikirika** kama vile kuzimuni, mbinguni, peponi na kadhalika. Katika hadithi nyingi za masimulizi wanatumia mandhali pa kubuni kwa sababu mandhari hayo huwa ni ya kujiundia.

### 2. Muktadha

Muktadha ni mazingira au hali ambamo tukio au jambo fulani hutendeka. Ni kusema kuwa msanii huishi katika jamii na jamii huzungukwa na mazingira mbalimbali. Mazingira haya yanaweza kuonekana katika hadithi. Ukichambua hadithi za masimulizi utagundua mazingira yaliyokuwa yakiwazunguka wasanii. Haya yote huonekana kulingana na msamiati na dhamira msanii alizotia ndani ya hadithi.

**Tanbihi**: Mbali na vipengele vilivyotajwa hapo juu, tunapochambua hadithi tunaanzia kwa kutaja kichwa na mtunzi kama anajulikana. Lakini mara nyingi watunzi wa kazi za masimulizi hawajulikani. Kazi za masimulizi ni mali ya jamii.

- **Maudhui katika hadithi za masimulizi**

**Maana ya maudhui**

Katika somo la kwanza katika mada hii tuliona kuwa, katika kazi ya fasihi, maudhui ni jumla ya mambo yote yanayozungumzwa au yaliyomsukuma msanii kuisana kazi yake.

Katika uhakiki wa hadithi za masimulizi kimaudhui, vipengele vifuatavyo ni lazima vizingatiwe: dhamira, migogoro, mitazamo falsafa, ujumbe pamoja na msimamo wa msanii.

**1. Dhamira**

Dhamira huelezwa kama wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Kwa kawaida, dhamira zinagawika katika makundi mawili, kuna dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Dhamira zinazozungumziwa sana katika hadithi za masimulizi ni uongozi, amani na maendeleo, mauaji, uroho, ujanja, hila, uchoyo, upendo, uzalendo, ushirikiano, ujinga, uhaini, usaliti, wivu na kadhalika.

**2. Migogoro**

Migogoro ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi za fasihi. Migogoro inaweza kuwa kati ya wahusika, familia zao, matabaka yao, au hata katika nyadhifa mbalimbali.Vilevile, migogoro yaweza kuwa ya kiuchumi, kijamii, migogoro ya nafsi, migogoro ya kisiasa, n.k. Katika hadithi za masimulizi nyingi tunakuta migogoro kati ya wahusika wenye nguvu na wale wasio na nguvu na kwa mara zote wenye nguvu huishia kwa kuanguka.

**3. Falsafa**

Kimsingi, falsafa ni elimu ya asili; busara au hekima. Falsafa ya msanii hugusiwa kutokana na jinsi anavyoelewa matatizo ya jamii na jinsi anavyoyatolea suluhisho kwa njia ya busara, amani na utulivu. Falsafa ya msanii wa hadithi za masimulizi hugundulika unaposoma hadithi zake nyingi. Hapo ndipo utagundua mawazo au saikolojia yake.

**4. Ujumbe**

Kila kazi ya sanaa huwa na ujumbe maalumu ambao msanii anataka uifikie jamii aliyoikusudia. Ujumbe katika hadithi za masimulizi ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana ndani yake. Kwa kuwa hadithi zina umuhimu wa kuelimisha jamii ndiyo maana kila unapomaliza kusoma au kusikiliza hadithi unaombwa kueleza somo ambalo umepata.

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Katika uhakiki wa fani ya hadithi tunachunguza nini ?
2. Taja na ueleze aina tano za hadithi.
3. Falsafa ya masanii ni nini?
4. Kwa sababu gani kuelewa usuli ni jambo muhimu?

- **Mfano wa uhakiki wa hadithi ya masimulizi**

**1. Fani**

- **Kichwa cha hadithi**: Kobe na Kijumbamshale
- **Mtunzi**: hajulikani.
- **Wahusika**
- **Wahusika wakuu**: Kijumbamshale, Kobe
- **Wahusika wadogo**: Jogoo, Fisi na Nyani na wanyama waliokuwa wakisafisha mbuga.
- **Watetezi**: Jogoo (Alimwamsha Kobe) na Nyani (alimpatia ndizi)
- **Wapinzani**: Wanyama waliokuwa wakisafisha mbuga (walimcheka Kobe).
- **Tabia za wahusika**: Kobe ni mhusika bapa kwa sababu hakubadilika na Kijumbamshale ni mhusika duara kwa sababu alibadilika kimawazo (alianzia kwa kupinga uwezo wa Kobe lakini mwishowe alikubali).
- **Aina ya hadithi**: Hurafa (wahusika ni wanyama na ndege).
- **Mtindo**: Katika hadithi hii masanii alitumia lugha ya kawaida. Hadithi imeandikwa kwa lugha ya nathari (katika aya). Msanii alitia mazungumzo katikati. Msanii alitumia:

- Nahau: kunyakua ushindi (kushinda), kupunga hewa (kupumuzika), kukunja uso (kukasirika)
- Methali: Chelewachelewa utamkuta mtoto si wako, bandubandu huisha gogo, linalowezekana leo lisingoje kesho.
- Tamathali za usemi: kukimbia mbio kama umeme (tashbiha), takriri (chelewachelewa, bandubandu).

- **Muundo**

- Mwanzo wa hadithi ni "Hapo zamani za kale". Na mwisho wake ni "Na huu ndio mwisho wa hadithi."
- Msanii alitumia msago kwa sababu alisimulia moja kwa moja bila kuchanganya matukio.
- Msanii alitumia nafsi ya tatu kwa kusimulia hadithi yake. Lakini pia alitumia nafsi ya kwanza na ya pili alipotumia mazungumzo kati ya Kijumbamshale na Kobe.

- **Mandhari**

Mahali panaposimuliwa hadithini ni njiani, kasri ya Malkia Tembo, Mbuga ya wanyama: mandhari haya ni halisi kwa sababu ni mahali panapoweza kuonekana.

- **Muktadha**

Mtunzi alikuwa akiishi katika mazingira yenye dharau, bezo na upinzani kati ya watu.

**2. Maudhui**

- **Dhamira**
- **Dhamira kuu**: kupingana kati ya kobe na Kijumbamshale
- **Dhamira ndogo**: usafi, harusi, michezo, dharau

- **Migogoro**

Migogoro inayopatikana katika hadithi hii ni migogoro kati ya wahusika Kijumbamshale na Kobe (kutokubaliana kwa yule anayeweza kushinda mwingine katika mbio).

- **Falsafa**

Falsafa ya mtunzi inatazamwa kwa kuangalia ni kipi ambacho mtunzi anaangalia kuwa huo ndio ukweli katika maisha. Katika hadithi hii, inaonekana mtunzi anaamini kwamba mafanikio katika maisha yanaletwa na uthubutu na maandalizi ya kina.

- **Ujumbe/ funzo**

- Kutodharauliana
- Kukubali matokeo ya shindano
- Kuwa na adabu njema (Fisi alipitia wenzake bila kuwasalimu)

## 13.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 12**

***Kumbuka hadithi uliyowahi kusikiliza, uihakiki kisha uwasilishe darasani.***

## 13.6. Kuandika

**KAZI 13**

***Tunga hadithi ya masimulizi huku ukizingatia vipengele vya fani na naudhui.***

**Tathmini ya Mada ya Sita**

1. Ni ipi maana ya uhakiki?
2. Ni mambo gani makubwa tunayochunguza kwa kuhakiki kazi ya fasihi?
3. Taja na ueleze tabia za wahusika.
4. Ni tofauti gani iliyoko baina ya mandhari na muktadha?
5. Katika uhakiki wa fani ya hadithi tunachunguza nini?
6. Taja na ueleze aina tano za hadithi.
7. Kwa sababu gani tunatumia wanyama katika hadithi za kimasimulizi?
8. Taja aina zote za maneno zinazojenga sentensi zifuatazo :

i) Mvua ambayo ilinyesha jana ilisababisha mafuriko mabondeni.

ii) Yeye ni mwanafunzi mcheshi sana.

iii) Tumbiri huishi ndani ya msitu wa Nyungwe.

iv) Lo! Majangili walichoma msitu ili wawaue wanyama.

v) Mama yetu alikuwa akipenda kutushauri kuhusu uwekezaji.

# MADA YA 7

# TANZU ZA FASIHI ANDISHI

## Uwezo mahususi

Kuelezea na kutofautisha tanzu za fasihi andishi

**Malengo ya Ujifunzaji**

- Kueleza kwa ufasaha maana ya fasihi andishi,
- Kubainisha na kueleza tanzu za fasihi andishi,
- Kutetea dhima au umuhimu wa fasihi andishi katika jamii,
- Kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi,
- Kutunga sentensi sahihi za Kiswahili kwa kuzingatia muundo wa sentensi.

**Kidokezo**

Toa maoni yako kuhusu maswali yafuatayo:

1. Fasihi andishi ni nini?
2. Ni vipengele au tanzu gani ambazo zinaiunda fasihi andishi?
3. Unadhani fasihi andishi ina umuhimu gani katika jamii?
4. Kuna tofauti gani kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi?

# SOMO LA 14: FASIHI ANDISHI NA DHIMA YAKE KATIKA JAMII



**KAZI 1**

***Tazama kwa makini mchoro hapa juu. Je, watu hawa wanashughulikia kazi gani?***

## 14.1. Kusoma na Ufahamu: Mwangaza wa Maisha

*Belinda na Didier ni wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Malezi Bora. Katika mawasiliano yao wametetea umuhimu wa fasihi andishi katika kuimarisha ushirikiano, umoja na maridhiano katika kijiji chao.*

**Belinda**: Didy, hapa nimekufumbia fumbo aina ya chemshabongo. Tunu ya kupendeza kwako utakapolifumbua wazi.

**Didier**: Tunu gani hiyo? Niambie Beli! Udadisi umeniingia mwilini kote! Maana yake nimesumbuka sana!

**Belinda**: Didy umenaswa! Wewe hupenda kulipwa kabla ya kazi! Fumbua kwanza zawadi baadaye.

**Didier**: Samahani dada! Sasa nimetega sikio. Lakini tafadhali usiniangushe mtegoni wa kushindwa.

**Belinda:** Punguza wasiwasi kakangu! Fumbo ni hili: Ni kitu gani cha maajabu kilichochangia kuleta umoja na maridhiano katika kijiji chetu cha Ushujaa miaka miwili iliyopita?

**Didier**: Fumbo kali sana! Jambo ninalokumbuka ni kwamba kabla ya miaka miwili iliyopita, hali ya umoja na maridhiano katika kijiji chetu ilikuwa imezorota mno. Iliboreshwa baadaye na mchango wa maigizo ya tamthilia kutoka Shirika la Burudani katika Jamii. Wachezaji waliigusia migogoro kadhaa inayoiangamiza jamii yetu na kuitolea suluhisho ambalo matokeo yake yalitufikisha kwenye ushirikiano, umoja na maridhiano.

**Belinda:** Hongera Didy kwa fumbuo hili! Fumbo la pili sasa: Maigizo hayo ya tamthilia ni aina ya fasihi andishi. Kwa maoni yako, fasihi andishi ina lengo gani katika jamii kwa ujumla?

**Didier:** Sitaki Beli, usininyang'anye! Kwanza kumbuka kuwa ahadi ni deni. Zawadi yangu vipi?

**Belinda:** Hahaaaa! Bado fumbo halijafumbuliwa kikamilifu. Usikate tamaa, tunaelekea mwishoni mwake.

**Didier:** Haidhuru! Fursa ninayo. Kwa maoni yangu, dhima ya fasihi yoyote ni kuielimisha na kuionya jamii kwa ajili ya kurekebisha mienendo ambayo si mizuri ndani ya wanajamii.

**Belinda:** Vizuri sana Didy! Je, ni hayo tu? Hukumbuki jinsi raia walivyofurahia mdundo wa ngoma pamoja na sauti nyororo za wachezaji wa tamthilia hiyo?

**Didier:** Kweli sana! Tamthilia ile ilikuwa na lengo jingine la kukuza lugha pamoja na kuiburudisha jamii.

**Belinda:** Asante sana Didy kwa nia yako ya kuchunguza maendeleo ya jamii yetu.

**Didier:** Inayofuata ni fursa ya kupewa zawadi yangu.

**Belinda:** Umeishapewa! Kuelewa umuhimu wa fasihi andishi katika maendeleo ya jamii ni zawadi yenye thamani kubwa kuliko pesa au kitu kingine.

**Didier:** Jambo hilo naliunga mkono. Matokeo ya fasihi ile yalikuwa mwangaza wa maisha katika jamii yetu.

**Maswali ya ufahamu**

## KAZI 2

***Soma kifungu cha habari hapa juu na kujibu maswali ya ufahamu yafuatayo*:**

1. Ni wahusika gani wanaozungumza katika mazungumzo haya?
2. Nini umuhimu wa fasihi uliotetewa katika mazungumzo yao?
3. Jamii yao ilikuwa na matatizo gani?
4. Suluhisho lilipatikanaje?
5. Je, Didier alipewa zawadi ambayo alikuwa ameahidiwa na Belinda? Eleza msimamo wako.

## KAZI 3

***Chagua jibu lililo sahihi kuliko mengine***

**1. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia:**

a) Wanafunzi wa Chuo cha Ualimu  Malezi Bora
b) Umuhimu wa fasihi andishi katika jamii
c) Shirika la Burudani katika Jamii
d) Zawadi baada ya kufumbua fumbo

**2. Dhima ya fasihi andishi ni:**

a) Kuigiza tamthilia
b) Kuhifadhi kazi za sanaa kimazungumzo
c) Kukuza lugha na kuelimisha
d) Hakuna jibu sahihi

**3. Maana ya fasihi andishi ni:**

a) Maigizo ya tamthilia
b) Fasihi ya wazungu
c) fasihi yenye umuhimu sana katika jamii
d) sanaa inayopitishwa kwa njia ya maandishi

**4. Kweli au uongo**

a) Belinda na Didier walikuwa wanaelewa kwa kiwango sawa dhima ya fasihi andishi katika jamii
b) Belinda alimnyang'anya Didider zawadi yake
c) Belinda atakuwa mwalimu mzuri
d) Didier alifaulu zoezi lake la kufumbua fumbo
e) Belinda aliwahi kumshawishi Didier

## 14.2. Matumizi ya msamiati

### KAZI 4

***Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kutunga sentensi yako binafsi bila kutegemea ile kutoka kifungu cha habari.***

1. Mwangaza
2. udadisi
3. tunu
4. kunasa
5. maridhiano

### KAZI 5

***Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia fumbo, kukatisha tamaa, kunyang'anya, mzozo, chemshabongo, kuburudisha***

a) Kama mwalimu, si vizuri .....................wanafunzi haki za kutoa hoja zao darasani.

b) Uvivu ni jambo la............................katika harakati za kuiendeleza jamii.

c) Hali ya kuzorota kwa amani katika familia ya jamaa ilitokana na................ wa ukosefu wa ushirikiano.

d) Mdundo wa ngoma hutumiwa katika michezo ya .......................

e) Vitendawili ni aina ya.......................la ..................................

## 14.3. Sarufi: Maana ya tungo

### KAZI 6

***Tazama sentensi zifuatazo na kueleza maana ya neno tungo na muundo wake.***

i) Tumefurahi

ii) Tunaipenda nchi yetu

iii) Elimu hukuza akili.

**Maelezo muhimu**

Tungo ni neno au nomino inayotokana na kitenzi "tunga." Kutunga ni kuweka/kushikamanisha vitu pamoja kwa kutumia kitu kama kamba au uzi kwa kupitishia ndani yake. Tunaposhikamanisha vitu pamoja tunapata kitu kinachoitwa utungo (katika umoja) au tungo (katika wingi). Kwa maana nyingine, utungo au sentensi ni kundi la neno moja au maneno zaidi yenye kiima na kiarifa na inayofuata kanuni za sarufi. Tungo ni neno au kikundi cha maneno ambacho hudokeza taarifa fulani ambayo huweza kuwa kamili au isiyo kamili.

**Muundo wa tungo**

Muundo wa sentensi kimapokeo/kikazi/kidhima huwa na vipengele vifuatavyo:

- Kiima: Ni sehemu katika sentensi ambayo hujaza sehemu ya mtenda au mtendwa wa jambo linaloelezwa. Katika tungo kiima hutokea kushoto mwa kitenzi.
- Kiarifa: Ni sehemu katika sentensi inayojazwa na maneno yanayoarifu tendo lililofanywa, linapofanywa au litakapofanywa. Kiarifa ndiyo sehemu muhimu zaidi katika sentensi ambayo wakati mwingine huweza kusimama pekee, kwani wakati mwingine huchukua viwakilishi vya kiima.

Sentensi huwa na vifungu mbalimbali. Baadhi ya vifungu hivi ni vishazi na virai.

**i) Virai**

Kirai ni fungu la maneno lisilokuwa na kitenzi.

Kuna aina nne za virai:

- **Kirai Nomino**: ni fungu la maneno katika sentensi lenye nomino (Kikundi Nomino/Kiima)

**Mfano:**

<u>Wanafunzi</u> wanapaswa kushirikiana darasani na nje ya darasa.

<u>Walimu na wazazi</u> wanaombwa kushughulikia pamoja maadili ya wanafunzi.

<u>Elimu kuhusu usawa wa jinsia</u> inatakiwa kwa watu wa marika yote.

- **Kirai Kiwakilishi**: ni fungu la maneno linalowakilisha nomino katika sentensi

**Mfano:**

Wenyewe watajenga nchi yao.

Atakayetumia dawa za kulevya atahatarisha maisha yake.

Wao walipanda miti mingi kwa ajili ya kuhifadhi mazingira.

- ***Kirai Kivumishi***: *ni fungu la maneno katika sentensi linalotupa habari zaidi kuhusu nomino.*

**Mfano:**

Matunda tuliyokuwa tunatarajia yatapatikana.

Mahali penye kutupwa taka ovyo panaambukiza magonjwa.

Mtu mkatili kuliko shetani hataleta mchango wowote katika jamii.

- **Kirai Kielezi*:*** ni fungu la maneno linaloelezea zaidi kuhusu kitenzi au kivumishi.

**Mfano:**

Raia wanakatazwa kuponda mali yao ovyo ovyo.

Wanawake na wanaume wakishirikiana wataishi kwa amani na furaha milele na milele.

**b) Vishazi**

Kishazi ni sehemu ya sentensi yenye kitenzi. Kuna aina mbili za vishazi:

1. **Kishazi huru:** huwa na maana kamili na kinaweza kujisimamia chenyewe kama sentensi.

**Mfano:**

Wanafunzi wote wa mwaka wa nne wamefanikiwa.

Anayeingia katika mambo ya uzinifu anaweza kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

Tutafungua akaunti benkini kwa ajili ya kukuza kazi za kibiashara.

2. **Kishazi Tegemezi:** huhitaji kuunganishwa na kishazi kingine ili kuleta maana iliyokusudiwa. Aghalabu huwa na kirejeshi k.v amba-, -enye, n.k

**Mfano:**

Kila mtu atapewa zawadi baada ya kuonyesha mwenendo mwema.

Yeyote aliyehusika na vitendo vya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi atahukumiwa.

**KAZI 7**

***Bainisha vishazi katika sentensi zifuatazo:***

1. Mahali pengi pamesafishwa isipokuwa pale.
2. Aliyetajirika atatajirika zaidi.
3. Tutakaposhirikiana kikamilifu tutaweza kuiendeleza nchi yetu.
4. Tulichagua mchepuo wa Ualimu kwa madhumuni ya kuimarisha sekta ya elimu.

## 14.4. Matumizi ya lugha: Fasihi andishi na dhima yake katika jamii

**KAZI 8**

**Jadili maana ya fasihi andishi**

**Maelezo muhimu**

**Fasihi andishi ni** **sanaa** itumiayo **maandishi** kufikisha **ujumbe** kwa hadhira iliyokusudiwa.

Kwa maana nyingine, fasihi andishi ni aina ya sanaa ambayo hutumia maneno yaliyoandikwa kupitisha ujumbe.

Ni sanaa inayopitishwa kwa njia ya maandishi.

**KAZI 9**

**Jadili dhima au umuhimu wa fasihi andishi katika jamii**

**Maelezo ya kuzingatia**

- Kuburudisha jamii. Takribani vipera vyote vya fasihi huwa na kusudi la kufurahisha, kutumbuiza na kusisimua hadhira.
- Kuelimisha. Fasihi hukusudia kuelimisha hadhira kuhusu jamii, mazingira, n.k
- Kudumisha maadili katika jamii kwa kuelekeza, kuonya na kunasihi hadhira jinsi ya kufuata mwelekeo unaokubalika katika jamii.
- Kuunganisha jamii. Fasihi huleta pamoja watu katika jamii. Kwa mfano, katika nyimbo, miviga, vichekesho.

- Kukuza lugha. Aghalabu tungo zote za fasihi hutumia lugha. Isitoshe, fasihi hutumia mbinu nyingi za lugha. Wasimulizi na wandishi wa fasihi huhitaji kuwa na ukwasi wa lugha.
- Kuhifadhi mila, tamaduni na itikadi za jamii. Aghalabu kazi za fasihi (hasahasa Fasihi Simulizi) huambatanishwa na desturi mbalimbali za jamii husika.
- Kukuza uwezo wa kufikiri. Vipera vingi vya fasihi huwachochea hadhira kufikiri sana ili kupata suluhisho. k.m vitendawili, ngano za mtanziko, n.k

**KAZI 10**

**Onyesha tofauti baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi**

**Maelezo ya kuzingatia**

| FASIHI SIMULIZI | FASIHI ANDISHI |
|---|---|
| ▪ Huwasilishwa kwa njia ya mdomo na/au matendo. | Huwasilishwa kwa njia ya maandishi. |
| ▪ Ni mali ya jamii | Kazi andishi ni mali ya mwandishi (na mchapishaji). |
| ▪ Msimulizi anaweza kubadilisha sehemu fulani. | Kitabu kilichoandikwa hakiwezi kubadilishwa. |
| ▪ Huhifadhiwa akilini na kusambazwa kwa njia ya masimulizi. | Huhifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa njia ya maandishi. |
| ▪ Kazi simulizi hubadilika na wakati. | Kazi andishi haibadiliki na wakati. |
| ▪ Huhitaji msimulizi na hadhira yake wawe mahali pamoja wakati wa masimulizi. | Msomaji anaweza kusoma kitabu cha hadithi peke yake, mahali popote, wakati wowote. |

## 14.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 11**


***Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo kati ya Belinda na Didier***


## 14.6. Kuandika

**KAZI 12**

***Tunga kifungu cha habari chenye aya nne kuhusu faida za maandishi katika maisha ya jamii ya kila siku.***

# SOMO LA 15: TANZU ZA FASIHI ANDISHI





KAZI 1

***Tazama kwa makini mchoro hapa juu na kujadili kinachoendelea hapo.***

## 15.1. Kusoma na Ufahamu: Akili ni Mali

Dhana ya utajiri inaendelea kuwa mada tata kati ya matajiri na watu duni. Kuna wanaoshuku kuwa utajiri ni mali iliyorithiwa na vizazi vikongwe kwa vizazi vichanga. Watu wanaotetea msimamo huu hukubali kwamba unapozaliwa na kulelewa katika familia fukara hivyo utafariki katika hali ya wasiwasi na ya masumbuko. Wengine huamini kuwa utajiri hushughulikiwa na hufikiwa kwa njia tofauti. Hivyo utawasikia watu wakitoa madai kama ifuatavyo:

“Utajiri wa jamaa yule ulipatikana kwa matumizi ya hila za hali ya juu.”

“ Bwana yule hakuwa na nguo ya kujikinga dhidi ya upepo wala chumba cha kulala. Lakini leo ameishajenga ghorofa tele. Ametajirika hivi majuzi baada ya kutoka kuzimuni.”

“ Unamuona bibi yule katika gari lenye thamani kubwa sana! Habari zilizosambaa zinasema kwamba alipandishwa vyeo miongoni mwa matajiri wanaojulikana kwa ngazi ya kimataifa baada ya kuwadhulumu urithi watoto yatima aliokuwa anawalea”.

Licha ya madai haya yote, mimi nina ushahidi wangu niliòshuhudia mimi mwenyewe kwa macho yangu kuhusu familia moja ambayo ilipata utajiri kwa kutegemea akili za kielimu. Familia ya bwana Bahati na bibie Fifi ilikuwa haijulikani kamwe katika kijiji chao. Bahati alikuwa na kibarua katika kampuni moja ya utangazaji habari wakati ambapo mkewe Fifi alikuwa anaajiriwa katika duka la mavazi mjini. Ingawa wafanyakazi hawa walikuwa wanapata mshahara kila mwezi, mahitaji ya kimaisha yalikuwa yanaendelea kuwasumbua. Siku moja, bwana Bahati alijadiliana na mkewe juu ya njia mwafaka wangelipitia ili waridhike na masharti ya kimaisha. Makubaliano yao yaliichagua shughuli ya kutumia akili kama watu waliokuwa wasomi. Shughuli ya kuendeleza kazi za fasihi andishi ilipewa alama asilimia tisini na tano. Baada ya mpango kuiva, Bahati na mkewe waliunda kampuni yenye jina la Maisha ni Bora Ltd. Waliwaajiri wataalamu wa kutunga hadithi fupi, riwaya, tamthila pamoja na mashairi. Miezi minane baadaye, matunda ya kampuni yalikuwa yameanza kujitokeza. Matini za riwaya, hadithi fupi pamoja na mashairi yalichapwa na kununuliwa kwa wingi wakati ambapo kundi la wachezaji wa tamthilia lilikuwa likizunguka sehemu mbalimbali za nchi. Raia walifurahia sana maadili kutoka tanzu hizo kwa sababu zilichangia sana kuijenga upya jamii yao.

Baadhi ya mada zilizokuwa zimegusiwa mno katika kazi hizo za fasihi andishi ni kama vile umoja wa jamii, mapenzi, uhifadhi wa utamaduni, amani na utulivu katika jamii pamoja na vita dhidi ya umaskini. Mafanikio kutoka kazi hizi zote yaliiwezesha familia hii kununua magari ya kazi na ya ziara, kujenga nyumba ya kisasa, kuishi kwa raha na kuwalipia karo watoto wao katika shule siyo tu za humu Rwanda bali pia Marekani na Ulaya. Leo, familia ya bwana Bahati na mkewe Fifi imekuwa kielelezo kwa wasomi wote kuwa akili ni nywele, kila mtu ana zake.

## KAZI 2

***Soma kifungu cha habari hapa juu na kujibu maswali ya ufahamu yafuatayo*:**

1. Kutokana na kifungu cha habari hapa juu, watu hudai kuwa utajiri unatoka wapi?
2. Eleza jinsi familia ya Bahati na Fifi ilivyo mwanzoni na mwishoni.
3. Je, kichwa cha habari hii kinaoana sana na yaliyomo? Tetea msimamo wako.
4. Ni kitu gani kilichowawezesha bwana Bahati na mkewe kujiepusha na matatizo ya kimaisha na kufika kwenye upeo wa utajiri?
5. Utajiri wa familia ya bwana Bahati na mkewe Fifi umeelezewa vipi?

## KAZI 3

***Soma kauli zifuatazo na kutoa jibu kwa kuchagua Kweli au sikweli. Tetea msimamo wako.***

1. Huwezi kuwa tajiri bila kutumia njia zisizo rasmi.
2. Utajiri unaweza kufikiwa kutoka kuzimuni.
3. Ujishughulishaji wa kazi za fasihi andishi huweza kumfanya mtu tajiri.
4. Wachezaji mashuhuri wa tamthilia huwa na uwezo wa kuibadilisha jamii kimila na kiuchumi.
5. Baadhi ya tanzu za fasihi andishi kuna hadithi fupi, riwaya, tamthilia pamoja na mashairi yaliyoandikwa.

## 15.2. Matumizi ya msamiati

**KAZI 4**

***Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.***

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) akili | iv) kurithi | vii) kudhulumu | x) matini |
| ii) duni | v) fukara | viii) kudai | xi) kushuku |
| iii) hila | vi) kusambaa | ix) yatima | |

**KAZI 5**

***Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati ufuatao: tajiri, kongwe, dai, kuajiri, thamani***

a) Inahakikishwa kuwa fasihi simulizi ni fasihi...................ukiilinganisha na fasihi andishi.

b) ..............hutajirika zaidi.

c) Usafi ni kitu chenye ...................mithili ya dhahabu.

d) Kusema kuwa utajiri ni urithi kutoka kizazi kimoja kwa kingine ni .................lisilo na misingi ya kisayansi.

e) Kazi za fasihi andishi huiendeleza jamii kwa ........................wafanyakazi mbalimbali.

## 15.3. Sarufi: Aina za tungo katika Kiswahili

### Maelezo ya kuzingatia

Kimuundo na kimaana, tungo hujigawa katika aina tatu kuu kama ifuatavyo:

1. **Tungo Sahili** : Ni sentensi zenye kishazi kimoja na huwakilisha wazo moja tu.

**Mfano:**

Tumeelewa faida za fasihi andishi.

Wanaume na wanawake huwa na haki sawa.

2. **Tungo ambatano**: Ni sentensi zenye zaidi ya kishazi huru kimoja na huwakilisha mawazo mawili au zaidi. Aghalabu sentensi hizi hutumia viunganishi (U) au alama za uakifishaji kama vile kituo (.) na nukta-nusu (;) ili kubainisha wazo moja toka jingine.

**Mifano:**

Tulipanda miti kwa ajili ya kupigana dhidi ya mporomoko wa ardhi. Ardhi yetu iliporomoka.

- Ingawa tulipanda miti kwa ajili ya kupigana dhidi ya mporomoko wa ardhi, ardhi yetu iliporomoka.

Bwana Bahati na mkewe Fifi waliunda kampuni ya uandishi wa riwaya. Bwana Bahati na mkewe Fifi waliwaajiri wafanyakazi wengi.

- Bwana Bahati na mkewe Fifi waliunda kampuni ya uandishi wa riwaya na kuwaajiri wafanyakazi wengi.

Familia ya Bwana Bahati na mkewe Fifi ilijitafutia ajira. Familia ya Bwana Bahati na mkewe Fifi ilitajirika.

- Familia ya Bwana Bahati na mkewe Fifi ilijitafutia ajira ikatajirika.

3. **Tungo Changamano:** Ni sentensi zinazoundwa kwa kuunganisha kishazi huru pamoja na kishazi tegemezi au sentensi mbili kwa kutumia o-rejeshi ili kuleta zaidi ya wazo moja.

**Mifano:**

- Tumepata maelezo ya kutosha kuhusu elimu ya usanifishaji. Tulikuwa tunaomba maelezo hayo toka mwezi uliopita.

- Tumepata maelezo ya kutosha kuhusu elimu ya usanifishaji ambayo tulikuwa tunayaomba toka mwezi uliopita.

- Shirika jipya lilitunga tamthilia hii. Ni tamthilia inayovutia sana.

- Shirika jipya ndilo lililotunga tamthilia hii inayovutia sana.

## KAZI 6

***Soma sentensi zifuatazo na kuzitofautisha kwa kuzingatia muundo wake pamoja na jinsi wazo au mawazo yalivyojitokeza***

i) Kazi za fasihi andishi hutajirisha kiuchumi.

ii) Tulitunga tamthilia na kuziigiza jukwaani.

iii) Waliuliza maswali kuhusu magonjwa ya zinaa ambayo yalizusha kelele nyingi darasani.

## KAZI 7

**Bainisha tungo zifuatazo kwa kutegemea aina zake:**

a) Hili ni jibu ambalo lilikuwa likisubiriwa na wengi.
b) Tulisoma kwa bidii na kushinda mtihani wa taifa.
c) Walifurahia matokeo ya kazi yao.
d) Soma kwa sauti!
e) Wao ndio waliopatiwa kombe la uhifadhi wa mazingira.
f) Bahati na mkewe walishirikiana katika kazi zote na kufaidika.

## KAZI 8

***Badilisha tungo zifuatazo katika tungo ambatano au tungo changamano.***

a) Walifanya matayarisho mengi ya kushiriki kwenye mapambano. Walipoteza ovyo kombe la almasi.
b) Waliwaandikia rafiki zao barua. Barua hizi ziliwafurahisha rafiki zao.
c) Yeye ni daktari mashuhuri. Alizawadiwa na Wizara ya Afya.

## 15.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Tanzu za Fasihi Andishi

## KAZI 9

***Taja na kujadili tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili***

**Zingatia yafuatayo**

Kuna tanzu nne kuu za fasihi andishi ambazo ni zifuatazo:

1. Hadithi fupi
2. Riwaya
3. Tamthilia
4. Mashairi yaliyoandikwa

**A. HADITHI FUPI**

Hadithi Fupi ni aina ya kazi andishi ambayo huwa fupi; na huangazia wazo moja kwa kurejelea kisa kimoja.

Hadithi fupi huwa na wahusika wachache na huchukua muda mfupi. Masuala mbalimbali huzingatiwa katika hadithi fupi kama vile masuala ya kijamii, kisiasa, kidini, kielimu, kiutamaduni, kiuchumi, n.k.

**Mfano:** Hadithi fupi za Alley Yusufu Mugenzi

Mifano mingine ya hadithi fupi za Kiswahili:

- Kachukua Hatua Nyingine
- Mayai Waziri wa Maradhi
- Siku ya Mganga
- Ngome ya Nafsi

**B. RIWAYA**

Riwaya ni kazi ya fasihi andishi ambayo huwa ndefu na aghalabu riwaya moja hujaza kitabu kizima. Riwaya huwa na wahusika wengi na huangazia mawazo kadhaa. Aidha, riwaya hufanyika katika mazingira mbalimbali na aghalabu huchukua muda mrefu ikilinganishwa na hadithi fupi. Kazi hii huhusisha binadamu,wanyama ama vitu vingine vinavyopewa uhai kama vile mizimu.

Kunazo aina nyingi za Riwaya katika Fasihi Andishi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

**Riwaya sahili:** Ni aina ya riwaya ambayo visa vyake husimuliwa moja kwa moja na huwa rahisi kueleweka.

**Riwaya changamano**: Hii ni riwaya ambayo huhitaji kusomwa kwa makini ili kueleweka. Aghalabu huwa na maudhui mengi na wahusika wengi ambao wanachangia katika tatizo kuu katika riwaya hiyo. Hujengwa kwa taharuki ili kuwavutia hadhira kutazamia jinsi tatizo kuu litakavyotatuliwa. Hutumia mbinu za taharuki na visengere nyuma/mbele.

**Riwaya ya kibarua:** Ni riwaya ambayo hutumia muundo wa barua kuwasilisha ujumbe wake.

**Riwaya kiambo:** Ni riwaya ambayo huhusisha masuala ya kawaida katika jamii.

**Mfano wa riwaya:**

*Adili na Nduguze*

*Utengano*

*Siku Njema*

*Mwisho wa Kosa*

*Kiu*

**Tofauti kati ya hadithi fupi na riwaya**

| | HADITHI FUPI | RIWAYA |
|---|---|---|
| 1. | Huwa fupi - hadithi fupi nyingi huhitaji kuunganishwa pamoja kuunda kitabu kimoja. | Huwa ndefu - huunda kitabu kizima. |
| 2. | Huwa na wahusika wachache. | Huwa na wahusika wengi. |
| 3. | Hurejelea wazo au kisa kimoja tu. | Huwa na visa vingi na mawazo mengi yanayojenga wazo kuu. |
| 4. | Husimuliwa kwa lugha ya moja kwa moja. | Masimulizi yake yanaweza kuchanganya visengere nyuma na visengere mbele. |
| 5. | Huwa na muundo rahisi kueleweka. | Aghalabu huwa vigumu kueleweka. |
| 6. | Hufanyika katika mandhari/ mazingira moja tu au chache. | Visa mbalimbali hufanyika katika mandhari mbalimbali. |

## C. TAMTHILIA

Tamthilia ni sanaa ambayo huwasilisha mchezo wa kuigiza kwa njia ya maandishi. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, halafu hufuatiwa na maneno halisi yaliyotamkwa na mhusika huyo. Kwa maana nyingine,tamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani kwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

### Aina za jukwaa

Kuna aina mbili za jukwaa:

- Jukwaa la akilini kama hali ya kujiundia akilini k.v. mchezo unaoigizwa redioni.
- Jukwaa la hadharani, yaani mahali ambapo maonyesho ya tamthilia yanaigiziwa mbele ya watazamaji au wasikilizaji.

### Aina za tamthilia

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huwa na aina mbalimbali kulingana na dhamira kuu inayoendelezwa. Utaipata tamthilia ya mapenzi, ya kihistoria, ya kisiasa, ya kidini, ya kiuchumi, n.k. Tamthilia hizi zote huangukia baadhi ya makundi makuu yafuatayo:

### Tanzia

Ni aina ya tamthilia iliyojaa, huzuni ndani yake, mikasa, matokeo ya vifo na mateso makali. Mwisho wa tamthilia za aina hii huwa ni wa masikitiko, maanguko na hasara kubwa kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Wengine huita aina hii tamthilia simanzi au trejedia.

**Ramsa**

Tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, kejeli, maneno yaonyeshayo ujinga, n.k. Iwapo tamthilia hizi huwa na dhana ya uchekeshaji, lengo lake ni kukosoa jamii, watawala na tabia mbaya na watu binafsi. Aina hii huitwa tena Tamthilia cheshi au komedia.

**Tanzia – ramsa**

Tanzia – ramsa au simanzi – cheshi ni mchezo wenye sifa za ramsa, lakini ndani ya uchekeshaji wake na tanzia kama vile kifo cha mhusika mkuu au kuanguka kwa jamii. Pengine huitwa Trejikomedia.

**Mfano wa tamthilia**

*Hawala ya Fedha*

*Kifo Kisimani*

*Shamba la Wanyama*

*Mstahiki Meya*

## D. MASHAIRI YALIYOANDIKWA

Ushairi ni utungo wa kisanaa unaotumia maneno ya mkato na lugha yenye kuvutia (lugha teule na mpangilio fulani wa maneno badala ya kutumia lugha natharia) na ambayo yamepangwa kwa urari wa mizani na vina maalum. Ushairi unaweza kuwa kipera cha fasihi simulizi (nyimbo) na pia katika fasihi andishi kwa sababu mashairi yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya kukariri na pia kwa njia ya maandishi. Mashairi yanayoghaniwa badala ya kusomwa huitwa maghani.

Kuna aina kuu tatu za ushairi: Mashairi, Ngonjera, Tendi au Tenzi.

**Mashairi:**

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika na kuwasilisha ujumbe fulani. Mashairi hugawika katika makundi mawili: mashairi ya kimapokeo au mashairi arudhi na mashairi huru. Mashairi arudhi hutungwa kwa kufuata au kuzingatia sheria na kanuni au kaida za utunzi kama vile kuzingatia vina, idadi fulani ya mizani, mishororo na vipande vya mishororo. Kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti, mashairi huweza kugawika tena katika aina mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Tamonitha ni shairi lenye mshororo mmoja kwa kila ubeti.
2. Tathnia ni shairi lenye mishororo miwili kwa kila ubeti.
3. Tathlitha ni shairi lenye mishororo mitatu kwa kila ubeti.
4. Tarbia ni shairi lenye mishoro minne kwa kila ubeti.
5. Takhmisa ni shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti.
6. Tasdisa shairi lenye mishororo sita.

**Ngonjera:**

Ngonjera ni shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi.

**Tenzi**

Tenzi ni aina ya shairi ambayo ni mtungo mrefu wa kishairi unaoelezea habari au masuala mbalimbali kishairi. Utenzi huwa hauna vina vya kati katika mistari yake bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho wa ubeti.

Kuna mambo mengine muhimu kuhusu shairi. Mishororo ya shairi huwa na majina maalum.

Mwanzo huwa ni mshororo wa kwanza wa ubeti.

Mloto huwa ni mshororo wa pili wa ubeti.

Mlea huwa ni mshororo wa tatu wa ubeti

Kituo huwa ni mshororo wa mwisho wa ubeti.

Kuna aina mbili za vituo ambazo ni kituo kimalizio na kituo kibwagizo. Kituo kimalizio ni kituo ambacho hakirudiwi mwishoni mwa kila ubeti katika shairi. Kituo kibwagizo ni kituo kinachorudiwarudiwa mwishoni mwa kila ubeti.

Vipande au sehemu za mishororo ni zifuatazo:

**Ukwapi:** Ni kipande cha kwanza cha mshororo.

**Utao:** Ni kipande cha pili cha mshororo.

**Mwandamizi:** Ni kipande cha tatu cha mshororo.

**Dhima ya ushairi**

Kama mtungaji wa kazi nyingine za fasihi, mshairi huwa na madhumuni yafuatayo kwa jamii:

- Kuburudisha
- Kuhamasisha jamii
- Kukuza sanaa na ukwasi wa lugha
- Kuliwaza
- Kuelimisha
- Kuonya, kutahadharisha, kunasihi na kuelekeza
- Kupitisha ujumbe fulani
- Kusifia mtu au kitu
- Kukejeli au kukemea mambo yanayoenda kinyume na maadili ya jamii.

## 15.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 10**

***Sikiliza kipindi cha tamthilia Urunana kutoka Idhaa ya Kinyarwanda kutoka BBC au Indamutsa kutoka Radio Rwanda na kusimulia hadharani muhtasari wa tamthilia moja uliyoisikiliza.***

**KAZI 11**

***Fikiria tamthilia moja, riwaya au hadithi fupi ambayo ujumbe wake ulichangia kuijenga jamii ya Wanyarwanda. Wasilisha hoja zako darasani.***

## 15.6. Kuandika

**KAZI 12**

***Buni hadithi fupi yenye kichwa hiki "Mama wa kambo ni mama"***

**KAZI 13**

***Tunga shairi lenye beti nne kuhusu sifa za mpenzi wako.***

## Tathmini ya Mada ya Saba

1. Nini dhima ya fasihi andishi?
2. Toa tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi
3. Fasihi simulizi ni fasihi kongwe wakati ambapo fasihi andishi ni fasihi changa.Tetea kauli hii.
4. Kamilisha sentensi zifuatazo:

i) Kuna tanzu kuu ............za fasihi andishi ambazo ni zifuatazo: .............. ........................

ii) Tofauti iliyopo kati ya hadithi fupi nariwaya ni hii:.................................... .......................

iii) Aina kuu za tamthilia ni zifuatazo:............................................................

iv) Ushairi ni utungo.......................................................................................

v) Shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi huitwa........................

5. Bainisha aina za tungo kupitia sentensi zifuatazo:

a) Tutafurahi na kupiga mayowe na vigelegele.

b) Walimu na wanafunzi hupaswa kushirikiana.

c) Ingawa walijikinga dhidi ya mbu, watoto wa jirani yangu wameambukizwa ugonjwa wa malaria.

# MADA YA 8

# UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

## Uwezo mahususi

Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi andishi


**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kueleza uhakiki wa kazi za fasihi na umuhimu wake,
- Kubainisha vipengele muhimu katika uhakiki wa kazi za fasihi andishi,
- Kutofautisha fani na maudhui,
- Kuhakiki kazi za tanzu mbalimbali za fasihi andishi,
- Kutumia kwa ufasaha viambishi rejeshi katika ngeli za majina mbalimbali.

### Kidokezo

1. Tunapozungumzia uhakiki wa kazi za fasihi, unafahamu nini?
2. Nini umuhimu wa kuhakiki kazi za fasihi?
3. Unapohakiki kazi ya fasihi andishi ni mambo gani muhimu ya kuzingatia?

# SOMO LA 16: MAANA YA UHAKIKI NA DHIMA ZAKE




**KAZI 1**

***Umevutiwa na nini kwenye michoro hii?***

## 16.1. Kusoma na Ufahamu: Uhakiki kama Kazi ya Kitaalamu

Jinsi binadamu alivyo, na anavyomudu maisha yake ya kila siku, hutokana na maarifa ya kielimu aliyoyapata darasani au katika tajiriba yake ya kimaisha. Aidha, watu hujishughulisha na kazi mbalimbali. Kutokana na tofauti za kazi, utawakuta mafundi katika kazi za ujenzi wa nyumba, mabingwa katika uwanja wa kiteknolojia, wabobezi katika uchumi na wataalamu katika mambo ya fasihi au lugha kwa ujumla. Hali kadhalika, jinsi dereva anavyojiamini katika uendeshaji wa gari, ndivyo mhakiki wa kazi za fasihi anavyotawala katika uchambuzi au uchanganuzi wa kazi za kifasihi zilizotungwa na wasanii.

Jambo hili linatupeleka kwenye maswali yafuatayo: Je, uhakiki unamaanisha nini? Kwa nini uhakiki? Ni jukumu gani mhakiki wa kazi za kifasihi anastahili kutimiza?

Kimsingi, kazi ya fasihi andishi ni aina ya sanaa ambayo hutumia maneno yaliyoandikwa kupitisha ujumbe, au ni sanaa inayowasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na hadithi fupi, tamthiliya, riwaya pamoja na ushairi.

Kwa hiyo, msanii hatungi kwa kutunga tu ila huongozwa na kutawaliwa na misingi ya kisanii katika ufundi wake. Katika mwelekeo huu, mhakiki hustahili kushiriki katika uchunguzi wa kazi ya msanii iliyotolewa ili kuichunguza au kuitathmini. Kwa hivyo, uhakiki ni kitendo cha kutathimini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Hali kadhalika, uhakiki wa kazi za fasihi ni kitendo cha kuchambua, kutathmini na kuainisha kazi ya fasihi ili kuona ubora na udhaifu wa kazi hiyo kwa kutumia kaida au vigezo husika vya fani na maudhui.

Kutokana na maelezo haya, inaeleweka wazi kuwa mhakiki wa kazi za fasihi bila shaka huwa ni mtaalamu au mwerevu katika uwanja wa kifasihi ambaye huwa na uwezo au stadi za kuzisoma, kuzitafakari, na kuzitolea tathmini kazi za fasihi kwa kujiegemeza katika mwelekeo wa kaida maalum zinazotakiwa kuzingatiwa katika utunzi wa kazi hizo.

Hivyo basi hatuna budi kukubali kuwa mhakiki wa kazi za fasihi huwa na jukumu au nafasi kubwa katika kazi za fasihi kama ifuatavyo:

Kwanza, mhakaki ndiye anayefafanua kazi ya fasihi ili hadhira iweze kuelewa vizuri kazi hiyo. Vilevile mhakiki huwaonyesha watunzi au wasanii wa kifasihi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hayo mhakiki huwawezesha watunzi kutoa kazi bora zaidi.

Pengine, inambidi mhakiki huyo awe na habari kamili juu ya mwandishi au msanii wa kazi inayohakikiwa. Maana yake, inambidi mhakiki kuelewa hali pamoja na mazingira aliyokuwemo msanii kama kielelezo cha hisia zake au hoja zake. Hivi mhakiki hufanikiwa kutambua sababu za hisia au dhamira zilizoendelezwa na msanii katika kazi yake.

Hali kadhalika, mhakiki hutafakari kikamilifu kazi ya msanii na kuichambua kimawazo au kimalengo kwa kudhihirisha au kutambua maudhui pamoja na dhamira kuu au ndogondogo ambazo ni kiini cha kazi kamili ya msanii. Ili kulikabili jukumu hili, mhakiki hutoa majibu kwa maswali yafuatayo:

Msanii anatufahamisha nini? Kazi ya msanii inamlenga nani? Anazungumzia nini na ni suluhisho gani analotutolea kwa shida alizozitaja? Mwandishi ametunga katika kipindi gani cha historia na katika mazingira gani?

Mwisho, mhakiki huwa na jukumu la kurahisisha mawasiliano au kiungo kati ya hadhira na mtunzi. Jukumu hili hujidhihirisha kwa njia ya uchunguzi wa jinsi msanii alivyojenga sanaa yake ili ujumbe wake uwafikie walengwa husika, yaani uhakiki wa lugha iliyotumiwa na msanii pamoja na jinsi alivyowajenga wahusika katika kazi yake ya kifasihi. Kwa upande mwingine, uhakiki wa kazi mbalimbali za kifasihi humsaidia msomaji wa kazi husika ya kifasihi kuielewa au kupata mwangaza fulani juu ya kazi husika aisomayo.

## KAZI 2 a.

**Jibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Kifungu cha habari kinazungumzia nini?
2. Uhakiki wa kazi za fasihi ni nini?
3. Jadili majukumu ya mhakiki wa kazi za fasihi.
4. Zungumzia umuhimu wa kuhakiki kazi za fasihi.

## KAZI 2 b.

**Chagua jibu lililo sahihi kuliko mengine**

1. ……………ni uchambuzi wa kina wa kazi za fasihi.
   a) Maudhui
   b) Fani
   c) Fasihi
   d) Uhakiki
2. Kitendo cha uhakiki huongozwa na:
   a) Kaida
   b) Maudhui
   c) Fani
   d) Hisia
3. Mtu anayefanya kazi ya uhakiki huitwa
   a) Mwandishi
   b) Mfasiri
   c) Mkalimani
   d) Mhakiki

4. Yafuatayo ni mambo yanayofanyika katika uhakiki, isipokuwa:
a) Kutoa maoni
b) Kuainisha
c) Kutathmini
d) Kutafuta makosa

5. Uhakiki haufanywi katika ombwe, kwa sababu:
a) Hufuata hisia
b) Hauna kanuni
c) Hufuata kanuni
d) Hauna kanuni maalum

## 16.2. Matumizi ya Msamiati

**KAZI 3**

***Kwa kutumia kamusi ya Kiswahili sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.***

i) Tajiriba
ii) Ajira
iii) Muktadha
iv) Kaida
v) mtaalamu

**KAZI 4**

**Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati unaofaa kutoka kifungu cha habari**

i) .............la mhakiki ni kutathimini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu.
ii) Mhakiki hufafanua kazi ya fasihi ili.................... iweze kuielewa vizuri kazi hiyo.
iii) Kazi ya fasihi andishi ni sanaa inayo........................... ujumbe kwa njia ya maandishi.

## 16.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Rejeshi – ye -

**KAZI 5**

***Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia jinsi kiambishi rejeshi – ye - kinavyotumiwa***

i) Mtu aliyeshiriki katika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi nchini Rwanda amekamatwa na kupelekwa mahakamani.

ii) Mwanafunzi ambaye hufanya bidii hushinda mitihani bila tatitizo.

iii) Mbwa ni mnyama alindaye nyumba za watu.

iv) Binadamu ndiye kiumbe mbaya kuliko wanyama.

### Maelezo muhimu ya kuzingatia

Kiambishi rejeshi –ye- ni kiambishi kinachotumika katika tungo kwa kurejelea mawazo, nomino au mambo yaliyokwisha tajwa au yanayojulikana. Kiambishi hiki hujihusisha tu na majina ya ngeli ya A-WA- katika umoja, yaani majina ya watu, Mwenyezi Mungu, pamoja na wanyama. Matumizi ya kiambishi rejeshi – ye – hutumiwa kama ifuatavyo:

- Katikati ya kiambishi nafsi cha kitenzi na mzizi wa kitenzi.

**Mfano:** Ali**ye**shiriki

- Kwenye mzizi wa amba- na ndi-

**Mfano:** Mwanafunzi amba**ye**

Binadamu ndiye

- Mwishoni mwa kitenzi

**Mfano:** Mnyama alinda**ye**

**Tanbihi**: Kiambishi rejeshi –ye- hugeuka – o - katika wingi.

**Mfano:**

i) Watu wali**o**shiriki katika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi nchini Rwanda wamekamatwa na kupelekwa mahakamani.

ii) Wanafunzi amba**o** hufanya bidii hushinda mitihani bila tatitizo.

iii) Mbwa ni wanyama walinda**o** nyumba za watu.

## KAZI 6

***Tumia kiambishi rejeshi –ye- au –o- mwishoni mwa kitenzi***

a) Mzazi ambaye anatoa malezi bora atazawadiwa.

b) Wasanii wanaojishughulisha na kazi za fasihi hutoa mchango mkubwa kwa ujenzi wa jamii.

c) Mfugo ambaye anatakiwa sana katika harakati za kupigana dhidi ya ufukara ni ng'ombe.

## KAZI 7

***Tumia kiambishi rejeshi katikati ya kiambishi nafsi cha kitenzi na mzizi wa kitenzi.***

a) Mbu ni mdudu ambaye anahatarisha maisha ya binadamu kwa kumwambukiza ugonjwa wa malaria.

b) Kuku wachinjwao kila siku hawahesabiki.

c) Watu ambao hutenda mema huishi kwa utulivu.

## 16.4. Matumizi ya Lugha: Dhima za Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi na Nafasi ya Mhakiki

## KAZI 8

***Jadili umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi andishi pamoja na nafasi ya mhakiki***

### MAELEZO MUHIMU YA KUZINGATIA

### DHIMA ZA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

Uhakiki ni kazi ambayo ina mchango mkubwa sana katika kazi za fasihi. Kwa msingi huo uhakiki una dhima zifuatazo:

- Husaidia wasomaji kuilewa kazi ya fasihi kwa urahisi:

Watunzi wa kazi za fasihi hutofautiana katika matumizi ya lugha na taswira, hivyo mhakiki anapofanya kazi ya uhakiki anamsaidia msomaji kuelewa vipengele hivi kwa kuvifafanua kwa lugha rahisi.

- Husaidia ukuaji wa kazi za fasihi:

Mhakiki anapoonyesha ubora na udhaifu wa kazi ya mtunzi fulani, watunzi wengine pia watafunguka kifikra na kutunga kazi iliyobora zaidi.

- Hukuza uelewa wa mhakiki:

Kwa kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi, mhakiki hujiongezea maarifa ya lugha pamoja na mambo yanayotokea katika jamii.

**NAFASI YA MHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI**

Mhahiki kama mtaalamu wa kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum, huwa na nafasi kubwa katika kazi za fasihi. Mhakiki ndiye anayefafanua kazi ya fasihi ili hadhira iweze kumwelewa vizuri mtunzi wa kazi hiyo. Kwa hiyo, hapa mhakiki anasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya hadhira na mtunzi. Vilevile mtunzi huwaonyesha watunzi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hivyo, huwawezesha watunzi kufanya kazi bora zaidi.

## 16.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 9**


***Jadiliana na mwenzako au wenzako stadi angalau 10 anazostahili mhakiki kuwa nazo ili kuhakiki kazi fulani ya fasihi andishi***

## 16.6. Kuandika

**KAZI 10**

***Buni kifungu cha habari chenye aya angalau tatu kwa kutetea kauli hii: "Mhakiki ni sawa na refarii wa kabumbu uwanjani."***

# SOMO LA 17: TARATIBU ZA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI




**KAZI 1**

***Mchoro huu unaibua nini katika fikra zako?***

## 17.1. Kusoma na Ufahamu: Uhakiki wa Fani na Maudhui

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali ya ufahamu hapo chini**

Wahenga walisema kuwa maneno huwa na utamu zaidi yanaporudiwa. Kwa hiyo, hatuna budi kukumbusha kuwa uhakiki ni kitendo cha kuchambua, kutathmini na kuainisha kazi ya fasihi ili kuona ubora na udhaifu wa kazi hiyo kwa kutumia kaida husika. Ili kazi yake itimizwe kwa hali mwafaka, mhakiki anastahili kupitia hatua tatu zifuatazo:

Kwanza ni kuisoma kazi ya fasihi; hapa mhakiki anatakiwa kuisoma kazi husika ya fasihi kwa kina na kuielewa vizuri.

Pili ni kuainisha na kuchambua mambo muhimu yanayojitokeza katika kazi hiyo kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui.

Tatu ni kutoa tathmini au kuelezea ubora na udhaifu wa kazi inayohusika. Je, tunapozungumzia vipengele vya fani na maudhui tunagusia nini?

Tuchukue mfano wa barua pepe ambayo imeandikwa ovyo ovyo bila kuzingatia mitindo ya kisarufi, aya pamoja na alama za vituo. Mambo haya yote huchukuliwa kama umbo la barua pepe hii. Kama umbo hili halivutii basi msomaji hatakuwa na nia ya kuisoma barua pepe hii. Mfano wa pili ni wa nyumba inayong'aa kwa rangi na mapambo mbalimbali yaliyoko kwenye nyumba hiyo. Atakayeiona nyumba hii, atakuwa ameingiwa na udadisi wa kuingia ndani kwa sababu uzuri wake umemvutia mtazamaji. Umbo hilo ndilo linalolinganishwa na fani katika kazi za kifasihi.

Hivyo, baada ya kuvutiwa na umbo la barua pepe, hamu au hiari ya kusoma ujumbe unaowasilishwa ndani yake itaongezeka. Ujumbe huo utatiliwa maanani na kupokewa kwa urahisi. Vilevile, mtazamaji aliyeridhika na umbo la nyumba hatasita kuingia ndani ili ashuhudie jinsi vifaa vya nyumbani vilivyo kama vile mpangilio wake, vyumba, milango, n.k. Atatafakari yeye mwenyewe ujumbe kuhusu uwezo mkubwa wa fundi aliyeijenga na kuipamba nyumba hiyo. Ujumbe huu au yaliyomo hufananishwa wazi na maudhui katika kazi za fasihi.

Mifano ni wa msichana mrembo ambaye maumbile yake ni mithili ya malkia. Ah! Utapatwa na bumbwazi utakapomtathmini kimwenendo au kitabia. Mfano huu ungelikwenda sambamba na mtu ambaye unamkuta amevaa nguo za bei ghali iwapo mwili wake unatoa harufu mbaya; maana yake mwezi mzima umemalizika bila mtu huyo kuoga.

Kwa hiyo, kazi ya msanii wa fasihi yoyote huwekwa mikononi mwa mhakiki ili kuitathmini na kutoa maoni yake kuhusu kufanikiwa au kutofanikiwa kwa msanii. Kwa upande mmoja, kufaulu au kutofaulu kwa msanii hutokana na jinsi umbo au fani ya kazi yake inavyowavutia walengwa wake.

Kwa upande mwingine, kufaulu au kutofaulu kwa msanii huelezwa na jinsi ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa ulivyopangwa toka mwanzoni hadi mwishoni.

## KAZI 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Katika uhakiki wake wa kazi za fasihi, mhakiki hustahili kupiga hatua gani?
2. Mwandishi ameelezaje fani na maudhui?
3. Mafanikio ya kazi ya msanii hutokana na nini ?
4. Kutofaulu kwa msanii husababishwa na nini?

## 17.2. Matumizi ya Msamiati

## KAZI 3

***Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia mojawapo ya msamiati huu: wahenga, udhaifu, vipengele, barua pepe, kung'aa, kuvutia, pambo, kuridhika, bei ghali, kusita. Tafadhali husika na mabadiliko ya kisarufi yanayoweza kujitokeza.***

i) Katika mtindo mpya wa mawasiliano ya kiteknolojia, ......................... husaidia kuwasilisha ujumbe kwa haraka na urahisi kupitia simu ya mkononi au tarakilishi /kompyuta.

ii) Baadhi ya ......................au tanzu za fasihi andishi kuna hadithi fupi, riwaya, tamthilia pamoja na mashairi yaliyoandikwa.

iii) Inasemekana kwamba methali, nahau au vitendawili ni urithi tulioachiwa na....................................

iv) Mavazi yake yalikuwa yana..............................kama dhahabu.

v) Umoja ni nguvu utengano ni ........................................................

vi) Ukiwa na swali lolote usi....................kuuliza.

vii) Ghorofa ni nyumba yenye...........................

viii) Almasi, dhahabu na mawe mengine ya thamani hutumiwa kama .......................

ix) Shairi hutumia lugha ya mkato na ya...............................

x) Asante sana! Maelezo yako yameni....................................

## 17.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi rejeshi – o – katika Majina ya Ngeli ya A-WA, LI-YA na KI-VI

### KAZI 4

***Soma sentensi zifuatazo. Bainisha kiambishi rejeshi kilichotumiwa na kueleza jinsi kilivyotumiwa.***

i) Watoto ndio watakaoendeleza jamii ya kesho.

ii) Kitabu kilichonunuliwa jana kimetusaidia sana.

iii) Jicho likupendalo hukuangalia kipekee.

**Maelezo muhimu ya kuzingatia**

Kiambishi rejeshi husika ni – o - . Kirejeshi hiki hujihusisha na ngeli za majina kama ifuatavyo:

- Katikati ya kiambishi nafsi cha kitenzi na mzizi wa kitenzi.
- Kwenye mzizi wa amba- na ndi -
- Mwishoni mwa kitenzi

**Mifano** mbalimbali kuhusu ngeli za majina husika.

**Ngeli ya majina** **Matumizi ya kirejeshi – o –**

**LI-YA- :** Swali ambalo litaulizwa na wengi ndilo litakalojadiliwa.

**zaidi –** Maswali ambayo yataulizwa na wengi ndiyo yatakayojadiliwa zaidi.

**KI-VI- :** Kikulacho kinguoni mwako – Vikulavyo vingoni mwako.

### KAZI 5

**Unganisha sentensi mbili kwa kutumia kirejeshi – o -**

i) Wanafunzi walifanya bidii. Wanafunzi hao wameshinda mtihani wa taifa.

ii) Mezani kuliwekwa vitabu. Mezani huko ni kuchafu.

iii) Vitambulisho viliibiwa. Vitambulisho hivyo vimerudishwa.

iv) Tabia ya uzembe ni mbaya. Inaangamiza maendeleo ya jamii.

v) Ukuta wa nyumba umeanguka. Ukuta huo umekuwa chanzo cha vifo vya watu.

## 17.4. Matumizi ya lugha: Mwongozo katika uhakiki wa kazi za fasihi andishi

**KAZI 6**

***Jadili kwa uundani mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa tunapohakiki:***

a) Hadithi fupi, riwaya
b) Tamthilia
c) Shairi

**MWELEKEO WA MAELEZO**

**i) UHAKIKI WA HADITHI FUPI NA RIWAYA**

Kwa kawaida, uhakiki wa kazi za fasihi andishi hutegemea FANI na MAUDHUI.

**A. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UHAKIKI WA FANI**

Kama sura ya nje ya hadithi fupi au riwaya, fani hufanyiwa uhakiki kwa kuzingatia vipengele fifuatavyo:

- Wahusika
- Muundo
- Lugha
- Mtindo
- Mandhari

**a) WAHUSIKA:** Ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi.

**Aina za wahusika:** Wahusika wa hadithi fupi au riwaya hujigawa katika makundi makuu mawili:

**Wahusika wakuu**: Mhusika mkuu ni mhusika mmoja au wawili ambao hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi fupi.

**Wahusika wadogo**: Ni aina ya wahusika muhimu sana ambao humsaidia mhusika mkuu kuipa hadithi au riwaya mwelekeo wa kisanaa na kimaudhui.

**Tabia za wahusika:** Kutokana na majukumu yao, wahusika huonyesha tabia za aina tatu:

**Wahusika bapa**: Ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki kitabia kutoka mwanzoni mpaka mwishoni mwa hadithi fupi.

**Wahusika duara**: Ni wahusika ambao wanabadilika kitabia kutokana na mabadiliko ya mazingira.

**Wahusika foili**: Ni wahusika wenye tabia zinazobadilika kinusu. Wako kati ya wahusika bapa na wahusika duara.

b) **MUUNDO:** Ni namna msanii anavyopanga visa vyake au fikra zake katika hadithi fupi, yaani mtiririko wa visa na matukio. Kinachozingatiwa hapa ni jinsi mwandishi alivyopanga kazi yake; mfano sura na sura, kisa na kisa au tukio na tukio.

c) **LUGHA:** Kipengele cha lugha ni muhimu sana katika fasihi kwani ndicho hutenganisha fasihi na sanaa nyinginezo. Matumizi ya lugha katika fasihi yapo ya aina mbalimbali: kuna tamathaili za semi, misemo, nahau, methali, lahaja za wahusika, uchaguzi wa msamiati, miundo ya sentensi.

**Mifano ya tamathali za semi:**

- **Tanakali za Sauti:** Ni mbinu ya kutumia maneno yanayoiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika.

**Mfano:** anguka pa!

- **Tashbiha**: Hii ni mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; 'kama', 'mithili ya', 'sawa na'.
- **Tashihisi**: Hii ni mbinu ya kupatia kitu kisicho hai sifa za kiumbe mwenye uhai (sifa za kibinadamu).
- **Takriri**: Ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani.
- **Ukinzani**: Ukinzani ni mbinu ya kusisitiza ujumbe kwa kuambatanisha maneno ya kinyume au yanayokinzana.
- **Sitiari**: Ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kutotumia viunganishi ambapo kitu kimoja hufanywa kuwa sawa kabisa na kitu kingine.
- **Taswira**: Ni matumizi ya lugha/maneno yanayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji.
- **Taashira**: Ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani. Jina au kitu fulani kinatumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa.
- **Majazi**: Majazi ni pale tabia za wahusika zinapoambatana na majina yao halisi.
- **Lakabu**: Ni mbinu ya mhusika kupewa/kubandikwa jina na wahusika wengine ama yeye mwenyewe kujibandika jina linalooana na tabia/sifa zake.

- **Chuku**: Ni kutumia maneno yaliyotiliwa chumvi ili kusisitiza ujumbe fulani au kusifia kitu, kutilia chumvi.

d) **MTINDO:** Mtindo ni namna ambavyo mwandishi huipa hadithi yake sura ya kifani na kimaudhui.

Mtindo ndio unaotofautisha wasanii. Katika mtindo tunachunguza sana matumizi ya lugha.

e) **MANDHARI:** Mandhari ni mazingira au mahali tukio la hadithi fupi lilipotokea. Kuna mandhari ya kubuni na mandhari ya kweli.

## B. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MAUDHUI

**Maudhui** ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi. Hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi fulani ya kifasihi. Mawazo na mafunzo haya hayazuki hivihivi tu. Kwa hiyo wakati wa kuyachambua na kuyajadili ni lazima yahusishwe na hali halisi ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi zilizopo katika jamii, hali hizi ndizo zilimzaa, zilimlea na kumkuza msanii.

Wakati wa kuchambua kazi za kifasihi mhakiki ni lazima ajiulize amaswali yafuatayo:

- Je, msanii anatueleza nini?
- Je, msanii kamtungia mtu wa tabaka gani?
- Anamtukuza nani?
- Anambeza nani?
- Msanii anataka tuchukue hatua gani katika utatuzi wa matatizo ayashughulikiayo katika kazi yake?

Maudhui hujengwa na vipengele muhimu vifuatavyo: **Dhamira, ujumbe, migogoro, msimamo wa msanii pamoja na falsafa yake.**

a) **Dhamira:** Ni mawazo yanayojitokeza sana katika kazi ya fasihi. Ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake.

Kifasihi kuna aina mbili za dhamira yaani dhamira kuu na dhamira ndogondogo

**Dhamira kuu** ni kiini cha kazi ya fasihi, ni wazo kuu.

**Dhamira ndogondogo** ni mawazo madogomadogo ambayo hujenga dhamira kuu.

b) **Migogoro:** Ni hali ya kutoelewana baina ya pande mbili yaani mtu na mtu, mtu na kikundi au mtu mwenyewe na nafsi yake. Migogoro ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi za fasihi. Migogoro inaweza kuwa kati ya wahusika, familia zao au matabaka yao. Migogoro hii inaweza kuwa ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kifalsafa, n.k.

c) **Ujumbe:** Ni funzo na maadili yaliyokusudiwa na mtunzi yaifikie jamii aliyoilenga kufikisha kazi yake ya fasihi.

d) **Falsafa:** Ni imani na mwelekeo wa mwandishi kuhusu maisha katika jamii.

e) **Msimamo wa msanii:** Msimamo wa msanii kuhusu masuala mbalilmbaili ya kijamii hubainishwa na mawazo, mafunzo, lengo na falsafa. Msimamo ndio uwezao kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaotunga kazi za fasihi zilizo na kiini na chimbuko moja. Kwa hiyo, msanii huweza kuchukua msimamo wa kimapinduzi au wa kiyakinifu kulingana na jinsi anavyoyazingatia maisha ya jamii inayozungumziwa.

## C. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA TAMTHILIA

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huweza kuhakikiwa jukwaani au kupitia maandishi.

### a) Uhakiki wa Kifani

***Wahusika***: Wahusika katika tamthilia huwa wengi pamoja na tabia zao mbalimbali.Tamthilia huwa na wahusika halisi ambao wanajitetea jukwaani kimatendo na kitabia wakati.

***Muundo***: Tamthilia huwa na sehemu tatu: Mwanzo, Katikati na Mwisho. Sehemu zake zinatazamiwa kuingiliana, kujengana na kukamilishana. Muundo katika tamthilia huangaliwa kwa kuzingatia idadi ya vitendo/ sehemu na idadi ya maonyesho.

***Mtindo***: Tamthilia huwa na mgawiko wazi wa matendo na matukio kwa mujibu wa sehemu na sura mbalimbali. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, halafu hufuatiwa na maneno halisi yaliyotamkwa na mhusika huyo.

***Lugha***: Tamthilia inatawaliwa na lugha ya mazungumzo katika majibizano au hata mazungumzo pweke. Ucheshi, porojo au mizaha, tamathali za usemi na onomatopia hutumiwa sana.

***Mandhari***: Kuna aina mbili za jukwaa: jukwaa halisi na jukwaa la akilini.

### b) Uhakiki wa Kimaudhui

Dhamira, ujumbe, migogoro, msimamo wa msanii pamoja na falsafa yake hushughulikiwa.

### D. UHAKIKI WA MASHAIRI

Sawa na kazi nyingine za fasihi, uhakiki wa mashairi huzingatia fani na maudhui.

#### a) Fani

Uhakiki wa fani ya shairi huzingatia muundo wake, yaani jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuangazia mizani, vina, mishororo n.k Aidha, ni muhimu kutaja aina na bahari za shairi zinazohusiana na kila sifa uliyoitaja.

***Idadi ya mishororo katika kila ubeti*** - Tumia idadi ya mishororo kubainisha aina ya shairi hilo.

**Kwa mfano**: Shairi lina mishororo minne katika kila ubeti, kwa hivyo ni Tarbia.

***Idadi ya mizani katika kila mshororo na katika kila kipande cha mshororo***.

**Kwa mfano**: Kila mshororo una mizani kumi na sita: nane katika utao na nane katika ukwapi.

***Idadi ya vipande katika kila mshororo*** - Taja ikiwa shairi lina kipande kimoja, viwili, vitatu au vinne kisha utaje bahari yake.

***Kituo, kiishio au kibwagizo*** - Ikiwa mstari wa mwisho umerudiwa rudiwa, basi shairi lina kibwagizo au kiitikio, la sivyo lina kiishio.

***Vina*** - Zingatia vina vya kati na vya mwisho kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kisha utaje ikiwa ni Mtiririko, Ukara au Ukaraguni.

***Matumizi ya lugha:*** Mtindo wa lugha hurejelea namna mbalimbali ambazo mshairi anatumia mbinu za lugha. Mshairi anaweza kutumia mbinu za lugha. kama vile: Tanakali za sauti, Tamathali za semi, n.k.

Katika mtindo wa lugha mhakiki huchunguza uhuru wa msanii, yaani mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani.

#### b) Maudhui

Uhakiki wa maudhui ya shairi huzingatia vipengele vikuu ambavyo ni **Dhamira** (Dhamira kuu na dhamira ndogondogo) pamoja na **Ujumbe.**

## 17.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 7**

Sikiliza tamthilia moja kutoka idhaa ya BBC kipindi Urunana au Indamutsa kutoka Radio Rwanda. Zungumzia wahusika wa tamthilia moja na kuwasilisha kazi yako hadharani.

## 17.6. Kuandika

**KAZI 8**

**Buni hadithi fupi yenye mojawapo ya vichwa vifuatavyo:**

"Wema hauozi"

" Chelewachelewa utamkuta mtoto si wako"

" Mbuzi wa maskini hazai"

"Asiyesikia la mkuu huvunjika guu"

"Baada ya dhiki faraja"

# SOMO LA 18: MFANO WA UHAKIKI WA TAMTHILIA

## 18.1. Kusoma na Ufahamu: Muhtasari wa Hawala ya Fedha

Familia ya Mzee Ibrahim CHANDE imetumiwa hawala ya fedha na mpwaye anayesomea mjini London. Thamani ya hawala hiyo ni shilingi elfu mbili. Ibrahim CHANDE anapaswa kuchukua kiasi cha shilingi mia tatu, kiasi kingine cha shilingi miatano ampatie mama yake Abdul, mia tano zinazobakia amwekee mpwa wake.

Hawala hii inaleta matumaini katika familia ya Ibrahim CHANDE. Familia nzima wanafikiri kwamba umaskini na njaa vimemalizika. Kwa kuwa wake zake CHANDE walitafuta mtu wa kuwasomea hawala ya fedha (kwa kuwa wao hawakujua kusoma wala kuandika), habari inazagaa mahali pote na majirani zote wanaarifiwa.

Watu kadha wa kadha wanakuja kukopa fedha na chakula kwenye familia hiyo. Wengine wanamfuata Ibrahim CHANDE kila anapokwenda ili awasaidie kutokana na fedha hizo.

Inambidi Ibrahim CHANDE aende kubadilisha hawala ya fedha posta. Anapofika anaombwa kuwa na kitambulisho lakini anakikosa. Hana kitambulisho chochote kile ila kadi ya chama isiyo na picha. Hivyo analazimika aende kwenye kituo cha polisi.

Anapofika, anaelezwa kuwa hawezi kuwa na kitambulisho kama hana picha. Ibrahim CHANDE anamwendea AMBROZI ambaye ni mpigapicha. Anampiga picha na kumwambia kurudi kesho yake baada ya kulipa shilingi thelathini. Kwa bahati mbaya, anaporudi AMBROZI huyu anamnyang'anya picha pamoja na pesa zake.

Siyo hayo tu, bali anamfanyia mabaya zaidi. MBAYE anajitolea kumsaidia CHANDE kutoa fedha kwenye posta. Kwa upande mwingine, dada yake CHANDE, yaani Mama Abdul, anakuja kudai pesa zake zilizoelezwa kwenye barua iliyokuja pamoja na hawala hiyo.

Mzee huyo inambidi auze hereni za dhahabu za mkewe ili dada yake asiende mikono mitupu. Ibrahim CHANDE hapumziki hata kidogo. Mwishowe, MBAYE aliyejidai kumsaidia anamwambia kuwa fedha alizichukua kutoka posta lakini akanyang'anywa na wezi akiwa njiani.

Matumaini yote ya Ibrahim CHANDE pamoja na wake zake yakafifia. Amne mke wake wa pili akaamua kwenda zake na Mama Dogo, mke wake wa kwanza akaenda kijijini kulima shamba.

## KAZI 1

**Maswali ya Ufahamu**

1. Kifungu cha habari kinazungumzia nini?
2. Ni wahusika gani wanaozungumziwa?
3. Hawala ya fedha iliyotumwa kutoka mjini Landon ilikuwa na shabaha gani?
4. Ni matatizo yapi yaliyokuwa vikwazo dhidi ya mafanikio ya Ibrahim Chande?
5. Tamaa mbele mauti nyuma. Husisha methali hii na kisa cha familia ya mzee Ibrahim Chande.

## 18.2. Matumizi ya Msamiati

### KAZI 2

***Jaza sentensi hizi kwa kutumia msamiati ufuatao: hawala ya fedha, mpwa, kuzagaa, kuarifiwa, kituo chapolisi, kunyang'anya, herini, mikonomitupu, kwenda zake. Husika na mabadiliko ya kisarufi kwenye vitenzi.***

a) Baada ya kuibiwa pesa zake zote, Ibrahimu Chande alirudi nyumbani...................................

b) Daktari alimdunga mgonjwa sindano na kumwambia,"............................. ukapumzike!"

c) ...................ni cheti kitumiwacho katika benki kuidhinisha kupewa pesa kwa mhusika aliyebainishwa na karani wa benki.

d) Alipofikishwa kwenye ............................jamaa alishitakiwa kwa...........................raia mali zao.

e) ...........................ni aina ya pambo la wanawake linalovaliwa masikioni.

f) Mtoto wa dadako huitwa.............................

g) Kabla ya .......................tarehe ya mtihani wa taifa wanafunzi wote walikuwa na udadisi sana.

h) Habari ya ushindi wa timu yao ilipo .............................nchini kote mashabiki walifurahi kwa kupiga shangwe na vigelegele.

## 18.3. Sarufi: Matumizi ya kirejeshi – o – katika majina ya ngeli ya U-I na U-ZI

### KAZI 3

***Soma sentensi zifuatazo. Bainisha kiambishi rejeshi kilichotumiwa na kueleza jinsi kilivyotumiwa.***

a) Miti ipandwayo karibu na nyumba huingiza hewa nzuri.

b) Kurasa ambazo zimetajwa ndizo zitakazokubaliwa.

**Maelezo muhimu ya kuzingatia**

Kiambishi rejeshi – o – kimehusishwa na majina ya ngeli za majina ya U-I na U-ZI. Kimetumiwa kama ifuatavyo:

- Katikati ya kiambishi nafsi cha kitenzi na mzizi wa kitenzi.
- Kwenye mzizi wa amba- na ndi-
- Mwishoni wa kitenzi

Mifano mbalimbali kuhusu ngeli za majina husika

**U-I- :** Mti ulioanguka umefunga njia – Miti iliyonguka imefunga njia.

Mti ulioanguka ndio uliofunga njia – Miti iliyoanguka ndiyo iliyofunga njia.

**U-ZI- :** Tumenunua uzi unaoonekana vizuri - Tumenunua nyuzi zinazoonekana vizuri.

**KAZI 4**

**Weka sentensi zifuatazo katika umoja au wingi**

i) Mwitu uliotembelewa ndio uliopatikana na wanyama kama vile chui na sokwe.

ii) Mlo upendwao ni ule unaohusika na mboga pamoja matunda.

iii) Miiko itakayopigwa marufuku katika jamii itaelezwa vilivyo.

iv) Funguo zinazotumiwa benkini huhifadhiwa kwa utaratibu.

## 18.4. Matumizi ya lugha: Uhakiki wa Tamthilia

**KAZI 5**

***Soma tamthilia ya Amandina Lihamba, Hawala ya Fedha na kuhakiki fani na maudhui yake.***

**MWELEKEO MUHIMU**

**UHAKIKI WA FANI**

1. **Wahusika na tabia zao**

**a) Wahusika wakuu**

Ibrahim CHANDE ndiye mhusika mkuu katika tamthiliya "Hawala ya fedha". Ana wake wawili: MAMA DOGO na AMNE. Habadiliki kitabia tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo, yeye ni mhusika bapa. Ubapa wake unadhihirishwa na ujinga wake anaokumbana nao katika habari yote. Mhusika huyu hajui kusoma wala kuandika. Isitoshe, hataki pia wake zake wawe na kisomo (uk. 4). Kwa kuwa inaruhusiwa katika dini ya Uislam, Ibrahim CHANDE ana wake wawili. Katika usemi wake wote kuna rejesta ya dini. Pengine anaonekana akitoa sadaka kwa maskini, wengine anakataa kuwapa.

Isipokuwa ujinga wake wa kutojua kusoma na kuandika, mzee huyu anaonyesha moyo wa kusikiliza shida za watu wengine hasa hasa wale wanaotaka msaada kutoka kwake.

**b) Wahusika wadogowadogo au wasaidizi**

***i) Mama Dogo***: Huyu ni mke wa kwanza wa Ibrahim CHANDE. Yeye na Amne ni wake wenza. Hali yao ya uke wenza haiwatenganishi wala kuwafanya wachukiane. Wanaonyesha ushirikiano tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo. Mama Dogo anaonyesha busara katika maneno yake. Mfano bayana ni usemi wake (uk. 41), pale ambapo anasema:"Afugaye punda lazima ampendelee mlimaji nyasi. " Katika usemi huu alitaka kuonyesha namna ambavyo hakuna mtu pekee anayeweza kujitosheleza. Kama mtu ana duka, anategemea wale ambao wanakuja kununua vitu katika duka hilo. Kwa sababu hiyo, mtu yeyote anapaswa kutodharau mwenzake. Kila wakati, Mama Dogo anaonekana akimtetea mumewe. Anaonekana akihangaishwa na usalama wa mumewe. Ili watu wasiendelee kumfuata Ibrahim CHANDE kwa ajili ya fedha, yeye alibuni kisingizio na kuwaambia watu kuwa mume amenyang'anywa fedha hizo (uk. 36-38). "Alipopata pesa watu wakamvamia (uk. 36)." "Majangili ndugu yakamvamia. Hata senti moja si yake. Mungu na Mtume, sasa pesa zimekwenda na heshima yetu pia imekwenda." Pengine Mama Dogo anaonyesha imani katika Mungu. Anaamini kuwa Mwenyezi Mungu hasahau waamini wake (uk. 1). Yeye ndiye anaweza kunusuru maisha ya mtu aliye hatarini (uk. 37).

***ii) AMNE***: Huyu ni mke wa pili wa Ibrahim CHANDE, yaani mke mwenza wa Mama Dogo. Tabia yake inaonyeshwa na ushirikiano anaokuwa nao kati yake na Mama Dogo mbele ya mume wao. Amne ana tamaa ya kuwa na kisomo. Anamwona mumewe kama mjinga wakati wowote anapomzuia kwenda kusoma. Mwishoni mwa mchezo, anaonyesha tabia ya kutoweza kuvumilia hali ya umaskini na njaa inayojitokeza katika familia yake. Alipokata tamaa ya kupata fedha zilizokuwa kwenye hawala iliyotumwa na Abdul, yeye aliamua kumtoroka mumewe.

***iii) Mbarka***: Ni mwenye duka. Kutokana na mazingira au hali mbalimbali, yeye anabadilika kitabia. Wakati alipojua kuwa Ibrahim alikuwa na hawala ya fedha, alifurahi sana na kumkopa mchele bila wasiwasi. Lakini alipopata habari kuwa pesa za Ibrahim zimeibiwa, alikasirika na kuanza kumdai kwa fadhaa. Mbarka anaonyesha tabia za uduara.

***iv) Issa:*** Huyu ni rafiki yake Ibrahim CHANDE. Urafiki wao unatokana na kuwa Issa anataka sehemu ya fedha alizonazo Ibrahim. Yeye anaonyesha tabia ya unyonyaji. Kila alipoongozana na Ibrahim wakienda mjini, alitaka Ibrahim amlipie basi. Unyonyaji wake unaonyeshwa pia na kunyang'anya watu akitumia ujanja (uk. 16). Yeye alikuwa anaganda kwenye Ibrahim kama rubu ama kupe wagandavyo kwenye ng'ombe.

***v) Ambrozi:*** Ni mwenye studio. Yeye anaonyesha tabia ya kunyanyasa watu duni. Yeye ni mjangili: anachukua pesa za watu kwa bure na kuwadhulumu ili wasije wakamdai fedha zao. Lugha anayoitumia ni ya matusi. Amandina Lihamba alitumia katika mchezo wake wahusika wengine wa aina mbalimbali ili kuonyesha hali halisi ya maisha. Mojawapo wa wahusika hao ni bapa vielelezo. Majina yao yanaonyesha shughuli au tabia zao. Hao ni kama mchuuzi, polisi, karani, maskini na kadhalika. Mhusika Abdul anasimamia kundi la watu waliopata kisomo. Yeye anajua umuhimu wa kusoma, ndiyo sababu alienda Landon. Vilevile, anajua wazazi wanahitaji msaada kutoka kwa watoto wao wakati wakiwa na uwezo. Kwa sababu hiyo, alitumia mjomba wake pamoja na mama yake hawala ya fedha.

**2. Mtindo**

Mtindo ni kiwango cha lugha alichotumia mwandishi katika Hawala ya fedha. Lugha inayotumiwa ni ya mazungumzo kwani kitabu hiki ni cha mchezo wa kuigiza, yaani tamthiliya. Vipengele vya lugha vilivyotumiwa na msanii ni tamathali za usemi, nahau, methali, misemo na rejesta. Pengine alitumia lugha ya kawaida, lugha inayoeleweka kwa wazungumzaji wengi wa lugha hiyo.

**Tamathali za usemi**

***a) Sitiari***: mifano, - Umaskini bila nyumba ni kifo - Madeni yatushika mpaka pwani - Ndiye shetani mkubwa. b) ***Tashibiha*** - Kukusanyika kama sisimizi, (uk. 3) - Asiponilipa haraka nitamganda kama rubu, (uk. 16)

***ii) Methali*** - Kutoa ni moyo si utajiri, (uk. 13) - Ulimi hauna mfupa: ulimi husema yote, yaani mazuri na mabaya. - Dawa ya moto ni moto: kwa tatizo nzito lazima kauli nzito.

***iii) Nahau*** - Kutia chumvi, - Chungu nzima, - Kukata kauli, - Kuwa na mkono mrefu (kuwa na huruma kwa kila mtu), - Kuwa na mkono wa birika (kinyume na kuwa na mkono mrefu), - Kukata tamaa, - Kufariki dunia/kuaga dunia.

**3. Muundo**

Msanii alitumia muundo wa moja kwa moja, yaani hakufanya mazungumzo yanayoweza kutatanisha msomaji. Visa na matukio muhimu vya kuzingatia katika Hawala ya fedha ni hivi vifuatavyo: - Taarifa inayomfikia Ibrahim CHANDE yenye ujumbe wa kupelekewa hawala ya fedha na kuwa postani. - Tumaini la kuwa hawala ya fedha ingemwokoa toka hali yake ya umaskini, - Kupanda kwa madeni, - Harakati za kubadilisha hawala hiyo, - Kupanda kwa tumaini la Ibrahim, - Matumaini ya kupata vitambulisho, - Kupatikana kwa fedha na kuibiwa kwake (Upeo wa habari), - Kushuka chini kwa tumaini. Msanii amefaulu kujenga kiini kimoja kutokana na mchanganyiko wa matukio mbalimbali.

### 4. Mandhari

Mandhari inayozungumziwa mchezoni ni halisi. Kama tulivyoelezwa na mwandishi, habari hii inatokea katika mji mdogo pwani mwa Afrika Mashariki.

## UHAKIKI WA MAUDHUI

Katika uchunguzi wa maudhui ya mchezo wa Hawala ya fedha tunachambua dhamira kuu pamoja na dhamira ndogo.

### Dhamira kuu

#### a) Unyonyaji na kuharibika kwa urasimu

Unyonyaji ni hali ya kutegemea wengine bila ya kufanya kazi; ni hali ya kuishi kwa jasho la mwingine. Katika tamthiliya Hawala ya fedha, unyonyaji unadhihirishwa na hasa hasa na majirani wa Ibrahim CHANDE wanaotaka awasaidie kwa kila hali baada ya kupata habari kuwa ametumiwa hawala ya fedha. Kuna wanaotaka awakopeshe mchele na wengine fedha kiasi kwamba angetimiza hoja zao angebaki mikono mitupu. Mhusika anayeonekana kuwa mnyonyaji kuliko wengine ni ISSA. Huyu anamsindikiza Ibrahim CHANDE katika harakati za kubadilisha hawala ya fedha ili apate fedha. Kila wanapoenda, ISSA anataka Ibrahim amlipie basi. Si hayo tu, anataka ampatie fedha za kutumia katika shughuli mbalimbali. Watu wengine wanaodhihirisha unyonyaji ni msichana aliyekutana na Ibrahim CHANDE akimuomba msaada kwa mara nyingi. Pengine ni Ambrozi, aliyemnyang'anya pesa zake alipoenda kujipigisha picha. Mhusika mwingine ni MBAYE aliyefaidi hawala isiyokuwa yake. Kwa upande mwingine kuna katika mchezo huu, hali ya kuharibika kwa urasimu. Ijulikane kuwa urasimu ni utaratibu wa kuendesha kazi za kiofisi kulingana na kanuni za kiutawala. Katika mchezo (tamthiliya) Hawala ya fedha kuharibika kwa urasimu kunatambulika kutokana na viongozi (makarani). Hawa hawafanyi kazi yao kama ilivyo. Hawakutaka kuendesha haraka mambo ya hawala ya fedha ya Ibrahim ili yeye awapatie rushwa.

#### *b) Ujinga*

Ujinga unatokana na tabia ya Ibrahim: kutojua kusoma, kukosa vitambulisho ambavyo ni mambo muhimu ya raia. Kwa ajili ya kutojua, ilimbidi Ibrahim kusomesha barua yake iliyohusu Hawala ya fedha. Habari hiyo ilipaswa kuwa siri lakini ilisambaa katika kijiji kizima kutokana na kuwa barua imesomeshwa.

**Dhamira ndogo**

- ***Mvutano baina ya vizazi*** (vijana mbele ya wazazi)

Mvutano huu unaelezwa na msichana mmoja aliyetukana Ibrahim baada ya kujionyesha mbele yake akitaka msaada na kunyimwa. Matusi yake yalienda pamoja na kumsingizia kuwa alitaka kumtongoza. Mvutano unaonekana pia kutokana na tabia ya Ambrozi aliyempiga Ibrahim badala ya kumpa picha zake. Alionyesha dharau kubwa mbele yake mzee.

- ***Nafasi ya mwanamke katika jamii***

Katika nchi nyingi za Afrika, mwanamke huonekana kama kiumbe duni. Mambo yanayokuwa vilevile katika Hawala ya fedha. Ibrahim anaonyesha dharau lakini wanawake hawa wanaonekana kuwa washauri wa nafasi ya kwanza wa mume wao.

AMNE anaonekana kujikomboa kutoka dharau hiyo. Katika kitabu hiki, wanawake wengine huonekana wakitaka kusitisha mambo ya rushwa.

- ***Nafasi ya fedha katika maisha ya kila siku***

Dhamira hii inajidhihirisha katika matukio mengi ya habari hii. Kusomesha barua lazima fedha, kutafuta vitambulisho ni fedha, picha, chakula, safari katika basi ni mambo hayo hayo. Inadhihirika kuwa watu wote wametekwa na tamaa ya fedha ili waweze kufanya shughuli zao mbalimbali. Mfano wa watu wanaotamani fedha kuliko wengine ni ISSA. Huyu anatumia hila ili aweze kuzipata.

**Migogoro**

Tamathiliya hii ina migogoro kadhaa ambayo inajitokeza katika jamii.

***Mgogoro wa kiuchumi*** ni wa kwanza kuonyeshwa. Mgogoro huu unaiathiri jamii kwa kiwango kikubwa. Wenye nacho wameonyeshwa kuwa ndio wanyanyasaji wakubwa wa watu wa chini. Mwandishi anaelekea kueleza kwamba si sawa kuwa na matabaka ya wafanyakazi na wafanyiwa kazi, yaani, mabwana na watwana (uk.38).

***Mgogoro mwingine unatokana na hali ya mazingira kati ya ukale na usasa***. Mwandishi anaelezea athari za kutojua kusoma na kuandika katika jamii. Kwa upande mmoja kuna watu wangependa kusoma, wengine hawataki.

**Ujumbe**

Tamthiliya ya Hawala ya Fedha ina ujumbe ufuatao:

- Ni vema kuwa na busara katika utekelezaji wa mambo.
- Elimu ni ufunguo wa maisha. Ni vema kuwa na tahadhari wakati wa matumizi ya fedha.
- Uvivu ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya jamii.

**Falsafa**

Hawala ya Fedha ni tamthiliya inayoonyesha falsafa ya mapambano dhidi ya unyonge. Msimamo wa mwandishi na falsafa yake juu ya maisha ni kuwa watu wasikate tamaa wanapokutana na matatizo. Utatuzi wa matatizo si wa siku moja, unachukua muda na hatimaye ushindi lazima upatikane.

## 18.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 6**

***Sikiliza tamthilia moja kutoka idhaa ya BBC kipindi Urunana au Indamutsa kutoka Radio Rwanda. Zungumzia fani na maudhui ya tamthilia hiyo na kuwasilisha kazi yako hadharani.***

## 18.6. Kuandika

**KAZI 7**

**Fanya uhakiki wa tamthilia ya Kijiba cha Moyo**

# SOMO LA 19: MFANO WA UHAKIKI WA HADITHI FUPI



## 19.1. Kusoma na Ufahamu: Kila Mtoto na Koja Lake

Rubyogo lilikuwa jina la kupanga la bwana Ndizihiwe. Wengine walikuwa wanamwita Nyangufi. Majina haya aliyapewa utotoni mwake alipokuwa na umri wa miaka mitatu. Asili ya jina hili ilielezwa na kimo chake: Ndizihiwe alikuwa mfupi sana na mwembamba. Aliyekuwa amemwona hakuwa anaamini kwamba siku moja mtoto huyu atafikia kuwa mtu mzima. Wazazi wake walikuwa wakiishi kwa mnung'uniko na fedheha katika kijiji cha Shengerero, Jimbo la Kusini nchini Rwanda.

Ntawiheba (kifupi cha Ntawihebagihumeka) na mkewe Bazubagira walikuwa wazazi wa Rubyogo. Huyu alikuwa mtoto wa pekee. Familia ya Rubyogo ilikuwa inaishi kwa kutegemea kilimo tu. Wakati mmoja wazazi wake walikuwa wakifurahia mavuno ya kilimo chao na wakati mwingine kulalamikia hali ya hewa. Mathalan, hali hii ya malalamiko ilikuwa ikijitokeza hususan wakati wa maafa.

Ntawiheba na mkewe walifanya bidii kwa kumlea ipasavyo mtoto wao. Walimpatia maadili toka utotoni hadi alipoanza elimu ya msingi. Ntawiheba na Bazubagira walikuwa wanapendana sana na kushirikiana katika kazi zote za kijamii. Majirani zao walikuwa wakiitamani familia yao. Aidha, Ntawiheba na mkewe walikuwa kielelezo cha familia yenye kuishi kwa amani na masikilizano.

Siku moja alipokuwa katika kazi ya kupalilia migomba, Ntawiheba alipata fursa ya kuwaza juu ya maisha ya familia yake kwa siku za baadaye. “Je, ni jambo la busara kweli kumzaa mtoto mmoja tu na tena mwenye ulemavu wa kimo?” Alijinung’unikia. Wazo la ukewenza lilimtawala sana na kumsumbua kupita kipimo.

Alipofika nyumbani jioni, mkewe alimkaribisha kwa chakula cha mchana lakini yeye alikipokea kwa shingo upande. Mkewe alipomtupia maneno ya utani, mumewe hakumwonyesha jino. Aliendelea kuonyesha hali ya kukasirika na kukosa furaha moyoni mwake. Hali hii ilimkera mkewe na kumsogelea, “Mume wangu mpendwa, mbona hali yako leo imenitisha? Ni balaa ipi iliyokufikia siku ya leo?”, mkewe alimbembeleza.

Ntawiheba alishindwa kuficha sababu za huzuni yake. “Mke wangu, miaka kumi na miwili imemalizika tangu siku yetu ya kufunga ndoa. Maisha tuliyo nayo leo unajua wazi haturidhiki nayo. Zaidi ya hayo, unaona jinsi mtoto wetu alivyo kimaumbile: mfupi mithili ya kinu! Unadhani kuwa Rubyogo atatufuta machozi kweli? Mimi ningependekeza nimwoe....” Anguka pa! Kabla hajakamilisha sentensi hii, mkewe alipatwa na mshituko na kuanguka chini kama mtu aliyepoteza fahamu. Mumewe huruma ilimwingia na kumhudumia kwa haraka. Alimwimbia wimbo mzuri sana wa kimapenzi, ule ule ulioimbwa siku ya ndoa yao. Punde si punde, Bazubagira alizinduka na kumwangalia mumewe machoni. Alimkumbatia na kuweka kichwa chake kifuani pa mumewe. “Mume wangu, ni shetani yupi aliyekutembelea leo? Kwa nini unataka nijitoe uhai kweli? Ni kosa gani nililokutendea kusudi uchukue uamuzi huo wa kuniletea mkemwenza wa kunitesa? Kwa nini hukubali kwamba mtoto ni sawa na mwingine hata akiwa na kasoro fulani? Mume wangu, kila mtoto na koja lake!”, Bazubagira aliongea kwa huzuni mno machozi yakimtoka machoni.

Ntawiheba alipigwa na bumbuwazi kisha akaangua kilio. Hali hii ilirudisha kumbukumbu ya ahadi aliyoitoa siku ya ndoa yao mbele ya mkuu wa wilaya pamoja na mbele ya kasisi kanisani. Hivyo, alimwomba mkewe msamaha na kumwahidi kutofikiria tena hata siku moja mpango mbaya ule.

Ndizihiwe alipoingia shule za sekondari alionyesha maarifa yasiyo ya kawaida. Toka mwaka wa kwanza hadi wa mwisho alikuwa akishika nafasi ya kwanza. Vilevile, alichaguliwa kuendelea na elimu katika chuo kikuuu huko Huye. Hapo alifanya maajabu zaidi! Mwishoni mwa masomo yake ilitangazwa nchini kote kuwa ndiye aliyejinyakulia shahada yenye alama za juu katika Kitivo cha Uhasibu.

Miaka michache baadaye aliajiriwa kama meneja mkuu katika kampuni moja ya kuagiza bidhaa kutoka nje za nchi. Ndizihiwe alionyesha ubingwa sana katika kazi yake na kuongezewa mshahara wa kuridhisha. Aliwajengea wazazi wake nyumba ya kisasa na akawanunulia gari zuri la kutembelea. Leo wazazi

wake Ndizihiwe wanaishi kwa kheri na fanaka wakifurahia kuwasimulia hadithi wajukuu wao wanne: Fany, Fils, Fiyette pamoja na Fisto. Katika masimulizi yao hawakusahau kusisitiza kuwa "Akiba haiozi" pamoja na "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo".

## KAZI 1

**Maswali ya Ufahamu**

1. Kifungu cha habari kinazungumzia nini?
2. Ni wahusika gani wanaozungumziwa?
3. Ndizihiwe alikuwa mtu gani?
4. Familia ya Ntawiheba na mkewe Bazubagira ilikuwa inaishi vipi?
5. Kwa nini Ntawiheba wazo la kumwoa mke mwingine lilimjia?
6. Ndizihiwe alikuwa na watoto wangapi?
7. Kichwa cha habari hii kimeoanaje na yaliyomo?

## 19.2. Matumizi ya Msamiati

## KAZI 2

***Jaza sentensi hizi kwa kutumia msamiati ufuatao: jina la kupanga, manung'uniko, fedheha, mtoto wa pekee, ukewenza, balaa, kinu, koja, kimo, kujitoa uhai.***

a) Kisamvu hutwangwa kwa kutumia..................................
b) Kila mtu hata rais wa jamhuri huwa amepachikwa ....................................akiwa mtoto.
c) Watu wanaotumia dawa za kulevya huishia kwenye uamuzi wa............ ..................................
d) Ufukara husababisha hali ya ....................na..................kati ya watu duni na matajiri.
e) Ilikuwa ni........................kwake! Alipoteza ng'ombe wanne na mbuzi wawili.
f) Rubyogo alikuwa hana dada wala kaka. Alikuwa.............................
g) Sheria, nchini Rwanda, haiungi mkono utamaduni wa............................ kwa ajili ya kupunguza mizozo katika jamii.
h) ..........................ni mtungo mrefu wa maua avishwao mtu kama zawadi au pambo.
i) Watu hutofautiana kimaumbile kulingana na ...............chao: kuna warefu, wafupi, wembamba, n.k.

## 19.3. Sarufi: Matumizi ya kirejeshi – o – katika Majina ya Ngeli ya U- na PA-M-KU

**KAZI 3**

***Soma sentensi zifuatazo. Bainisha kiambishi rejeshi kilichotumiwa na kueleza jinsi kilivyotumiwa.***

a) Uzalendo ambao una maana ni ule kutoka nchi asili.
b) Ushirikiano unaotakiwa kati ya mume na mke ndio utakaoimarisha uchumi wa nchi yetu.
i) Mahali paliposafishwa ndipo pazuri.
ii) Chumbani mnamoingia ndimo mnamolala.
iii) Mezani ambako kumewekwa vitabu kumesafishwa.

### Maelezo muhimu ya kuzingatia

Kiambishi rejeshi – o – kimehusishwa na majina ya ngeli za majina ya U- na PA-M-KU. Kimetumiwa kama ifuatavyo:

- Katikati ya kiambishi nafsi cha kitenzi na mzizi wa kitenzi.
- Kwenye mzizi wa amba- na ndi-
- Mwishoni mwa kitenzi

a) Uzalendo ambao una maana ni ule kutoka nchi asili.
b) Ushirikiano unaotakiwa kati ya mume na mke ndio utakaoimarisha uchumi wa nchi yetu.
c) Mahali paliposafishwa ndipo pazuri.
d) Chumbani mnamoingia ndimo mnamolala.
e) Nchini tunamoishi ndimo tutakamofanikiwa.
f) Mezani ambako kumewekwa vitabu kumesafishwa.

**KAZI 4**

**Weka sentensi zifuatazo katika kanushi au hali yakinishi**

i) Ni mahali papi panapotakiwa?
ii) Umaskini ambao utapigwa marufuku ni wa akilini.
iii) Shimoni ndimo nyoka huishi.
iv) Begani kulikojeruhiwa ni kupi?

## 19.4. Matumizi ya lugha: Uhakiki wa Hadithi Fupi

**KAZI 5**

***Soma hadithi fupi "Kila mtoto na koja lake" hapo juu na kuhakiki fani na maudhui yake.***

**MWELEKEO MUHIMU**

**UHAKIKI WA FANI**

1. **Wahusika na tabia zao**

**a) Wahusika wakuu**

***Ntawiheba*** pamoja na ***Bazubagira*** ndio wahusika wakuu katika hadithi fupi "Kila Mtoto na Koja Lake." Ntawiheba ni mume wa Bazubagira. Ametawaliwa na tabia ya ufoili: mwanzoni alikuwa amevumilia hali ya familia yake hivi akisikilizana na mkewe. Baadaye amebadilisha mawazo na kutaka kumwoa mwanamke wa pili. Mwishoni amekubali kushawishiwa na mkewe na kutulia. Ni mwanamume mwenye huruma, mapenzi na msanii pia. Ameonyesha sanaa yake wakati alipomwiimbia mkewe wimbo wa mapenzi ili asiendelee kupoteza akili.

Bazubagira ni mkewe. Yeye ameongozwa na tabia ya ubapa: habadiliki kimawazo na msimamo wake ni kumlea mtoto wao Ndizihiwe ingawa kimo chake kilikuwa kinaonekana kama kasoro. Ni mwanamke mwenye huruma na mapenzi: anatimiza ahadi la ndoa yake na mumewe.

**b) Wahusika wadogowadogo au wasaidizi**

***Ndizihiwe*** ndiye mhusika msaidizi. Mtoto wa pekee wa bwana Ntawiheba na mkewe Bazubagira, Ndizihiwe ametumiwa na mwandishi kuendeleza mtiririko wa visa au matokeo. Iwapo kimo chake kinazusha dukuduku au fedheha katika familia yake, Ndizihiwe ni mtoto mwenye akili. Amemudu masomo yake na kupewa vyeo. Ni mtoto mwenye mawazo ya kimaendeleo na ya kijamii.

2. **Mtindo**

Mwandishi ametumia mtindo wa nathari, yaani aya. Lugha iliyotumiwa ni ya kawaida, rahisi kueleweka. Baadhi ya vipengele vya lugha vilivyotumiwa na msanii kuna tanakali za sauti tamathali za usemi, nahau, methali.

**Tanakali za sauti**

Mfano: Anguka pa !

Konsonansi (mbinu ya kusawazisha konsonanti mwanzoni mwa neno) - Fils, Fiyette pamoja na Fisto.

**Tamathali za usemi**

a) ***Tashihisi*** (mbinu ya kupatia kitu kisicho hai sifa za kiumbe mwenye uhai (sifa za kibinadamu) - ni shetani yupi aliyekutembelea leo?

***b) Tashibiha*** (mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; 'kama', 'mithili ya', 'sawa na') - mfupi mithili ya kinu.

***i) Methali*** – Kila mtoto na koja lake; Akiba haiozi; Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

***ii) Nahau*** – kufanya bidii, kupokea kwa shingo upande, kuonyesha jino, kufunga ndoa, kufuta machozi, kujitoa mhanga, kupatwa na bumbwazi.

**3. Muundo**

Msanii ametumia muundo wa moja kwa moja, yaani hakufanya mazungumzo yanayoweza kutatanisha msomaji. Mtiririko wa visa na matukio muhimu umejitokeza kama ifuatavyo :

- Asili ya jina la Rubyogo
- Maisha ya familia ya Ntawiheba na mkewe Bazubagira
- Elimu na mafanikio ya Ndizihiwe
- Upeo: Hali ya kheri na furaha katika familia ya Ndizihiwe na wazazi wake.

**4. Mandhari**

Hadithi fupi imetokea katika kijiji cha Shengerero, jimbo la kusini nchini Rwanda.

**UHAKIKI WA MAUDHUI**

**Dhamira kuu**

**a) Haki za Watoto**

Mtoto yeyote anastahili kupewa haki zake zote za kimaisha hata akiwa na ulemavu. Ingawa Ndizihiwe alikuwa na ulemavu wa kimo alijiamini katika masomo yake pamoja na kazi zake na kufurahia baadaye matokeo mazuri.

**b) Maadili Mema**

Malezi bora kwa watoto huchangia kukuza akili na mienendo mizuri. Ndizihiwe alipata manufaa kutokana na maadili aliyopewa na wazazi wake.

**Dhamira Ndogo**

- ***Mapenzi ya ndoa***

Ntawigira na mkewe wasingelikuwa na mapenzi ya ndoa hawangelisikilizana baada ya Ntawigira kubadilisha mawazo yake ya kutaka kumwoa mke wa pili. Wimbo wa mapenzi aliomwimbia Bazubagira na kumfanya apate nafuu.

- ***Uwazi***

Mume na mke wanapaswa kuwa wazi katika mawasiliano yao ya kila siku. Jambo la Ntawiheba kutoboa siri la mpango wake kwa mkewe lilichangia kupata suluhu la mzozo uliokuwa umezuka.

- ***Ukewenza***

Dai la Ntawiheba kwamba kumwoa mke wa pili kutakuwa suluhisho la matatizo katika jamii yake lilibanwa na pingamizi ya sheria. Hivyo sheria katika Jamhuri ya Rwanda haikubali utamaduni wa ukewenza.

- ***Umuhimu wa elimu***

Baadaya ya kuhitimu masomo ya uhasibu katika chuo kikuu, Ndizihwe alipata kazi katika kampuni ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi. Alipewa mshahara wa kuridhisha akawajengea wazazi wake nyumba ya kisasa na akawanunulia gari la kutembelea

**Migogoro**

Hadithi fupi imeizingatia migogoro mbalimbali:

***Mgogoro wa kijamii:*** Kimo cha Ndizihiwe kilileta hali ya manung'uniko na fedheha katika jamii yake;

Hali ya maisha ilimfanya Ntawiheba akimbilie kwenye suluhu ya ukewenza.

***Mgogoro wa kisheria na kidini :*** Ahadi ya ndoa serikalini na kanisani ilikuwa kizuizi kwa uamuzi wa Ntawiheba kumwoa mke wa pili.

***Mgogoro wa kielimu :*** Mafanikio katika familia nyingi hutokana na kiwango cha elimu wanajamii walicho nacho. Mathalan, Ndizihiwe alifaidika katika maisha yake kutokana na elimu yake.

**Ujumbe**

- Watoto wote wanapaswa kuwa na haki sawa hata walemavu
- Wazazi wana jukumu la kuwapatia watoto wao maadili
- Elimu ni msingi wa maendeleo ya jamii.
- Mvumilivu hula mbivu.

**Falsafa**

Msimamo wa mwandishi na falsafa yake ni kwamba mtu yeyote, apende asipende, huwa na nguvu kama sifa pamoja na udhaifu kama kasoro. Kwa hiyo, litakuwa jambo la aibu kumnyima au kumnyanyasa mtu haki zake kwa kupitia vigezo vya kimaumbile, kiafya, kikabila, kidini, kijamii, n.k. Hakuna mtu anayeweza kuthubutu kudai kuwa huyu au yule atakuwa nini wakati ujao au atafaulu hiki na kushindwa kile. Pengine, si vizuri kuzubaika mno kwa maisha uliyonayo leo kwa sababu hujui kitakochotokea kesho au kesho kutwa.

## 19.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**KAZI 6**

***Sikiliza hadithi fupi "Usio" kutoka https://www.youtube.com/watch?v=qVUc1i22IjU. Zungumzia dhamira zake na kuwasilisha kazi yako hadharani.***

## 19.6. Kuandika

**KAZI 7**

**Tunga hadithi fupi wewe mwenyewe na kuifanyia uhakiki wa kifani na kimaudhui.**

## Tathmini ya Mada ya Nane

1. Eleza dhima za uhakiki wa kazi za fasihi andishi.
2. Jadili majukumu ya mhakiki wa kazi za kifasihi.
3. Unapofanya uhakiki wa riwaya au hadithi fupi kifani, ni mambo yapi ya kuzingatia?
4. Uhakiki wa kimaudhui katika riwaya, hadithi fupi pamoja na tamthilia huzingatia nini?
5. Jadili mambo muhimu ya kuzingatia katika uhakiki wa umbo la shairi.
6. Rejelea tamthilia "Ngoswe: penzi kitovu cha uzembe" kutoka https://www.youtube.com/watch?v=7UA1f3FEq6E. Itolee uhakiki wa kimaudhui.
7. Kwa kutegemea mifano, onyesha matumizi ya kiambishi rejeshi – o – katika sentensi.

## MAREJEO


Bakhressa,S.K. na Wenzake (2008). *Kiswahili Sanifu. Kitabu cha Mwanafunzi. Darasa la Saba*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Elgon Road, Upper Hill, Nairobi, Kenya.

Bakhressa, S.K. na Wenzake (2008). *Kiswahili Sanifu. Kitabu cha Mwanafunzi. Darasa la 8*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Elgon Road, Upper Hill, Nairobi, Kenya.

Hererimana, F. (2017). *Tujivunie Lugha Yetu. Kitabu cha Mwanafunzi, Kidato cha 5*. MK Publishers (R) Ltd. Kigali, Rwanda.

Kenya Literature Bureau (2006). *Kiswahili kwa Darasa la nane. Kitabu cha Wanafunzi*. Kenya Literature Bureau, Nairobi, Kenya.

Kihore, Y.M. na Wenzake (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Massamba, D.P.B. na Wenzake (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Ndalu, A.E. (2016). *Masomo ya Kiswahili Sanifu. Kitabu cha mwanafunzi. Kidato cha 2*. Moran (E.A) Publishers Limited.

Niyirora, E. & Ndayambaje, L. (2012). *Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi kidato cha tano*, Tan Prints (India) Pvt. Ltd.

Nkwera, F.M.V (1979). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo*.Tanzania Publishing House, Dar es Salaam,Tanzania.

Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 5*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.

Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 6*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.

Waititu, F. na Wenzake (2008). *Kiswahili Fasaha. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha tatu.* Oxford University Press, East Africa Ltd, Nairobi, Kenya.

TUKI (2004): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la pili*. Oxford University Press.